

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 18 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nancy H. Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa David Kihenzile.

Na. 253

### **Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mufindi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE K.n.y. MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi na kuanza kutumia Hospitali ya Wilaya ya Mufindi?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Siliinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi shillingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi shillingi milioni 300 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi shillingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu katika Hospitali ya Halmashauri. Hadi Aprili 2021, ujenzi wa majengo saba ambayo ni jengo la utawala, jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje kwa maana ya *OPD*, jengo la maabara, jengo la mionzi, jengo la wazazi, jengo la kuhifadhia dawa, jengo la kufulia umekamilika na ujenzi wa wodi ya watoto na wodi ya magonjwa mchanganyiko kwa wanaume na wanawake upo katika hatua ya upandishaji wa ukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga shillingi milioni 500 kwa ajili ya

ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Mufindi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji, jengo la kuhifadhi maiti na wodi ya upasuaji kwa wanaume na wanawake. Hospitali ya Wilaya ya Mufindi imeanza kutoa huduma za wagonjwa wa nje na inatarajiwu ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022 hospitali hiyo itaanza kutoa huduma kwa zaidi ya asilimia 90 ya huduma zote zinazotakiwa kutolewa katika ngazi ya Hospitali ya Halmashauri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nataka niullize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, hospitali hiyo iko mbali na makazi ya watu, ni upi mpango wa Serikali sasa katika kujenga makazi kwa ajili ya watumishi wa hospitali hiyo? (*Makofu*)

Mheshimiwa Spika, pili, ni upi mpango wa Serikali katika kutatua kero kubwa ya wataalam wa sekta ya afya katika zahanati na vituo vya afya vilivyopo katika Jimbo letu la Mufindi Kusini? (*Makofu*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya Mheshimiwa David Kihenzile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza hapa ni lini Serikali itajenga makazi kwa ajili ya watumishi wa afya wa Hospitali ya Halmashauri ya Mufindi. Nimueleze tu kwamba katika jitihada za Serikali, moja ya

jitihada kubwa ni kama tulivyoeleza katika jibu letu la msingi tumekuwa tukiongeza fedha kuhakikisha tunaboresha hospitali hiyo na kila mwaka tumekuwa tukitenga fedha. Kwa hiyo, nimueleze tu kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo kuanzia wodi, *OPD* pamoja na nyumba za watumishi kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi, Serikali ina nia njema kwenye suala hili na tutalifanya kazi ombi lake na siyo tu kwa Hospitali ya Wilaya ya Mufindi bali kwa nchi nzima katika vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusiana na kero ya wataalam, Serikali inaendelea na ajira na katika kipindi hiki Serikali itaajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya zaidi ya 2,600. Katika mgawanyo huo, sehemu ya watumishi hao tutawapeleka katika Halmshauri ya Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya kupangwa kwenye vituo vyake vya afya. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa changamoto zilizoko katika swali la msingi ni sawa na zilizoko katika Jimbo langu la Kinondoni katika Kata ya Makumbusho ambako kuna *dispensary* ilianza kujengwa tangu mwaka 2019 na ilikuwa imalizike Aprili, 2020, sasa hivi ni mwaka mmoja haijamalizika.

Pamoja na juhudzi za Manispaa kusimamia ujenzi ule na Mfuko wa Jimbo, je, Serikali haiwezi ikatia mkono sasa kuhakikisha kwamba *dispensary* ile inamalizika ili wananchi wa Kata ya Makumbusho, Jimbo la Kinondoni waweze kupata huduma? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Abbas Tarimba, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameionomba Serikali kuweka mkono katika Kata ya Makumbusho kwenye eneo ambalo limejengwa *dispensary* ambayo ilikuwa imepaswa kumalizika Aprili, 2020. Tunatambua jitihada kubwa zinazofanywa na Halmashauri ya Kinondoni hususan katika sekta ya afya, tunatambua kazi kubwa anayofanya Mbunge katika Jimbo la Kinondoni na tunatambua kazi nzuri inayofanya na Serikali kuboresha sekta ya afya nchini.

Kwa hiyo, tumelipokea ombi lake lakini tutaendelea kusitiza Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni sisi pamoja na wao kwa pamoja tuimalize *dispensary* hii ili wananchi waanze kupata huduma za afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 254

### **Barabara ya Kiloba-Njugilo**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Kiloba – Njugilo yenye urefu wa kilometra 7 itajengwa ili kurahisisha mawasiliano ya wananchi na wanafunzi wanaokwenda Kata ya Masukulu – Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge Viti Maalum, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kiloba-Njugilo ni barabara inayounganisha Kata mbili za Bujela na Masukulu. Kwa kutambua umuhimu wake, barabara ya Kiloba-Njugilo ipo kwenye hatua za uhakiki ili iweze kuingizwa kwenye Mfumo wa Barabara za Wilaya kwa maana ya *DROMAS* ili iweze kupatiwa fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo na ujenzi. Utaratibu wa kuingizwa kwenye mfumo wa barabara za Wilaya ukikamilika barabara hiyo itatengewa fedha kuititia fedha za Mfuko wa Barabara kwa maana ya *Road Fund* ili iweze kujengwa walau kwa kiwango cha changarawe na kuiwezesha kuititika katika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imejenga Daraja la Kigange linalounganisha Vijiji vya Kiloba na Mwalisi kwa gharama ya shilingi milioni 46.8.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa kukubali kuitengeneza barabara hiyo ya Bujela – Masukulu - Matwebe.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, ni lini Serikali itaisaidia Sekondari ya *Lake Ngozi* iliyopo Kata ya Swaya ambapo ni ngumu kufikika majira ya mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali inajipangaje kuhusiana na barabara zote na madaraja ambayo yanaunganisha kati ya barabara na shule ambapo imewafanya wasichana wengi washindwe kwenda shulenii

kutokana na mvua nyingi zinazonyesha zaidi ya miezi nane katika Wilaya ya Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu ni lini Serikali tutasaidia kujenga barabara inayoelekea Sekondari ya *Lake Ngozi* kuhakikisha inapitika ili kusaidia wanafunzi ambao wanatumia barabara hiyo ili iweze kupitika kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuahidi kwamba Serikali tunaendelea kutenga fedha kuhakikisha barabara hizo zinapitika kwa wakati wote na tunazingatia maombi maalum kama haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainishaa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu barabara na madaraja yote ni ajenda yetu sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* kuhakikisha safari hii tunayashughulikia. Ndiyo maana katika bajeti ambayo mlitupitishia hapa, moja ya malengo yetu makubwa na ya msingi sasa hivi ni kuhakikisha tunakwenda kujenga madaraja hususan katika yale maeneo korofi, kujenga mifereji pamoja na zile barabara ambazo hazipiti ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo ya barabara muda wote. Kwa hiyo, nimwambie tu kwamba akae mkao wa kutulia Serikali ipo kazini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Ramadhani Abeid.

Na. 255

**Barabara Zinazounganisha Vijiji vya Jimbo la  
Singida Kaskazini**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE K.n.y. MHE. ABEID R.  
IGHONDÖ** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za Singida Kaskazini zinazounganisha Vijiji ambazo hazipitiki kwa sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOÀ NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Singida Kaskazini ina mtandao wa barabara wenyewe urefu wa kilometra 811.68 ambaao umekuwa ukifanyiwa matengenezo pamoja na kujenga na kukarabati vivuko. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Singida ilifanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometra 78.55 na vivuko 22 kwa gharama ya shilingi milioni 739.39.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka fedha 2020/2021, barabara zenye urefu wa kilometra 67.8 na vivuko 20 vimetengenezwa kwa gharama ya shilingi millioni 711.08 ambapo hadi Machi, 2021 barabara zenye urefu wa kilomita 45 na vivuko 15 vimekamilika.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 barabara zenye urefu wa kilomita 62.5 na vivuko 24 vitajengwa kwa gharama ya shilingi millioni 711.08.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Halmashauri ya Wilaya ya Singida itafanya tathmini ya barabara zote za Singida Kaskazini ili kuandaa mpango wa namna bora ya kuweka vipaumbele vya ujenzi na matengenezo ya barabara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyogeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Singida Mjini kupitia Kinyeto hadi Sagala eneo la Kinyagigi linalouanganisha Kijiji cha Minyaa na Kinyagigi ilikatika kabisa na wakati wa mvua ilikuwa haipitiki ambapo maji hujaa inakuwa kama bwawa vile. Pia barabara inayotoka Makuro kuelekea Jagwa nayo pia ilikatika kabisa na ilikuwa haipitiki kutokana na utengenezaji wa chini ya kiwango. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hizi zinapitika wakati wote hasa wakati wa masika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Naibu Waziri yupo tayari kuambatana na mimi wakati wowote kuanzia sasa kwenda kutembelea jimbo zima kuona uhalsia wa barabara zake zilivyo hoi na ambavyo hazipitiki? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza upi ni mpango mkakati wa

Serikali wa kusaidia hizi barabara ziwe zinapitika wakati wote. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba Mpango Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakarabati, tunatengeneza na tunaanzisha barabara mpya ili kuhakikisha tunatoa huduma hiyo kwa wananchi kwa wakati wote. Ndio maana katika bajeti ambayo mmetutengea sasa hivi kuna ongezeko la fedha na kazi mojawapo ya hizo fedha zilizoongezeka ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kushughulikia barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara za aina tatu; za lami, changarawe na udongo na zaidi ya asilimia 80 za barabara zetu ni za udongo. Kwa hiyo, lengu letu sisi kwa awamu ya kwanza chini ya Rais wetu wa Awamu ya Sita ni walau tuifikie nchi nzima kwa kiwango cha changarawe kwa asilimia 50. Tukijenga kwa kiwango hicho cha changarawe na tukijenga na madaraja, naamini kabisa huu uharibifu ambaao unasababisha hizi barabara zisipitike wakati wote tutakuwa tumeutatua ikiwemo za Jimbo lake la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili la kuongozana naye, naomba kusema kwamba nipo tayari. Bahati nzuri nilishafika Singida Kaskazini, nafahamu miundombinu yake na changamoto zake na nilikwenda wakati ni msimu wa mvua. Kwa hiyo, tutarudi tena tukafanye kazi kwa sababu huo ndiyo wajibu ambaao tumedhamiria kuufanya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Changamoto ya wananchi wa Singida ni sawa na changamoto wanayopitia watu wa Kyerwa na hasa Kata ya Songambele, eneo la Kitebe ambalo wanazalisha sana mahindi lakini kuna changamoto ya barabara tangu lile eneo limekuwepo kwenye Kijiji cha Kitega. Nataka kupata *commitment* ya Serikali kuhakikisha wanaiunganisha hiyo Kitega na Kata nzima ya Songambele

ili tuweze kufanya biashara na Jimbo la Karagwe lakini pia na Rwanda kwa sababu ni mpakani mwa Rwanda pia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tunatambua mchango mkubwa ambao wamekuwa wakiutoa, tunatambua umuhimu wa barabara zote nchini na ndio maana tunaendelea kuongeza fedha na tumekuwa tukizitenga ili kuhakikisha kwamba tunazitengeneza na zinapitika. Hata wananchi wa Kitega katika hiyo Kata ya Songembele tutahakikisha tunawaunganisha ili kuwaondolea hiyo adha ambayo ina wakabili. Kwa hiyo, tutatafuta fedha ili tuzipeleke katika eneo husika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swalii la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kituo cha Afya pekee kinachotegemewa na watu zaidi ya 300,000 pale Vunjo ni cha Kilema. Kwenda kwenye kituo hiki, barabara iliyopo ni hiyo ya Mandaka – Kilema au barabara ya Nyerere. Sasa hivi barabara ile haipitiki kabisa, wagonjwa hawawezi kwenda kwenye kituo hiki cha afya. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, chonde chonde atoe tamko la dharura watu waende kushughulikia barabara hii. Nitashukuru sana akitoa tamko hilo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei ameelezea hiyo

barabara inayoelekea katika Kituo cha Afya Kilema kinachohudumia zaidi ya wananchi 300,000 kwamba haipitiki wakati huu na ameitaka Serikali itoe tamko. Niiagize *TARURA* kwamba waende wakafanye tathmini watuletee katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuweze kusaidia, tuone namna gani tunapata fedha na kuitengeneza hiyo barabara kwa dharura ili wananchi waweze kupita.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana.

Na. 256

### **Kuanza kwa Mradi wa *TACTIC***

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, ni lini serikali itakuwa tayari kuanza mradi wa *TACTIC* ili kufikia Malengo Makuu ya Serikali ya mwaka 2020 – 2025 katika kuboresha miundombinu ya barabara?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uendelezaji Miundombinu katika Miji (*TACTIC*) unatarajiwa kutekelezwa katika Halmashauri za Miji 45 nchini. Mradi unatarajiwa kutekelezwa na Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) kwa fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Serikali inaendelea na mazungumzo na Benki ya Dunia kuhusu upatikanaji wa fedha hizo na mradi utaanza

kutekelezwa baada ya kukamilika kwa majadiliano na fedha kutolewa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula, swalii la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kifupi sana uniruhusu. Ninafahamu kwamba mradi wa *TACTIC* ni mradi mbadala baada ya mradi wa *TSP*. Mradi wa *TSP* umekuwa mkombozi mkubwa sana kwenye nchi yetu kwenye miji, majiji na Serikali kwa pamoja. Utakumbuka hata ukiitazama Mbeya leo ukaitazama Mwanza, Tanga, na Manispaa nyingine za Kigoma, Ujiji na maeneo mengine, zaidi ya kilometra 457 zilijengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu toka Juni, 2019 barabara nyingi sana zilitangazwa na wakandarasi wakahitajika, wakajaza fomu ili wapate kazi. Sioni jitihada za Serikali ambazo zitatusaidia kuhakikisha barabara hizi zinatengenezwa kwa wakati. Barabara ziko nyingi, mfano ukienda hata Mbeya leo barabara ya kutoka machinjo ya llemi kwenda Mapelele inategemea fedha hizi ili ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda barabara ya Buswelu ambayo itakwenda kuunganisha soko la mbogamboga mpaka stendi mpya inategemea barabara hii. Barabara ya Mkuyuni kwenda Nyakato inategemea fedha hizi. Soko jipya la Kirumba linategemea fedha hizi. Hata ukienda kule kwa Mheshimiwa Ummy, barabara ambayo inakwenda Masiwani kwenda Hospitali ya Wilaya inategemea fedha hizi. (*Makofii*)

Sasa jitihada za Serikali za Serikali kuhakikisha fedha hizi zinapatikana: ni lini Serikali itahakikisha mradi huu unaanza mara moja ili fedha hizi zipatikane tuone matokeo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inafahamu kwamba *TARURA* haina uwezo wa kujenga barabara hizi bila fedha hizi tunazozitegemea leo zipatikane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa maswali muhimu ya majiji ya nchi hii. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali lake la kwanza la msingi Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula Mbunge alijaribu kuainisha umuhimu wa mradi huu wa uendelezaji wa miundombinu katika miji kwa maana ya *TACTIC* kwa kutaja maeneo mbalimbali ikiwemo katika Jimbo ambalo anatokea Naibu Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Ametaja Jimbo ambalo anatokea Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Jimbo lake Mheshimiwa Mbunge, Jimbo la Nyamagana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunatambua umuhimu wa barabara hizi na tunatambua umuhimu wa mradi huu. Ndiyo maana tumesema Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na hata katika ile miji yote ambayo imeainishwa kwenye huu mradi mtaona tumetuma wataalam katika kila Halmashauri, wameshafika huko kujadiliana mambo gani ya msingi yaingizwe katika huo mradi. Hiyo yote ni nia njema ya kuhakikisha kwamba huu mradi unakamilika kwa wakati. Ninaamini chini ya uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Hassan Suluhu; chini ya uongozi wa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Ummy Mwalimu jambo hili litakamilika kwa wakati na huu mradi utatekelezeka kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili amesema kwamba *TARURA* haina uwezo wa kuzijenga barabara hizo. Ni kweli, ndiyo maana tumekuja na huu mradi wa *TACTIC* kuhakikisha zile changamoto za barabara katika hayo maeneo yote yalijotajwa tunazitatu. Kwa hiyo, lengo letu ni kuhakikisha tukidhi vigezo, tumalize majadiliano na mwisho wa siku barabara zianze kujengwa kwa sababu hilo ndiyo lengo la Serikali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeenda sana. Mheshimiwa Sima, maswali yawe mafupi. Niwakumbushe tena, huna haja ya kulinganisha swali la msingi na unalotaka kuuliza, wewe nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Mussa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mradi huu wa *TACTIC*, Singida mjini pale unatarajiwu kujenga soko la kisasa la vitunguu, soko la Kimataifa. Pia, wananchi wa Singida Mjini wanataka kujua ni lini mradi huu utakamilika? Kwa sababu *feasibility study* imekwishafanyika. Sasa ni lini, ili waweze kuendelea na soko lao la Kimataifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama nilivyojibu katika maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana na ndivyo ambavyo nitamjibu Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mussa Sima, kwamba nafahamu kwamba kulikuwa na awamu ya kwanza ya majadiliano, sasa hivi tuko katika majadiliano awamu ya mwisho. Ndiyo maana katika sehemu ya huo mradi tumewatuma wataalam kuhakikisha wanaainisha maeneo yale muhimu yanayojengwa na mradi huu ni *component* ya mambo mengi ndiyo maana kuna masoko, barabara, kuna madampo ndani ya huu mradi wa *TACTIC*. Huu mradi utakapokamilika maana yake utasaidia mambo mengi ikiwemo mpaka kujenga stendi za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba awe na subira kwa sababu tuko hatua za mwisho na hii kazi itafanyika. Ondoa wasiwasi. Chini ya

Awamu ya Sita, barabara hizi zitajengwa, mradi huu utafika na wananchi wa Singida Mjini na maeneo yote ambayo yameainishwa katika huu mradi watafaidika na mradi huu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, swalii la nyongeza. Mheshimiwa Waziri naona umesimama. Ngoja aulize Mheshimiwa Mavunde, utajibu hili la Mheshimiwa Mavunde pamoja.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa mradi huu unaligusa pia na Jiji la Dodoma na kwa kuwa wataalam walishakaa na kuibua miradi hii kuanzia ngazi ya mtaa, kata mpaka Ofisi ya Rais, TAMISEMI:

Je, ni lini sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Fedha mtakaa pamoja mkwamue vikwazo vilivyopo ili wananchi waweze kunufaika na huu mradi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde kwa majibu mazuri, pia namshukuru Mheshimiwa Anthony Mavunde na mleta swalii, mtani wangu Mheshimiwa Mabula kwa swalii zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, tunatambua kwamba mradi wa TACT/C ni mradi wa kimkakati katika Halmashauri za Majiji na Miji 45. Serikali ya Awamu ya Sita kama alivyosema Naibu Waziri, tumeweka mradi huu kuwa ndiyo mradi wetu wa kielelezo katika kujenga miundombinu ya barabara, masoko pamoja na madambo ya taka katika miji 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swalii la Mheshimiwa Anthony Mavunde ni lini TAMISEMI tutakaa na Wizara ya

Fedha? Ndiyo maana nilitaka kusimama. Jumatatu ya tarehe 10 Mei, 2021 nilikaa mimi pamoja na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu kwenye Ofisi ya Wizara ya Fedha pamoja na wataalam wetu na tukakubaliana kwamba majadiliano yamekamilika, sasa tunapeleka *World Bank* kwa ajili ya taratibu za kusaini mkataba wa kuanza ujenzi wa mradi huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu mradi huu ni muhimu sana kwa Jiji la Mbeya, nafahamu mradi huu ni muhimu sana kwa Jiji la Arusha, nafahamu mradi hii ni muhimu sana kwa Jiji la Dodoma, pia ni muhimu sana kwa Jiji la Mwanza. Na mimi Tanga Jiji mradi huu kwangu ndiyo utanipa kura za kurudi Bungeni mwaka 2025.

Kwa hiyo, kutopatikana kwa *TACTIC* maana yake sitarudi Bungeni 2025. Kwa hiyo, naubeba kama mradi wangu, lakini na kwa Majiji mengine yote 45 tutahakikisha tunaanza utekelezaji mara moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Edward Kissi Olelekaita, Mbunge wa Kiteto sasa aulize swalii lake.

Na. 257

### **Kuongeza Muda wa Mkopo wa Matrekta ya *NDC* kwa Wakulima**

**MHE. EDWARD O. KISAU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango wa kupunguza bei na kuongeza muda wa mkopo wa Matrekta waliokopeshwa Wakulima wa Jimbo la Kiteto na Shirika la *NDC*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Matrekta wa *URSUS* unatokana na mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Poland, uliosainiwa tarehe 28 Septemba, 2015. Serikali ya Jamhuri ya Poland iliiteua kampuni ya *URSUS* na Serikali ya Tanzania iliiteua SUMA JKT kama watekelezaji na baadaye mradi huu ukahamishiwa Shirika la la Taifa la Maendeleo (*NDC*) kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkataba huo, Serikali ya Poland ilitoa mkopo nafuu wa dola za Kimarekani milioni 110 kwa riba nafuu ya asilimia 0.3 kwa mwaka, ukiwa na kipindi cha mpito cha miaka mitano na utarudishwa katika kipindi cha miaka 30. Lengo la mkopo huo ilikuwa ni kugharamia maendeleo ya Sekta ya Kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kupanga bei ya matrekta, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*), ilifanya uchambuzi wa gharama na kupanga bei kulingana na uchambuzi huo. Bei hizi zilipangwa kwa kuzingatia gharama za uagizaji, kutolea bandarini, kuunganisha na gharama nyininge za usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipanga bei nafuu ambapo wakulima wengi wanaweza kununua na kukopa matrekta hayo kutokana na mchango wake katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na kuzalisha malighafi za viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kurahisisha uuzaaji wa matrekta hayo, mkopo uliotolewa haukuwa na riba. Lengo kuu la Serikali siyo kupata faida, bali kuwawezesha wakulima kujikwamua kutoka kwenye matumizi ya jembe la mkono na kuongeza tija zaidi. Hivyo bei ya matrekta hayo kwa sasa inarejesha gharama tu za matrekta hayo pekee bila kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kurahisisha ulipaji wa mkopo kwa wakulima, kuanzia mwaka 2020, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) iliongeza muda wa kulipa mikopo kwa wakopaji ambao muda wa mikataba yao umeisha. Utaratibu unaofanyika ni kuwapa mikataba ya nyongeza wakopaji wote wa matrekta ya *URSUS* nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba ya nyongeza inahusisha bakaa ya deni na haitozwi riba. Utaratibu wa kupewa mikataba ya nyongeza unahusisha mkulima na Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) kwa kukaa pamoja na kufanya majadiliano ya namna mkulima atakavyolipa deni liliobaki. Zoezi hili limeshaanza kwa wakulima wa Kiteto katika kipindi hiki na linaendelea ili kuwafikia wale wote ambao muda wa mikataba yao umepita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Niseme tu kwa majibu pia ya Serikali ambayo ni  *fifty fifty* hivi, wakulima hawa wameanza kusumbuliwa sana na TAKUKURU. Wanakamatwa kila mahali na sijui kwa nini? Kwa sababu ni mkataba; sijui kosa la TAKUKURU linakujaje hapo! Niseme tu Mheshimiwa Rais wetu hapendi sana wakulima waonewe. Kwa kuwa, sasa Serikali imesema ilipata mkopo wa miaka 30, kwa nini wakulima hawa msiwape muda wa miaka 15 ili waweze kurejesha mikopo hii? Kwa sababu naamini ilikuwa ni nia njema sana, nami nimefanya vikao na watu wangu tarehe 10 Januari, 2021 na watu wa *URSUS* na kuna Wabunge wengi sana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wizara hii, Waziri na Naibu Waziri ni wapya, kwa nini wasitengeze kikao cha pamoja na Wabunge na watu wote wenye matrekta ili tuanze kujadili namna bora ya kuwasaidia wakulima hawa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa ufuatiliaji ambao anafanya ndugu yangu Mheshimiwa Olelekaita kuhusiana na wakulima wa Jimbo la Kiteto. Nachukua maoni yake mazuri, lakini kwanza kuhusu TAKUKURU kuwasumbua hawa wakulima waliokopa, naomba Serikali tuchukue nafasi hii kusema kuwa tutawasiliana kwanza na wenzetu kupertia *NDC* tuone ni nini kilikuwa kinatokea mpaka TAKUKURU wakaingizwa kwenye utaratibu wa kufuatilia mikopo hii ambayo iliingiwa na wakulima wale waliokopa matrektta na *NDC*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ulipaji wa mikopo hii kwa kuongezewa muda, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nalo hili tutalijadili kwa sababu ni mikataba ambayo iliingiwa na wakulima na walitoa wao wenyewe nafasi ya kulipa kulingana na uwezo wao. Kwa sababu ni nia njema ya Serikali kuhakikisha wakulima wanawezeshwa ili tuweze kupata mazao na malighafi za viwandani, basi tutakaa pia kupertia ili tuweze kuona namna gani tunawawezesha walipe kwa unafuu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kikao cha pamoja, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutakuja, tutakaa na ninyi, tutajadiliana na viongozi wote na hasa wakulima ambao wanatakiwa kusaidiwa kwa namna yoyote ile ili waweze kufanya kazi zao killimo kiwe na tija.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, swali la msingi nami pia nina wakulima kwenye jimbo langu la Hanang wanасumbuliwa vivyo hivyo; na malalamiko makubwa ya wakulima hawa ni ubora wa matrektta ambayo wamepewa na pia kukosa usaidizi pale ambapo matrektta haya yanaharibika, kwa maana ya matengenezo na matengenezo kinga na vipuri:-

Je, sasa Serikali iko tayari kuwasimamia hawa *NDC* pamoja na *URSUS*, kampuni iliyouza matrekta kuhakikisha kwamba matrekta haya yanahudumiwa kadri ya mikataba ya wakulima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na changamoto kidogo kwa baadhi ya wakopaji kwa wakulima ambao walikopa matrekta haya ya *URSUS* katika suala la ubora. Kweli suala la teknolojia ambayo ilikuja na matrekta haya kulikuwa kidogo kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara kuititia *NDC* tulishaligundua hilo na hivyo tumeshaanza kulifanyia kazi kuona namna gani tunaweza kuwa na utaratibu mzuri wa kuwasaidia ili matrekta hayo yanayopata changamoto ya ubora kwa maana ya utekelezaji wa dhana nzima ya kuhakikisha trekta lile linafanya kazi, tumeshaanza kuainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba wenzetu wa *NDC* wameshaweka utaratibu mzuri wa kuwa na mafundi maalum ambao watapita kuwasaidia wakulima wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na vipuri, ni kweli matrekta haya kidogo yalikuwa na changamoto ya vipuri kwa sababu ni mapya na ile kampuni ya *URSUS* ilikuwa bado inaendelea kuleta baadhi ya *spare*. Kwa hiyo, hili nalo tunalifuatilia kuhakikisha kwamba matrekta haya yanaendelea kuwa na vipuri ili pale ambapo yanapata hitilafu au yanaharibika, basi angalau vipuri vyaa kurekebisha hitilafu hizo vinapatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 258

### **Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa Liganga na Mchuchuma ili uweze kuchangia katika kukuza Uchumi wa Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unanganishi wa madini ya chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma uliopo katika Wilaya ya Ludewa, Mkoani Njombe ni mradi wa kimkakati na upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Aidha, mradi huo unategemea kutekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) ambalo litakuwa na 20% na Kampuni ya *Sichuan Hongda Group Company Limited* ambayo itakuwa na 80% ambayo ni kampuni ya China baada ya majadiliano kuhusiana na baadhi ya vipengele katika mkataba wa utekelezaji wa mradi huo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi huo, utafiti wa kina umeshakamilika na kubaini kuwepo kwa tani milioni 428 za makaa ya mawe katika eneo la Mchuchuma na tani milioni 126 za chuma katika eneo la Liganga. Aidha, uwekezaji katika mradi huo utagharimu kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za awali ambazo zimeshafanyika ni pamoja na utafiti wa athari za mazingira zitakazotokana na utekelezaji wa mradi huo pamoja na njia ya kupunguza athari hizo. Uthamini wa mali na fidia kwa wananchi watakaopisha mradi umeshafanyika, lakini pia, tumeshatoa elimu ya kujenga uwezo wa wananchi kuweza kutumia kiuchumi katika eneo la mradi (*Local Content*) pale ambapo mradi huu utaanza kutekelezwa. Pia, uboreshaji wa kilometra 221 za barabara kutoka Itoni, Njombe, hadi maeneo ya mradi na ukamilishaji wa utafiti wa reli ya kisasa kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay* na matawi yake kwenda hadi Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea na utekelezaji wa mradi huu, mwekezaji aliomba vivutio (*incentives*) ambavyo vilishindwa kutolewa na Serikali kwa sababu vinakinzana na baadhi ya sheria za nchi. Kwa sasa, Serikali ipo katika hatua za uchambuzi wa mradi na kujiridhisha zaidi kuhusu namna bora ya kutekeleza mradi huo ili kukidhi matakwa ya Sheria mpya Namba 5 na 6 za mwaka 2017 zinazolinda rasilimali za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uchambuzi huo, Timu ya Serikali ya Majadiliano (*Government Negotiation Team*) ilishaundwa na inaendelea kujadiliana na mwekezaji. Hivyo, utekelezaji wa mradi huo utaendelea mara baada ya kukamilika kwa majadiliano baina ya Serikali na Mwekezaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swalii la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi. Swalii la kwanza; uthamini wa mali na fidia ulifanyika tangu mwaka 2015, takribani miaka sita sasa wananchi wa Kata ya Mkoma Ng'ombe, Lwilo, Iwela pamoja na Mundindi hawajalipwa fidia hii ya bilioni 11.

Je, Serikali haioni kwamba, kuchelewesha kulipa fidia kwa wananchi hawa kutaiingizia Serikali gharama kubwa kwa sababu, nina wasiwasi isije tathmini hii ikaja kushuka thamani

kipindi hicho wao watakachokuwa wanataka kuwalipa wananchi hawa fidia hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa kumekuwa na uhitaji mkubwa sana wa makaa ya mawe na *NDC* wamechukua vitalu vyote nya makaa ya mawe. Je, Serikali haionti umuhimu wa kutoa baadhi ya vitalu kwa wananchi wachimbaji wadogowadogo wazawa ili wawewe kuchimba na kuweza ku-stimulate uchumi? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, uthamini wa mali kwa ajili ya kulipa fidia ili kupisha kuendelea kutekeleza mradi huo ulifanyika mwaka 2015 na kweli wakati ule thamani ya fidia iliyokuwa imeainishwa ni bilioni 11.03.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba, utekelezaji wa mradi huu bado uko kwenye majadiliano. Moja ya vipengele ambavyo viko kwenye majadiliano ni kuona namna gani mwekezaji ambaye atapatikana atawezekana kulipa fidia ambayo illainishwa, lakini pia baada ya kupitiwa kutokana na hali halisi ya sasa itabainika. Kwa hiyo, ulipaji wa fidia huu nao ni sehemu ya majadiliano ambayo tunaona kwamba, mwekezaji ambaye atapata nafasi sasa kuwekeza katika eneo hili yeze pia atahusika katika kulipa fidia ambayo ilibainishwa kwa ajili ya wananchi kupisha mradi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitalu nya makaa ya mawe ambavyo vinasimiwa na *NDC*; naomba niwahakikishie kuwa ni kweli vitalu hivi kwa ajili ya maendeleo ya nchi *NDC* ndio inasimamia uendelezwaji wa uchimbaji katika maeneo hayo, lakini kwa ajili ya maendeleo endelevu mambo haya au biashara hizi za uchimbaji zinakwenda

kibashara zaidi. Kwa hiyo, wananchi au ambao wana uwezo kama wafanyabiashara au wawekezaji ikiwemo wananchi wa maeneo hayo wanaweza kwenda kuomba nafasi ya kushiriki katika maendeleo au uendelezaji wa uchimbaji wa makaa ya mawe katika vitalu hivi kwa kushirikiana au kupata vibali kutoka Shirika letu la Maendeleo la Taifa (*NDC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawakaribisha na kama watakidhi vigezo na kuweza kuwa na mitaji stahiki ya kuwekeza katika maeneo haya, nadhani hakutakuwa na shida, tunawakaribisha na shirika letu liko kwa ajili ya kusaidia Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza na nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Neema Mgaya kwa swali zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu ni lini Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara atakwenda kufanya mikutano na wananchi wa Mundindi kwa maana ya Liganga na Nkoma Ngo'mbe kwa maana ya Mchuchuma, ili kuweza kuwaeleza juu ya maendeleo ya mradi huu pamoja na kutoa kalenda ya utekelezaji wa miradi hii ili Waziri wa Ujenzi naye aweze kuona umuhimu wa kuweka miundombinu? Kwa sababu, mradi huu kielelezo na barabara zinapaswa ziwe za vielelezo kwa hiyo, kuna barabara inayotoka Mkia – Mavanga – Madaba kwa kaka yangu Mheshimiwa Mhagama na hii Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda nazo zinaendana na miradi hii. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, basi Mheshimiwa Waziri amesimama.

Sasa Mheshimiwa Waziri kabla hujajibu hilo swali la Mheshimiwa, nadhani pia ni fursa ya kuwaeleza Watanzania

kwa sababu, Mheshimiwa Rais nadhani alielekeza TAKUKURU ifanye majukumu yake na sio kazi yake kukusanya madeni. Sasa hapa kuna swali linalohusu wakulima ambao wanaumbuliwa na TAKUKURU wakati wanakusanya madeni ya matrektta.

Kwa hiyo, nadhani upate fursa ya kuyazungumzia mambo hayo mawili pia. Lile swalii la Mheshimiwa Kamonga na hiyo hoja ya TAKUKURU kukusanya madeni wakati Mheshimiwa Rais alishakataza.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza, moja hilo ambalo umelileta la TAKUKURU na hili la Mheshimiwa Kamonga ambalo ameliuliza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimepanga kutembelea mradi huu mara baada ya bajeti yetu, Ijumaa. Katika ratiba zangu moja ya *weekend* nitatembelea mradi huu na tutazungumza na wananchi kwa ajili ya kuwapa maendeleo. Kwa kweli, katika bajeti yetu ambayo tutaitoa wiki hii tutaeleza kwa kina zaidi hatua ambazo zimefikiwa katika utekelezaji wa mradi huu na lini hasa utaanza. Kwa hiyo, nitafurahi sana Mheshimiwa Mbunge tukifuatana tukaenda kuzungumza na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la TAKUKURU. Naomba nilichukue hilo, tulifanyie kazi, tupate *details* hasa TAKUKURU wanafuatilia nini na katika mazingira yapi, ili tuweze kutoa jibu ambalo linaleweka. Kwa sababu, kwa kweli, sina *details* za kutosha kuhusu TAKUKURU wanawakamata wananchi na kuwahoji katika masuala yapi hasa. Kwa hiyo, tunaomba tupate nafasi tulifuatilie tupate *details*, ili tukitoa jibu hapa tutoe jibu ambalo linaleweka. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, sasa aulize swali lake.

Na. 259

**Kutoa Hati kwa Wananchi wa Kata za Kibamba,  
Kwembe, Mbezi, Msigani, Goba na Saranga**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa Hati katika Mradi wa Urasimishaji kwa Wananchi wa Kata za Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani, Goba na Saranga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angelina Mabula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kurasimisha na Kuzuia Makazi Yasiyopangwa Mijini, programu ambayo ilianza 2013 na inakwenda kwisha 2023 katika maeneo mbalimbali nchini. Kuanzia mwaka 2015, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipanua wigo wa kushirikisha sekta binafsi kufanya kazi za urasimishaji ambapo jumla ya kampuni 163 za upangaji na upimaji ardhi zilisajiliwa zimevezesha kuandaa michoro ya urasimishaji 3,832 na jumla ya viwanja 1,638,062 katika mamlaka za upangaji 134. Kampuni hizi zinafanya kazi kwa kuingia mikataba na wananchi kuititia Kamati za Urasimishaji za Wananchi Nchini na kuratibu wa mamlaka za upangaji kuchangia gherama za urasimishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata sita za Saranga, Mbezi, Goba, Kwembe, Msigani na Kibamba, jumla ya wananchi 30,216 wamechangia gherama za upangaji na

upimaji kati ya wananchi 147,299 walio tegemewa kuchangia. Aidha, Kampuni za urasimishaji kwa kushirikiana na Serikali zimeandaa michoro ya Mipangomiji 384 yenye viwanja 141,881 ambapo kati ya hivyo, viwanja 8,316 vimepimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na kutoa hati katika viwanja 8,316 ambavyo upimaji wake umekamilika katika Kata ya Kibamba, Kwembe, Mbezi, Msigani, Goba na Saranga ambapo mpaka sasa kuna jumla ya hati 1,754 zilizoandaliwa kati ya maombi 1,925 yaliyowasilishwa. Serikali pia imekwishaandaa ankara 2,889 na kusambaza kwenye mitaa ya Kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna changamoto ya wananchi kutolipa ankara zao kwa wakati ili kuchukua hati zilizoandaliwa. Hivyo tunawasihi wananchi wa maeneo hayo kulipia gharama za umililikishwaji ili waweze kupewa hatimiliki. Vilevile kampuni zilizopewa kazi ya urasimishaji kukamilisha kwa wakati kazi walizopewa kwa kuzingatia mwongozo wa urasimishaji uliotolewa na Wizara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu yaliyotolewa na Serikali yanayoridhisha kwa wastani, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, majibu ya Serikali yanaeleza wazi juu ya utoaji wa hati 845 tu kati ya upimaji uliokamilika wa watu 100,041 asilimia 0.0056 katika kipindi chote cha miaka miwili. Je, Serikali haionti sasa ni muda sahihi wa kupunguza lile tatizo la *premium* ambalo linasababisha bei kubwa kwa wananchi ambao wanashindwa zaidi ya ile 180,000 ambayo wamelipa kwa wale wa kampuni? Sasa hapa ni kupunguza ile *premium*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni kweli kwenye majibu ya msingi inasema wachangiaji ni 30,000, lakini kwa taarifa nilizonazo kama Mbunge ni zaidi ya wachangiaji

80,000. Kwa hiyo, jumla ya fedha ni bilioni nne wanazisema, mimi nasema bilioni 15. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kupeleka Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ili akafanye ukaguzi maalum tuje na takwimu zilizo sahihi kwa ajili ya fedha za wananchi zilizopotea? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimsahihishe, si kweli kwamba, hati 847 tu ndio zimeandaliwa. Kwenye jibu langu la msingi nimesema hati 1,754 katи ya waombaji 1,925 tayari zimeandaliwa na wamechukua, lakini tunaendelea kuandaa hati kwa sababu, viwanja vilivyokamiliika ni 8,316 kwa hiyo sio 845 kama alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumzia suala la kupunguza *premium* kwamba, pengine wananchi wanashindwa kuchangia. Naomba tukumbuke tu kwamba, *premium* hii awali ilikuwa ni 15% kwa viwanja vyote. Ikapungua ikawa 7.5%, lakini badaye Wizara ikapunguza zaidi kwenye zoezi la urasimishaji wanalipa 1% ya *premium* ambayo wanatakiwa kulipa tofauti na ule upangaji wa kawaida, ilitoka 7.5% wao wanalipa 2.5%. Kwa hiyo, kama ni suala la kupunguza ni kweli upunguzaji tumepunguza, lakini kwa sababu ni hoja inatolewa na Serikali ni sikiu basi tutaona namna kama kuna haja ya kupunguza tena au tuendelee na ileile 1%. Tukumbuke kodi hizi pia ndio zinarudi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili amezungumzia kwamba, pesa ambazo zimekusanya tulizotoa takwimu hapa ni tofauti. Si kweli anachosema, kwa mitaa mitano haiwezi kukusanya bilioni 15 kwa zoezi la urasimishaji, ukizingatia kwanza walipaji wenyewe ni wachache na

nimetaja kati ya waombaji 147,000 tunaoshughulika nao sasa hivi ni 1,925 tu ambao wamekamilisha malipo yote. Kwa hiyo, si kweli kwamba, kuna pesa nyingi ambazo zipo,

Mheshimiwa Naibu Spika, kama pengine Mheshimiwa Mbunge anajua kuna mahali ambapo kuna pesa zimekusanywa na pengine hazijulikani zilipo, ameomba ukaguzi ufanyike, tutalifanya kazi ili tuweze kujua ukweli wa Mheshimiwa Mbunge aliouleta na takwimu tulizonazo Wizarani ili tuweze kuwa na uhakika na alichokisema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani mnaona muda wetu unavyokwenda. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 260

#### **Hitaji la Kivuko Ruvuvu – Ngara**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Kivuko katika Mto Ruvuvu ili kuunganisha Vijiji vya Mayenzi na Kanyinya vilivyopo Wilayani Ngara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuendelea kuboresha huduma za usafiri kwa njia ya maji ikiwa

ni pamoja na kuunganisha maeneo yenye mahitaji ya vivuko ikiwemo Mayenzi na Kanyinya kila inapopata fedha. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Sekta ya Ujenzi, ilitenga fedha kwa ajili ya kujenga maegesho ya Mayenzi na Kanyinya, ili iweze kupeleka kivuko ambacho kitaunganisha wananchi wa maeneo hayo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maegesho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wakala wa Ufundı na Umeme Tanzania (*TEMESA*) uko kwenye hatua za ununuzi wa kumpata mkandarasi wa kufanya ujenzi wa maegesho ya kivuko hicho na mkandarasi wa kufanya ukarabati huo chenye uwezo wa kubeba abiria 60 na magari mawili ambacho hapo awali kilikuwa kinafanya kazi eneo la Rusumo – Nyakiziba, yaani *MV Ruvuvuya* zamani, ambacho kwa sasa kimeegeshwa katika Mto Ruvuvu. Baada ya ukarabati huo kukamilika, kitatoa huduma kwenye eneo la katı ya Mayenzi hadi Kanyinya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swalı la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mto Ruvuvu una tabia ya kujaa, hali inayoweza kusababisha kivuko hiki kutofanya kazi, hasa nyakati za masika; na kwa kuwa vivuko hivi vina tabia pia ya kupata hitilafu, hali ambayo inasababisha huduma ya kuvusha wananchi isiwepo. Swalı la kwanza; je, Serikali iko tayari kutuletea mtumbwi wa kisasa ili uweze kutoa huduma pindi ambapo kivuko kitakuwa hakiwezi kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na mimi twende kwenye Jimbo la Ngara akashuhudie changamoto zetu za vivuko pamoja na miundombinu mingine, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Waitara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA**

**M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nihampongeza kwa swali lake zuri kwa sababu anatu-*alert* kwamba tunapojenga vivuko tuweke pia na mitumbwi kama *backup* ikitokea tatizo tuweze kupata huduma katika maeneo hayo. Naomba nimuelekeze Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi atume wataalam wetu waende katika eneo hili la Mto Ruvuvu akafanye tathmini tujue aina ya mtumbwi na gharama zake ili tuweze kupeleka huduma hii muhimu katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndaisaba kwamba kwakuwa ni mjukuu wangu nitaenda pale Kagera kutembelea Ngara katika eneo hili baada ya Bunge hili kumaliza Bunge la Bajeti, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi sasa aulize swali lake.

Na. 261

**Mkakati wa Kusambaza Maji ya Mto Diburuma**

**MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaanza mkakati wa kusambaza maji kutoka Mto Dibuluma kata ya Kibati Wilaya ya Mvomero na kuyasambaza katika kata ya Tunguli, Kwekivu, Masagal na Songe Wilayani Kilindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa *Engineer Mahundi* majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa niaba wa Waziri wa Maji naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa muda mrefu wa kutekeleza mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha mto Diburuma kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi. Hatua iliyofikiwa ni kufanyika kwa utafiti wa ubora na uwingi wa maji katika chanzo hicho ili kujiridhisha na kiwango cha maji kwa ajili ya kunufaisha vijiji vilivyopo kwenye kata nne (4) za Tunguli, Kwekivu, Masagalu na Songe. Utafiti huo utakamilika kabla ya mwezi Juni, 2021 na takwimu zitakazopatikana zitatumika kufanya usanifu wa kina kwa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kata za Tunguli, Kwekivu, Masagalu na Songe zinapata huduma ya maji safi na salama kupitia visima virefu vitano (5) na visima vifupi kumi na tano kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma ya maji katika kata hizo na Halmashauri ya Kilindi kwa ujumla, na mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 2.14 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake wa maji kwa kututengea kiasi cha shilingi bilioni 2,146,000,000 kwa ajili ya huduma kwa watu wa Kilindi, baada ya shukrani hiyo ningependa tu nimuulize swali moja tu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya kwamba wanafanya tafiti na tafiti hiyo itatoa majibu ndani ya mwezi ujao, sasa nataka tu kupata *commitment* ya Mheshimiwa Naibu Waziri je, wananchi wa Wilaya ya Kilindi wategemee nini kuhusiana na uhakika wa mradi wa huu ambao utahudumia zaidi ya vijiji 12? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa *Engineer Mahundi* majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kupokea pongezi zake kwangu pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa hakika tunashirikiana vema na wewe pia nikupongeze kwa sababu unatupa ushirikiano mzuri na tutaendelea kufanya kazi bega kwa bega kuhakikisha suala la maji tunakwenda kulitatua kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na lini sasa *commitment* ya serikali kwenye Mradi huu wa Diburuma ni kwamba tayari kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi utafiti unaendelea na hivi punde mwezi ujao tunakwenda kukamilisha usanifu hivyo kutokana na ghamra ambayo itapatikana sisi kama Serikali tumejipanga kuhakikisha kutumia chanzo hiki tukiamini kabisa kitakuwa ni chanzo endelevu na sehemu kubwa zaidi ya vijiji 10 ninafahamu zitapitiwa kwa hiyo tutaendelea kushirikiana kuona kwamba chanzo hiki tunakwenda kukutumia tutakitafutia fedha ili kuona kwamba tunatimiza azma ya kuleta maji.

**NAIBU SPIKA:** Tumalizie Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa sasa aulize swali lake.

Na. 262

#### **Ucheleweshwaji wa Malipo ya Wakulima wa Kahawa**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa Wakulima wa Kahawa ndani ya muda mfupi pale wanapomaliza kupima Kahawa zao kwenye *AMCOS*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate Mbunge wa Kyerwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto za mfumo wa soko Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kurejesha ununuzi wa mazao matano ya kimkakati kupitia vyama vya ushirika ili kunufaisha wakulima, wanunuzi na wafanyabiashara na Serikali kwa ujumla. Uamuzi huu ulikuwa ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 iliyoelezwa katika sura ya 2 Ibara ya 22 kuviiimarisha na kuviwezesha vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mfumo wa soko la Kahawa Serikali hainunui kahawa bali imeweka mfumo wezeshi kwa wakulima kuuza mazao yao kupitia mfumo wa Ushirika ambapo wanunuzi binafsi wameruhusiwa kununua kahawa kupitia vyama vya Ushirika, kwa maana ya vyama vya msingi mwongozo wa bodi ya kahawa unaelekeza kuwa Wakulima walipwe ndani ya siku tatu pindi *AMCOS* inapofanya makubaliano ya Kampuni yenyewe leseni ya wanunuzi binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha vyama vya Ushirika vimeshauriwa kutafuta masoko mapema ili kuwezesha kupata fedha kutoka taasisi za *TADB* au wanunuzi wanaoingia nao mkataba ili kuwezesha kulipa wakulima pindi wanapoleta kahawa kwenye vyama vyao vya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza nisikitike kwa kusema majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri sijaridhika nayo kwa sababu yeye anasema Serikali inaelekeza wananchi walipwe baada ya siku tatu, hili jambo si sawa wananchi wamekuwa wakikaa zaidi ya miezi mtatu hawajalipwa. Kwa hiyo,

mnapoleta majibu kwanza myafanyie utafiti, swalii la kwanza, Je, Serikali kama msimamizi mkuu wa Ushirika ipo tayari kushirikiana pamoja na vyama vikuu vya Ushirika ili wanapokwenda kuomba hii mikopo Benki waweweze kupewa haraka ili kuondoa adha ambayo wanaipata wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili Serikali baada ya kuruhusu wanunuvi binafsi je, ni utaratibu upi ambaaimeeuweka ili huyu mnunuzi binafsi kahawa yake aipate ikiwasalama lakini pia huyu mkulima apate fedha yake kwa wakati? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Bilakwate kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu mikopo ambayo tumekuwa tukisaidia katika vyama vya Ushirika ambavyo vimesaidiwa na Serikali kwa kipindi cha miaka miwili, mitatu mfululizo ni vyama vya *KDCU* ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka, Serikali ilikichukua chama hiki kikiwa kina deni la zaidi ya bilioni saba Serikali *ika-develop a bailout system* na kukifanya chama hiki sasa hakidaiwi hata shillingi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo tunawasaidia na ni vyama vya *KCU* na *KDCU* tumewasaidia kuititia Tanzania *Agricultural development Bank* na msimu uliopita wamepata jumla ya bilioni 23 kwa ajili ya *ku-aggregate* kahawa kutoka kwa wakulima na wamepata kwa *interest* ya asilimia 9. Ndio vyama pekee ambavyo katika ukanda ule, pamoja na matatizo ya korona wakulima wa Kagera walipata bei bora zaidi ya kahawa yenye maganda kuliko kahawa ya wakulima wa nchi ambazo zimekuwa jirani na sisi. Wakati wenzetu wakipata wastani wa Shilingi 700 hadi 800 kahawa ya Kagera ilinunuliwa kwa shilingi 1,200 kwa usimamizi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu na nitumie Bunge hili kuwaambiya Waheshimiwa Wabunge wa Kagera wiki liliyopita tumekaa na vyama vikuu vya Ushirika vya *KDCU*, *KCU*na makampuni binafsi. Mpaka sasa ni makampuni saba yameonyesha interest ya kununua kahawa katika vyama vya Msingi, na ninarudia hatutowaruhusu kwenda kwa mkulima mmoja mmoja wataenda kwenye vyama vya msingi na sasa mikataba itakuwa *tripartite* itasainiwa na Chama cha Msingi, itasainiwa na Mkulima, itasainiwa na Chama Kikuu lakini chini ya usimamizi wa Bodi ya Kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu mnunuzi anataja bei anayonunulia na kiwango anachohitaji na atakapochukua kahawa kutoka kwenye chama cha Msingi nilazima alipe ndani ya muda usiozidi masaa 72 hayo ndio maelekezo ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali kutoka kwa wabunge lakini majibu kutoka kwa Serikali kwanza nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele tangazo la kwanza ni la wageni ambaao wapo humu Bungeni. Kwanza ni wageni watano wa Mheshimiwa Kenneth Nollo kutoka Uongozi *Institute* wakiongozwa na Meneja Maarifa kwa Umma ndugu George Nchimbi, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Omari Kigua ambaao ni wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Kilindi Mkoani Tanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Kata, sijajua ni kama gani lakini ndugu Mnhambo Kadugu, sijui wamekaa upande gani hawa pengine hawajapata fursa ya kuingia. Lakini pia wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Arumeru Magharibi Mkoani Arusha wakiongozwa na Ndugu Justin Miredo, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Arumeru Magharibi Mkoani Arusha wakiongozwa na Ndugu Noel Saning'o karibuni sana. Tunao pia wageni wawili wa

Mheshimiwa Taska Mbogo ambao ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbulu ndugu Anna Mbogo na Ndugu Suzan Eng'wenyu, karibuni sana. Tunao pia wageni saba wa Mheshimiwa Jafari Chege ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Dodoma wenyeji wa Jimbo la Rarya Mkoani Mara wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Emmanuel Magige, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ambao ni wanafunzi wa chuo kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu John Obotto, karibuni sana, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato David Chumi ambao ni ndugu zake waliopata msamaha wa Rais kutoka Gereza la Nyabula Mkoa wa Iringa na hawa ni ndugu Yohana Changala na Ndugu Gervas Kafunde, karibuni sana. Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Samwel Hhayuma ambao ni wakulima wanaotumia matrekta ya *ULSUS* kutoka Hanang Kiteto Mkoa wa Manyara wakiongozwa na ndugu Jeremia Mahina karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni 29 wa waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Irene Ndyamkama, Mheshimiwa Janejelly Ntate na Mheshimiwa Fredy Mwakibete ambao ni wachungaji wa Injilisti na wanamaombi kutoka jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Cordnad Sayi, karibuni sana, tunao pia wageni 36 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni viongozi na wachezaji wa Timu ya Wananchi... (*Makofi/Vigelege*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hakuna kitu, hakuna kitu hao.

**MBUNGE FULANI:** tumewabeba!

**MBUNGE FULANI:** Vyura FC!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walishangalia)*

**NAIBU SPIKA:** Haya Waheshimiwa Wabunge mmeshasikika! (*Vigelegele*)

**MBUNGE FULANI:** Subirini tarehe walikimbia mechii hao.

**WABUNGE FULANI:** CCM, CCM! Ndoo!

**NAIBU SPIKA:** Sasa tusubiri kwanza tumalize kusoma tangazo wageni 36 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni viongozi na wachezaji wa Timu ya Wananchi Yanga *Sports Club* wakiongozwa na kiongozi wa Timu hiyo Eng. Hers Said sasa Mnawea kusimama maana tangazo... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Walikimbia Mechii.

**NAIBU SPIKA:** Haya sawa! Sasa msikilize kidogo Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo mkiwa bado mmesimama nadhani mmeputa picha namna ambavyo wabunge wapo pamoja nanyi mnafanya vizuri. (*Makofi/Vigelegele*)

Sasa jana walikuja hapa wachezaji wa Simba *Queens* nadhani tukubaliane nyie wenye nchi naona mmeshindwa makofi kwa hiyo, wamewashinda Yanga hilo tukubaliane sasa tusikilizane sasa sisi tunatamani timu zetu ziendee kufanya vizuri hapa ndani ya nchi lakini pia nje ya nchi na ninaamini ujio wao na makofi ya Waheshimiwa Wabunge yanaashirika kwamba timu yetu itakapokwenda nje ambayo hiyo nafasi wameipata kupitia simba mambo yatakwenda vizuri sana. (*Makofi/Vicheko*)

Kwa hiyo, timu zetu zinafanya vizuri na sisi tunatamani Simba inapokwenda nje ifanya vizuri na Yanga itakapokwenda nje pia ifanya vizuri kwa hiyo timu zote zifanya vizuri Taifa lisonge mbele, ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wasikimbie mechii, wasikimbie mechii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa hilo lifike mwisho nadhani tumeshakubaliana hapa kwamba Yanga humu ndani wametisha. (*Makofi*)

Sasa kanuni ya 53 Waheshimiwa Wabunge inahusu maswali kujibiwa kikamilifu kumekuwa na utaratibu wa Waheshimiwa Wabunge wakipewa majibu na Serikali kusema kwamba sijaridhishwa na majibu ama majibu haya hayajajibu swali lake na namna hiyo pengine ni lugha ambayo tumeshaizoea zoea sasa hivi. Lakini kanuni zetu zinataka ukitaka kusema hoja ya namna hiyo lazima uiseme kwa namna ambayo kiti kitardhika kwamba Serikali hajajibu swali ili ipewe nafasi ya kuja kulijibu hilo swali upya.

Kwa hiyo, hiyo kauli isizoeleke kwamba ni kawaida tu kuiambia Serikali kwamba swali ulilokuwa umepeleka kwa niaba ya wananchi wako halijajibwa kikamilifu yaani hiyo kauli inaonesha Serikali haifanyi vile ambavyo inapaswa kufanya kwa Wabunge amba ni wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, niwaombe sana tunapoitumia kauli hii basi utoe maelezo mahsus ambayo kiti kitaweza kutoa maamuzi kwamba hilo swali lirudiwe kujibiwa, tusjaribu kuonesha kana kwamba lazima kila Mbunge aseme sijaridhika labda ndio anaonekana amewakilisha sana wananchi hapana ndio maana unapewa fursa ya kuuliza swali la nyongeza ili kama kuna jambo limesemwa kwenye jibu ambacho unaona wewe unataka kuuliza cha ziada unasema namna hiyo.

Maana nimeona hizi kauli zinaongezeka sana kuna muda wamejibu asilimia ngapi na namna hiyo hapana, kanuni zetu zinatupa fursa Waheshimiwa Wabunge kama hatukuridhika na majibu tuseme hivyo Serikali ipewe fursa ya kujibu tena lakini tuseme tu hivyo kwa kuwa tume sema kwasababu pia tutakuwa tunaiweka Serikali mazingira magumu kwamba sasa ni majibu gani ambayo Mbunge anayataka maana yake Mbunge unayo tayari majibu yale ambayo unayatafuta tena kutoka Serikalini, hili nadhani limeshaeleweka.

Waheshimiwa Wabunge pia mnakumbushwa na uongozi wa Ubunge *sports club* kwamba muwe mnaenda mazoezini Jamhuri ili kuweza kwanza kujitayarisha na mech za kirafiki ambazo zinakuja lakini pia kujitayarisha kwa ajili ya mashindano, ambayo siku zote Mheshimiwa Spika huwa

anasisitiza hapa Waheshimiwa Wabunge huwa kuna kusafiri kwenda kuliwakilisha bunge hili katika michezo ya aina mbalimbali.

Kwa hiyo, ni vizuri kufanya mazoezi kujiardaa kwa ajili ya hayo yote. Pamoja na hayo, hapa tumeshatangaziwa wapima afya wapo, sasa kuna mtu kwenye mazoezi haendi, kupima afya haendi, sijui anamtaka nini Spika wangu jamani. Fursa zote umepewa, vyote hufanyi, mazoezi hufanyi na kupima hutaki.

Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge mfanye hivyo, lakini hata wale wanaofanya mazoezi waende wakapime ili uwe unafanya mazoezi ukiwa umeshafahamu afya yako. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hayo yote mawili. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu ulio mbele yetu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Kanuni gani?

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76 ambayo inasema, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwengine anayesema na kuomba Mwongozo kuhusu jambo ambalo ...

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo kwenye Kanuni ya 71(1)(k) ambacho kinasema kwamba, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha, wewe eleza hoja yako mimi ninazo hapa Kanuni.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nazungumzia kipengele (k) cha uchokozi kwamba nimechokozwa humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nimekabidhiwa Ubunge na wazee wangu wa Jimbo la Kibiti, nilikuwa nimepewa ahadi zifuatazo; ahadi ya kwanza niliambiwa kwamba iwapo utafanikiwa katika mwaka huu wa kwanza ukienda Bungeni, basi angalau ikatengwa bajeti tu ya barabara ya Bungu – Nyamisati, wazee wale waliniambia watanipa zawadi ya mke wa pili. Mimi dhehebu langu linaruhusu kuoa wake wanne. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, wazee wale wakaenda mbali zaidi wakaniambia kama utafanikiwa vilevile barabara ya kutoka Kibiti kwenda mpaka kwenye mradi wa Mwalimu Nyerere angalau shughuli za awali zikaanza basi mtoto wetu tutakupa mke wa tatu. Wakaenda mbali zaidi wakasema barabara ya Kata ya Mlanzi – Ruamke – Kikale - Mtunda – Moyoyo, hii ukifanikiwa vilevile mtoto wetu tutakupa mke wa nne. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nahisi kwamba Kanuni hapa imevunjwa kwa sababu nimechokozwa makusudi na Wabunge wenzangu watatu ambaye ni Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake wawili. Nasema hivyo kwa sababu kwangu mimi hii ni hoja ya msingi, wanankosesha hii amani ya kuweza ku-exercise *right* yangu ya kuwa na mke wa pili, wa tatu na wa nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 76 kama alivyokuwa ameanza kuísoma Mheshimiwa Mpembenwe inataka Mbunge asimame kuonesha jambo ambalo limefanywa humu ndani kinyume na Kanuni. Kwa

hiyo, Kiti huwa kinatakiwa sasa kutoa mwongozo kama limefanywa kinyume na Kanuni, au Mbunge hana hakika kama limefanywa kinyume na Kanuni. Kwa hiyo, anasimama akitaka ufanuzi ili mimi niseme jambo hilo linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Mheshimiwa Mpembewi kwa maelezo aliyojatoa hapa, hii Kanuni ya 71 inazungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni na yeze anataka kuashiria kwamba atakosa hao wake wengine watatu kama bajeti hii itakuwa hajazitaja hizo barabara. Kwa sababu jambo lenyewe limekuja kwa namna ambayo linataka kujaribu matumizi ya Kanuni kwenye hoja yake hiyo ambayo aliahidiwa na wazee wake ambao hawapo humu ndani, ahadi hiyo ilitolewa huko Jimboni kwake lakini sasa hapa sitatoa mwongozo wote kwa namna ya jambo lenyewe liliyokuja isipokuwa nimshauri Mheshimiwa Mpembewi kwamba wale wenye wake wanne tunawafahamu humu ndani na hali zao ni mbaya, kwa hiyo, tulizana na huyo huyo mmoja anakutosha. Nadhani umepata picha kwamba wake wanne siyo masihara huyo mmoja tu kaa naye anakutosha Mheshimiwa. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA  
UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea, nimeshaletewa hapa majina ya wachangiaji mbalimbali ambao watapata fursa ya kuchangia siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Kunti Majala atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu, Wizara ya Ujenzi ambayo inahusisha barabara zetu pamoja na viwanja vyetu nya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala zima la ulipaji wa fidia kwa wananchi wetu wanaokwenda kupisha maeneo yanayokwenda kujengwa viwanja nya ndege, lakini pili na barabara zetu. Wizara ya Ujenzi kuitia Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Dodoma, *Airport* hii hapa iliwasimamisha wananchi wa eneo la Makole tangu mwaka 2016 mwezi Mei wakiwa wanahitaji maeneo yale kwa ajili ya kupanua uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwanja ule wananchi wale waliosimamishwa baadhi walilipwa lakini wengine waliobaki zaidi ya wananchi 57 mpaka leo hawajalipwa fidia na wamezuiliwa kuendeleza makazi yao na hakuna tamko lolote linaloendelea, wamebaki wako pale nyumba zinapata ufa, hawawezi kupaka rangi, hawawezi kufanya chochote, wameshabomoa na wameshaweka uzio tayari. Wizara ya Ujenzi kuitia kwa Mheshimiwa Waziri atuambie wananchi wale waliobaki kwenye Uwanja wa Ndege, *Airport* hii iliyoko hapa Makole, ni lini watalipwa fidia zao ili waweze kuondoka eneo lile na kama hawalipwi hawaoni sasa ni wakati wa kwenda kuwaruhusu waendelee na ukarabati wa makazi yao na kuwapa kibali cha kuendelea kuishi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hilo, kwa kuwa wamewachelewesha, waliwafanyia tathmini ya kuwalipa fidia tangu mwaka 2016 mwezi Mei, wamewakalisha muda wote zaidi ya miaka mitano, sita sasa; watakakwenda kuwaruhusu kuishi kama hawawalipi fidia ya kuwaondoa hawaoni sasa kuna sababu pia ya kuwalipa kifuta jasho kwa kupoteza muda wao mrefu na kushindwa kuendeleza makazi yao hayo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna Uwanja wa Ndege wa Msalato hali kadhalika uwanja ule na wenyewe kuna wananchi waliotakiwa kupisha ujenzi wa uwanja ule,

walilipwa zaidi ya wananchi 200 wakabaki wananchi 89; tangu mwaka 2011 mpaka leo wananchi hawa hawajalipwa. Pia nataka kujua wananchi hawa wanalipwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ulipwaji wa fidia, nimeona hapa kwenye kitabu cha Waziri anasema uwanja huo wa ndege uko kwenye mchakato. Mchakato mpaka lini, zaidi ya miaka 10 kiwanja hiki ni mchakato tu. Waziri akija kuhitimisha hoja yake jioni ya leo, naomba kujua ni lini sasa kwa tarehe ili tuweze kujua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dodoma wa Msalato unakwenda kuanza ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala zima la barabara zetu. Nitazungumzia barabara moja muhimu sana kwa maslahi mapana ya wananchi wa mikoa minne. Tunafahamu fika barabara ndiyo uchumi wa Taifa letu. Bila barabara hauwezi kupata huduma ya afya au huduma yoyote ya msingi au kufanya shughuli zozote za kibinadamu. Tuna barabara ya kutoka Kilindi - Kiteto - Chemba (Dodoma) - Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii iliahidiwa na Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa; miaka 10 imeisha barabara hajajengwa. Akaja Rais wa Awamu ya Nne akaahidi barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami; miaka 10 imepita barabara hii hajajengwa. Akaja Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ikawekwa kwenye Ilani ya CCM mwaka 2015 - 2020 imepita bilabial. Imewekwa kwenye Ilani ya mwaka huu 2020-2025, kwenye kitabu cha Waziri inasema barabara hii inakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu; miaka 25 Ilani ya Chama cha Mapinduzi mnafanya upembuzi yakinifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo si sawa. Sisi wananchi wa Wilaya ya Chemba barabara pekee inayoweza kukuza uchumi wa wilaya yetu ni barabara ya kutoka Kilindi kuunganisha na Mkoa wa Singida. Kati ya kata 26 za Jimbo la Chemba; kata 12 ndizo zilizopitiwa na barabara

hii. Tukijenga barabara hii kwa kiwango cha lami tutakwenda kukuza uchumi wa wilaya yetu kwa kuwa ...

## TAARIFA

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti, kuna taarifa inatoka wapi sioni Mbunge akisimama. Waheshimiwa Wabunge ukisema neno taarifa inabidi usimame ili nikuone. Mheshimiwa Eng. Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba tu kumpa taarifa mzungumzaji nafikiri ana *lag behind the information*. Barabara anayoitaja inakwenda kujengwa kilomita 20 na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alitamka hapa Bungeni; *Phase 1* ilikuwa ni kilomita 50 lakini kutokana na *scarcity* ya bajeti kilomita 20 inakwenda kuanza kujengwa. Sisi watu wa Tanga tunaifuatilia kwa karibu kwa sababu ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Tanga. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niendelee kwa sababu ye ye anazungumza biashara ya kilometra 20; kwako Tanga kuna lami mama sisi Chemba hatuna lami. Kwa hiyo, ukiniaambia biashara ya kilometra 20 *none of my business*. Kwanza, hata hiyo kilometra 20 imeanza au iko tu kwenye maandishi? Bunge la Kumi na Moja tuliambiwa inakwenda kujengwa, haikujengwa. Kwa hiyo, tunachokitaka hapa na nachotaka kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kama barabara viongozi wetu wakuu wa nchi wanaahidi awamu zote mbili kipindi cha Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, miaka 20 hamjajenga barabara leo mtu anakuja kuniaambia kwamba wanajenga kilometra 20, *so what?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii sisi Wanachemba na Mkoa wa Dodoma ndiyo itakayokwenda kutusaidia kujenga uchumi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Serikali imekuwa ikitumia humu ndani kwamba Halmashauri ambazo zitakuwa na uchumi mdogo au zitakazoshindwa kukusanya mapato zitakwenda kunyang'anywa; sisi Chemba hatuna chochote tunategemea kilimo, wakulima wetu wanaolima Wilaya ya Chemba, tunatarajia tuwe na miundombinu rafiki kuwezesha kuza mazao ili tuweze kukuza uchumi wa Halmashauri lakini hatuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wafanyakishara wa mazao wanakuja kununua mazao kwa wakulima wetu kwa bei ya chini kwa sababu ya miundombinu mibovu ya barabara. Wawekezaji wanashindwa kuja kuwekeza ndani ya Wilaya ya Chemba kwa sababu miundombinu ya barabara si rafiki atakuja kuwekeza ili afanye nini? Sisi tuna mapori mawili; (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Mkungunero na Pori la Swagaswaga, tunaweza kupata watalii kama tutakuwa na barabara hii ambayo itatusaidia kuendelea kujenga uchumi wa Halmashauri yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atakapokuja biashara hii ya kilometra 20, tutashughulika humu ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu jana walikuwa wanasema kuna upendeleo na ukiangalia ni kweli; kata 26 huna barabara ya lami hata kilometra moja halafu unasema uko sawa, kweli? Hata watoto nyumbani mzazi ukimnunulia huyu leo kaptura, kesho mnunulie mwingine, inakuwaje mtoto huyo huyo kila siku ndiye unayemnunulia kaptura halafu mwingine unamuangalia? Kwa akili ya kawaida kama binadamu atahisi yeye kabaguliwa au katengwa na mwisho wa siku mtoto yule ataanza kuishi maisha ya kujitenga. Hatuhitaji ndani ya Bunge hili na ndani ya Taifa letu tuanze kuonekana kwamba kuna mikoa ambayo yenyele ndiyo mizuri zaidi na inastahili sana na mikoa mingine ambayo haistahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sera ya Wizara ya Ujenzi inakwenda kuunganisha barabara za mikoa kwa mikoa na wilaya kwa wilaya. Tuna barabara ya kutoka Mrijo Olbolotí, inapita mpaka daraja la Simba Kelema tunaunganisha na Wilaya ya Kondoa. Kuna daraja pale lilikatika mkaenda kuwaambia eti *TARURA* ndiyo waende wakajenge daraja lile, *TARURA* ana uwezo wa kujenga daraja la namna gani? *TARURA* mnaowapa bajeti ya 30% *TANROADS* wanachukua 70%, *TARURA* watawenza kujenga daraja lile? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aniambie daraja lile la Kelema Simba Maziwani ni lini litakwenda kujengwa la uhakika ili tuondokane na adha ya Watanzania wetu wa Wilaya ya Chemba kusafiri kwa shida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna eneo lingine korofi sana; kuna eneo la Mto Bubu ambao unapita Kata ya Songolo, wakati wa kipindi cha mvua maji pale huwa yanajaa kweli kweli na abiria wanaposafiri wakikutana na ule mto ni lazima wasimame ili mto upite na wao waweze kuweza kupita. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha naomba atuambie maana wananchi wa Wilaya ya Chemba tunahitaji Daraja la Songolo ili kuokoa maisha ya wananchi wetu na watoto wetu wa shule kwa sababu tuna shule ya msingi na sekondari ambapo mwaka jana watoto wawili; mmoja wa sekondari na mwingine wa shule ya msingi walifariki kwa kusombwa na maji kutokana na lile daraja pale maana wanavuka kwenda shuleni.

Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja pia atuambie nini anachokwenda kufanya kuhusiana na daraja hili, hata kama ni la dharura tutengenezeeni wakati mnaendelea kujipanga ili muweze kutuwekea daraja linalostahili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache haya, nakushukuru kwa muda wako lakini fidia Uwanja wa Ndege wa *Airport* pamoja na Msalato naomba kujua hatma yake. Pia naomba kujua hatma ya kilometra 461 za barabara ya kutoka Kilindi mpaka Singida zikiwa zinapita Chemba. Nakushukuru sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Kisangi atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenga, Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwake kwa kura za kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa jinsi walivyouwezesha Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Usiposhukuru kwa kidogo basi hata ukipata kikubwa huwezi kushukuru, ni lazima niipongeze na kuishukuru Serikali kwa yale yaliyofanyika katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Kwanza kupata Daraja la Kigamboni; Daraja la Mfugale TAZARA; *Interchange* Ubongo ya Kijazi; na ujenzi wa Daraja la Selander ambao umeanza na unaendelea vizuri ila nitaiomba Serikali waharakishe katika kulimaliza daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi wa barabara ya Bagamoyo. Barabara hii imejengwa vizuri lakini ina changamoto kubwa sana. Changamoto yake kubwa ni kwamba mvua inaponyesha inajaa maji katika maeneo yote. Hatuelewi hivi upembuzi yakinifu uliofanyika katika eneo lile hawakuliona hilo? Barabara ni nzuri na tunatarajia kweli itafungua uchumi katika maeneo hayo lakini ina changamoto ya kujaa maji. Niiombe Serikali wakaangalie hiyo barabara ina matatizo gani mpaka inajaa maji tena inajaa kwa kupililiza kama bahari, ni nini kimetokea pale? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeze Serikali kwa ujenzi wa daraja au *interchange* nyingine ya Uhasibu Chang'ombe na pale VETA. Miradi hiyo yote yote inaendelea

na kandarasi wako *site*, naipongeza sana Serikali kwa kutufanya mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa barabara za Ubungo, tuna wilaya mbili; Wilaya ya Ubungo na Wilaya ya Kigamboni ni mpya hazina mitandao mikubwa ya barabara. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie kwamba wilaya hizi ni mpya na tumeweka makao makuu ya wilaya na halmashauri lakini hayafikiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika barabara za Ubungo. Tuna wilaya mbili; Wilaya ya Ubungo na Wilaya ya Kigamboni ni wilaya mpya, hazina mitandao mikubwa ya barabara.

Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie kwamba Wilaya hizi ni mpya na tumeweka Makao Makuu ya Wilaya na Halmashauri, lakini Makao Makuu ya Wilaya na Halmashauri hizo hayafikiki. Kwa mfano, katika Wilaya ya Ubungo barabara ya Makabe kupitia Msakuzi hadi Mpiji, barabara hii ni muhimu sana katika kuwezesha wananchi wa maeneo haya kufika katika Ofisi zao za Wilaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara kubwa ya Kibwamba - Kibwegere mpaka Mpiji; barabara hii ni kubwa na imetupa shida sana katika kampeni zetu. Naiomba Serikali ianze ujenzi wa barabara hii angalau kwa kilometra moja, wananchi wa Kibamba waone kwamba angalau Serikali yao inawajali. Pia niombe barabara ya Kimara mwisho kwenda Segerea kupitia Bonyokwa, barabara hii ni muhimu ambayo inaunganisha wilaya mbili; Jiji la llala na Halmashauri ya Ubungo. Naiomba sana Serikali waiangalie barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika Jimbo la Kigamboni. Jimbo hili ni mtihani, hakuna barabara. Barabara ya lami ambayo ipo kuanzia Mji Mwema kwenda Pembra Mnazi, bado haijafikia kilometra hiyo, inaishia Somangira. Pia barabara hii inakubwa na changamoto kubwa ya kuharibika haribika. Mara tu inaanza kujengwa ni viraka viraka, sasa hii

hali inakuwaje? Naiomba sana Serikali, kama wanajenga, basi wajenge barabara imara kulingana na uchumi wa eneo ille. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile mwanzoni Mji wa Kigamboni ulikuwa haujajengeka, lakini sasa Kigamboni imejengeka ina viwanda, ina magari makubwa. Kwa hiyo, wakijenga wasiweke lami ya mparazo, wahakikishe wanaweka uimara wa sawa sawa kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo tunaiomba toka mimi nimeanza kuwa Mbunge humu ndani mpaka leo hii, barabara ya kutoka Kibada kwenda Kisarawe II, kwenda Pemba Mnazi kupitia Kimbiji; barabara hii jamani tumeiomba mimi toka naanza Ubunge kila nikisimama naomba barabara hii. Naomba Serikali sasa waianzishe. Hii barabara ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Marehemu kwamba sasa Mji wa Kigamboni unaenda kufunguliwa na barabara ikiwepo barabara hiyo. Naomba sana Serikali waiangalie.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umeisha Mheshimiwa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote naipongeza sana Serikali kwa yale waliyoyafanya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu mnachangia dakika tano, kengele itangongwa mara moja. Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunisimamia na kuniongoza mpaka kufikia hapa nilipo. Naomba kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya katika ujenzi

wa miundombinu ya nchi yetu na kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaokuja wa 2021/2022. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia suala nzima la ndege. Serikali imefanya kazi nzuri ambayo siyo ya kubezwa kwa kununua ndege nane nzuri kabisa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Katika mwaka wa fedha unaokuja, tumetenga shilingi bilioni 450 kwa ajili ya kununua ndege nyingine tatu, lakini vile vile, kwa ajili ya kuboresha karakana zetu za viwanja vya ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iweke msisitizo katika karakana zetu ndege ni karakana hii bilioni 450 iliyotengwa kwa hakika naona haitoshi kwenda kununua ndege tatu, kumalizia deni la *Airbus* na vilevile, kufanya karakana zetu za ndege. Naona kama ni kizungumkuti. Nafikiri ni muhimu tukaziboresha karakana zetu kwa uhakika zaidi wa kuhakikisha ndege zetu zitadumu kuliko kuongeza ndege nyingine tatu hali ya kuwa karakana zetu zinahitaji maboresho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Serikali iliangalie jambo hili kwa kina. Ndege ni karakana, tusipofanya hivi shirika letu la ndege litakuja kurudi nyuma kama huko nyuma tulipotoka; na mzimu wa Marehemu utatuandama kama hatutatengeneza karakana za ndege Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia pia na kuhusiana na kiwanda cha ndege cha Tanga. Kule tunafahamu kuna mgogoro na umewekwa katika bajeti. Naomba Serikali ikamalize mgogoro ule ili kuweza kujenga kiwanja cha ndege cha Tanga. Ni tangu Mheshimiwa Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli wakati anazindua mradi wa bomba la mafuta, aliahidi kiwanja cha ndege kule kujengwa lakini mpaka leo tunakwenda kusaini mkataba wa bomba la mafuta, kiwanja cha ndege cha Tanga bado hakijajengwa. Serikali iweke *commitment* kuhusiana na

jambo hili. Ni fedheha kama wataalamu watakaokuja kejenga bomba la mafuta watatokea Kenya wakati Tanga tuna kiwanja cha ndege. Tunahitaji kiwanja cha ndege hicho kiingizwe katika *commitment* ya Serikali na kijengwe haraka iwezekanavyo. Ni miaka minne sasa imepita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusiana na bandari. Niliwahi kusema jamani, tunafanya miradi mikubwa sana ya upanuzi wa bandari zetu, lakini tunahitaji tafiti na wataalam wa kujuu kwa nini kina cha bandari zetu zinapungua? Bila tafiti tutaendelea kutumia mabilioni ya pesa kuongeza kina cha bandari zetu, lakini mwisho wa siku tunapiga *mark time*; leo tutafanya *capital dragging*, baadaye tutafanya *maintenance dragging* lakini hatujui sababu kwa nini kina cha bahari kina pungua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Western California Beach* ya Marekani iliwhali *ku-sediment*, yaani kina kupungua; na sababu kuu ilikuwa ni ujenzi wa mabwawa ya maji ya umeme. Sasa tuangalie mahusiano ya mito yetu na bahari zetu ambapo tunajenga au tunapanua hizi bandari zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemwa kwa mujibu wa *port and coastal engineering*, mto hata ukiwa na kilomita 150 unaweza kuleta madhara katika bandari iliyoko huku. Kwa hiyo, bila tafiti pia hatuwezi kusema kwamba huu utaratibu wa kuongeza kina kwa maana hii ya *dragging* ni wa faida kiasi gani kwa Taifa letu? Kwa sababu siyo njia pekee ya *ku-control sedimentation*, zipo njia nyingine. Je, tunafanyaje cost comparison analysis kama hatuna tafiti za kujuu vyanzo vingine vinavyosababisha *sedimentation* na njia ya *ku-control?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala nzima la Bandari ya Tanga kuhusu ufanisi wake...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani naomba nimalizie...

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagongwa Mheshimiwa. (*Makof*)

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo aah.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, muda wangu umevana sana. Kwa hiyo,...

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja, nashukuru. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nina orodha ndefu sana hapa, kwa hiyo, Waheshimiwa, mtu uchague kile kilicho kipaumbele chako. Ukiweza, zungumzia jambo moja; yule yule mwenye maneno mengi ya haraka, labda ndiyo atawenza mawili.

Mheshimiwa Seif Gulamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Mheshimiwa Mrisho Gambo, ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Nina mambo matatu. Najua muda siyo mrefu sana, dakika ni chache; dakika tano siyo nyngi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niweze kutoa mawazo yangu kwenye wizara hii. Moja, nawaomba watu wa ujenzi; ujenzi wa viwanja vy a ndege wapewe watu wa Mamlaka ya Viwanja vy Ndege wajenje wenyewe. Kazi ambayo wanafanya sasa hivi *TANROAD* ni ujenzi wa viwanja vy a ndege wakati kazi hiyo inaweza kufanywa na watu wa Mamlaka ya Viwanja vy Ndege. Naomba Wizara ilichukuwe hili na ifanye mabadiliko. Kama kuna maboresho, wafanye maboresho lakini bajeti ipelekwe na isimamiwe na watu wa Mamlaka ya Viwanja vy Ndege. Hilo la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nawaomba watu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, katika *wind-up* mtuambie, kwa sababu kuna maombi ya kuundwa kwa Bodi ya Wataalamu ya Usafirishaji. Kuwepo na bodi hii ili iweze kusimamia masuala yoyote ya uchukuzi na usafirishaji ndani ya nchi yetu. Juzi nimemwona Mheshimiwa Waziri Mkuu ameenda kukagua *DART*. Msimamizi wa *DART* anatoka Ujenzi; watu wanaotoka uchukuzi, hawaendi kusimamia masuala yao. Huwezi kupata *performance*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba watu wa Ujenzi na Uchukuzi; *DART* na mambo yote ya uchukuzi, tunacho Chuo cha Usafirishaji, kinatoa wataalam, tuwatumie wataalamu hao. Haiwezekani masuala ya usafirishaji mchukue watu wa ujenzi wakasimamie fani ya usafirishaji, haiwezekani, mbadilishe. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi chukuwa wataalam kutoka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji wakasimamie kazi hizi za *DART* na bandari na maeneo menginge ili kuleta ufanisi katika kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba watu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, naipongeza kamati ya Ujenzi na Uchukuzi wamezungumzia ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa. Wakati wa kampeni yam waka 2015, Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alisimama Ziba akatuahidi barabara ya lami. Mwaka 2020 amesimama tena, ameahidi barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye llani ya Chama chetu cha Mapinduzi, imeandikwa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Ziba - Choma, Ziba - Nkinga - Ndala mpaka Puge; ili ujenzi huu uanze, lazima muweke bajeti. Hamuwezi kujenga bila kuweka bajeti ya *feasibility study*. Naomba tuweke bajeti. Niliiwahi kukutana na Mkurugenzi wa *TANROAD*, Mheshimiwa Eng. Mfugale akatuambia suala hilo la *feasibility study* litafanya na watu wa Mkoa. Leo ni mwaka wa tatu toka atoe maelekezo kwamba watatenga fedha watu wa mkoa waweze kufanya *study* hiyo. *Study* hajifanyika na katika bajeti hii sijaona *study*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema mkoa wanapata fedha za kuweza kufanya *feasibility study*; nakuomba sasa katika *wind-up* utoe maelekezo *study* hiyo ifanyike kwa sababu barabara hiyo ni muhimu na ikizingatiwa barabara hiyo inaunganisha Mkoa wa Tabora na Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo ina hospitali kubwa mbili, kila siku tunaeleza; tuna Hospitali ya Rufaa ya Nkinga ambayo inahudumu ndani ya Mikoa zaidi mitatu; Tabora, Shinyanga, Kigoma pamoja na Katavi na Singida, wanaletwa pale, wanatoka kule kote wanakuja kwa lami, wakifika pale wanatumia vumbi. Kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri lichukuwe hili na katika *wind-up* tunataka tuone ukitoa maelekezo ya barabara hiyo ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa muda wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Mathayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nataka kuanza kwa kushukuru Chama changu cha Mapinduzi, kwa mara ya kwanza kutambua umuhimu wa barabara ya Mabokweni - Maramba, Mtoni Bombo kuelekea Korongwe halikadhalika kuelekea Umba Junction mpaka Same, kwamba kwa mara ya kwanza barabara hii sasa imeingia kwenye llani ya uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuingia kwenye llani ya uchaguzi, kwa masikitiko makubwa, bajeti hii imeisahau barabara hii. Barabara hii nimeizungumzia kwa miaka 10 mfululizo tukipewa ahadi barabaraba itajengwa. Tukipewa

ahadi kipindi fulani kwamba barabara hii sasa itajengwa kwa kupitia *MCC*, mpango ule ukayeyuka. Akaja ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa mwaka 2019 akaahidi kwamba bajeti ijayo tutaiingiza kwenye mpango wa kufanya *feasibility study*, halikutokea na hata leo halikutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imeahidiwa na Mheshimiwa Benjamini Wiliam Mkapa, Marehemu, haikutokea; barabara hii akaiahidi Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, hakutokea; barabara hii amehiahidi Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli, haipo hata kwenye *feasibility study*; barabara hii walizungumzia viongozi wetu wa dini wakubwa wa nchi hii; Shehe Mkuu ameizungumzia barabara hii na alipewa ahadi na Mheshimiwa Rais pale Korongwe mwaka 2020, haijatokea; Askofu Mkuu wa Anglikana wa nchi hii ameizungumzia barabara hii, akaahidiwa itajengwa, haijajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mmepuuza maneno ya Kitandula, basi hata ya hawa viongozi mnayapuuza! Hivi mwambiwe na nani ili mwelewe? Sisi watu wa Mkinga tunasikitika sana na jambo hili; na ninataka niweke rekodi sawa hapa, kuna maneno huwa yanensemwa hapa, kwamba watu wa Kaskazini walipendelewa; jamani, Mkinga hatuna barabara, Tanga hatuna barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Mkinga tuna kilometra zisizozidi 25 za lami na hizi zinakwenda kule Horohoro kwenye *boarder* yetu na Kenya. Hazikwenda kwenye maeneo ya uzalishaji. Hebu tutendeeni haki, njooni mtusaidie kujenga barabara hii ya kutoka Mabokweni – Maramba - Mtoni Bombo - Mashewa kwenda Korongwe, vile vile tuiunganishe na barabara hii ya kwenda Umba Junction mpaka Same. Hivi ni kwa nini kwa upande ule wa Same *feasibility study* imekamilika, lakini huku kuna kigugumizi? Tunaomba maelezo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja hii, atupe maelezo ya kina, vinginevyo hakitaelewka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara iliyanza kujengwa ya kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kichekesho

ni kwamba tunajenga mita 200, mita 150; barabara ya kilomita 28 tunajenga mita 200, hivi tutamaliza lini? Naiomba Serikali ifikirie mambo haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedatus Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Salma Kikwete, ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nijitahidi kuwa *very honest*. Nawashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Ujenzi kwa maana ya Wizara ya Uchukuzi na *TANROADS* kuitia *Engineer Mfugale* na Meneja wetu pale wa Mkoa wa Arusha, Eng. Kalupale, wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana hasa kwenye Jimbo letu la Arusha mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba, Jimbo la Arusha Mjini tulipata bahati ya kuwa na barabara ya mzunguko ile ya Arusha *bypass*, tunaiita ya kilometra 42.4, lakini pia tulipata barabara ya Sakina - Tengeru ya Kilometra 14.1. Barabara hizi ni nzuri sana kwa sababu kuitia barabara hizi kwa mara ya kwanza ndiyo tumeweza kuwa na barabara za njia nne katika Mji wa Kimataifa wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyokuwepo, tunajua *phase* ya kwanza mmejenga barabara lakini mmetoa baadhi ya matoleo ambayo yanachukua maji kutoka Wilaya ya Arumeru yanawapeleka kwa wananchi, kiasi ambacho barabara kila mwaka zinaharibika.

Ombi langu ni kwamba, kwa sababu tunayo mito kwenye maeneo hayo; tuna Mto Nduruma, Mto Ngarenaro, Mto Balaa na Mto Naura, tulikuwa tunaomba sasa *phase* inayofuata, waisaidie *TANROADS* kuyazuia yale maji na kuyaelekeza kwenye mito ili yasiweze kuharibu barabara za kawaida na kuwapa changamoto kubwa zaidi wenao wa *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ambazo zinaathirika sana na changamoto hii, tuna Kata 12; Kata ya Sakina, Kata ya Sekei, Kata ya Balaa, Kata ya Levolesi, Kata Kaloleni, Kata ya Ngarenaro, Kata ya Kimandolu, Mushono, Ololien, Sombetini, Osunyai na *Unga Limited*; karibu nusu ya kata zote za Jiji la Arusha. Ni imani yangu kwamba *TANROADS* kuitia ujenzi wa barabara mpya ile ya kutoka *Arusha Airport* na ile barabara ya Arusha Kisongo ambayo na yenyewe ni ya njia nne, watakwenda kujenga mitaro ambayo itaweza kuya- *tap* yale maji na kuyapeleka kwenye mito ili wananchi wa Kata ya Sombetini Osunyai na *Unga Limited* wasipate hivyo changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwenye uwanja wetu wa ndege wa *Arusha Airport*, pale *TANROADS* na kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, wamefanya kazi kubwa na nzuri sana. Kuna barabara pale za kisasa zimejengwa na mazingira yamekuwa ni mazuri sana. Changamoto kubwa tuliyokuwa nayo sasa hivi ni changamoto ambayo inahusiana na majengo yaliyoko pale; majengo kama ya abiria wale wanaoingia na wanaotoka, *restaurant* za kisasa, maeneo ya kununua zawadi mbalimbali ili yafanane na mandhari ya Mji wa Arusha na masuala yaweze kuwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni Imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri na timu yake watakwenda kwenye *phase II* kutuwekea utaratibu mzuri zaidi ili maeneo yale yaweze kuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la tatu, pale tunao madereva *taxi*, madereva *taxi* wale kwao hii ni fursa, wamekuwa pale kwa muda mrefu, wengine wako toka mwaka 1998, lakini ukiangalia lakini ukiangalia sasa hivi wenzetu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamekuja na utaratibu wa kusema wanataka kuongeza mapato eti wanataka watangaze tenda ili wawapate watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani badala ya kutangaza tenda wangekaa na wale amba walikuwa pale

kwa muda mrefu kwa sababu ile kwao ni fursa na ni ajira pia ili mwisho wa siku waweze kuangalia utaratibu mzuri zaidi wa kuweka mazingira mazuri zaidi ili walewale waliokuwepo waweze kuendelea. Vinginevyo watakuja watu wengine ambaao wana uwezo zaidi, watatenda kwa juu zaidi halafu wale watu ambaao wako kwa muda mrefu na ni watu ambaao ni wanyonge watakosa hiyo fursa. Ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake watakwendwa kulipa jambo hili kipaumbele ili Watanzania wanaopata riziki zao pale waweze kuwepo na waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la nne ni kwamba tuna barabara yetu ya Tipekazi - Losinyai ambayo yenye imewekwa kwenye mzunguko ule wa kawaida wa barabara ya Arusha – Kibaya - Kongwa ambayo ni ya kilometra 430. Ile barabara ni kubwa sana inawezekana ujenzi wake ukawa ni wa muda mrefu.

Mheshimiwa NaibU Spika, tuna ombi maalum, tunaomba pale kwenye Kata ya Mwishono kuna kipande kidogo sana kilometra ambazo hazizidi saba kutoka kona ya Kiseriani mpaka kwenda kwenye eneo la *By pass* ambapo barabara hiyo ikijengwa itatusaidia kuondoa msongamano katika Jiji la Arusha lakini pia na watalii wakiingia mijini watakuwa na *route* nyangi zaidi za kutuletea dola katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu pia tunayo changamoto ya corona katika nchi yetu. Ni imani yangu wale wafanyakazi sasa wa Mamlaka za Viwanja vya Ndege mara baada ya ripoti ya jana, ya timu ambayo imeundwa na Mheshimiwa Rais wataanza kuvaas sasa zile barakoa na vifaa vingine vyote ambavyo vitairejesha dunia kwamba Tanzania tuko makini na jambo hilo, ili watalii waje wengi zaidi tuendelee kupata dola na miradi hii ambayo tunaililia leo hapa iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Abubakari Asenga ajandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kusema ukweli bajeti tumeiona, kwangu mimi leo ninachoweza kusema ni masikitiko yangu. Ni masikitiko yangu kwa maana kwamba, yako mambo ambayo yanazungumzwa ambayo tunataraji kwamba ndani ya muda mfupi yanapaswa yapate utekelezaji. Kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya mambo ambayo naamini kwamba watendaji wetu aidha wanayapuuza au basi tu wanayawekwa kwa muda ambao hata haukustahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Musoma Mjini tuna tatizo la uwanja wa ndege na tatizo hili ni la muda mrefu kwa sababu ule uwanja wetu ni wa vumbi na sasa hivi hakuna ndege ya abiria ambayo inatua pale. Sasa kinachonisikisha ni kwamba katika awamu iliyopita kwa maana ya marehemu John Pombe Magufuli aliahidi kwamba tutajenga uwanja wa ndege. Kwa hiyo nikashukuru kwamba ndani ya muda mfupi, mpaka fedha za fidia zikaja shillingi bilioni 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha ni kwamba, fedha hizo zimekuja toka mwaka jana, lakini mpaka leo yaani zililipwa tu fedha kidogo kama bilioni mbili hivi na kitu, watu wengine walitathminiwa gharama za fidia, lakini mpaka leo ni zaidi ya mwaka hawajapata fidia, fedha zile 4.2 bilioni ziko kwenye akaunti pale Musoma. Sasa unajiuliza kwanza Sheria yenye ya Fidia inasema baada ya miezi sita inatakiwa ifanyike *evaluation* mpya. Sasa wale watu wameendelea kukaa pale hawajalipwa, wamelipwa watu kiasi na fedha zipo, sasa tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonipa mashaka kabisa ni kwamba, leo Waziri huyu ndiye aliyekuwa Katibu Mkuu wakati huo. Kwa maneno mengine nasema ye ye ndiye ametoa zile fedha, leo tena amekuja, bahati nzuri amekuwa

Waziri, kwa nini hawa watu wasilipwe ili wakaendelee na maisha yao kuliko kuwaacha wakaendelea kupata adha ambayo watu hawa wanaendelea kuipata hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake ni kwamba, siku watakuwa tayari kulipa fidia, maana yake kwamba miezi sita imeisha na kwa kuwa miezi sita imeisha *evaluation* mpya inapaswa ikafanyike na zile nyumba kwa sababu watu walishahama wanashubiri walipwe fidia zitakuwa zimeanguka, kwa hiyo labda huyo mtu badala ya kulipwa milioni 100 au milioni 200, sasa atalazimika kulipa milioni 50 au chini ya hapo.

Kwa hiyo na hilo ningependa Mheshimiwa Waziri aweze kulitolea ufanuzi, ni lini hao watu watalipwa fedha yao mara moja ili maisha yao yaendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo vilevile linanifanya nishindwe kufahamu, kama tulisikia ripoti ya CAG japo kuwa labda muda wake bado wa kuzungumza, katika jambo alilolisema ni kwamba Shirika la Ndege ni shirika ambalo limefanya vibaya katika kipindi sasa cha miaka mitano.

Sasa nimejuliza, nimejaribu kusikiliza katika hotuba ya Waziri yote na kuipitia, hakuna mahali ambapo pameonesha kwamba ni hatua gani ambazo Wizara imechukua kwa ajili ya kulinusuru shirika lile la ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa haraka haraka nilichokifahamu ni kwamba, aidha basi yawezekana habari hiyo labda haikuwa sahihi na kama ilikuwa sahihi, mbona basi suala hilo Wizara haijazungumza chochote katika kulinusuru hilo Shirika la Ndege. Naenda mbali zaidi naanza kujenga mashaka yawezekana kuna habari zingine za upotoshwaji ambazo labda wakitueleza vizuri tunaweza kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naunga mkono hoja lakini nasubiri majibu sahihi kuhusu fidia ya watu wa Musoma. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Inocent sebba Bilakwate ajiandae

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu. Hatimaye nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri ambao umegusa sehemu nydingi katika eneo lake la Wizara yake, vile vile nawapongeza wataalam kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite katika mambo machache sana, kwanza kuhusiana na suala zima la barabara. Kama mnavyofahamu na mnavyojua barabara ya kuelekea kusini inaanzia Kilwa inaishia Mtwara lakini katikati hapa kuna sehemu inaltwa Mingoyo. Hii barabara ni barabara ya Taifa na hii barabara iko chini ya *TANROAD*, lakini barabara hii sidhani kama kuna barabara inayofanana nayo katika nchi hii kwa upungufu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mvua barabara hii imeharibika sana tena sana. Ninachoomba na ninachoshauri pamoja na kwamba Mheshimiwa Dkt. Pombe Joseph Magufuli, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema, alipokuja kwenye mbio za kuzima mwenge kitaifa ilifanyika kule, alisimama pale njiani na akatoa *order* na ile *order* ilitekelezwa kwa kile kipande. Tunashukuru imemalizika, lakini sehemu kubwa barabara hii sio nzuri na wala sio salama na inapitiwa na magari mengi na mazito.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, katika bajeti haipo, sikuiiona sehemu yoyote barabara hii. Lindi - Dar es Salaam ni sawa na sehemu nydingine yoyote katika Taifa hili la Tanzania. Naomba waiwekee bajeti ili barabara hii nayo itengenezwe, maeneo mengi ya barabara hii ni mabovu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninalotaka niliombe kwa ujumla wake naongelea Jimbo la Mchinga ambalo ndio

jimbo langu. Katika jimbo hili kuna sehemu inaitwa Mchinga A na Mchinga B au Mchinga I na Mchinga II. Pale kuna wanafunzi wanaotoka Mchinga I kuelekea Mchinga II, wanafunzi wale wanapata adha kubwa ya kuvuka kwa miguu na yale maji ni mengi, pale kuna mkondo wa bahari maji yale ni mengi sana. Watoto wengi na watu wazima wamepoteza maisha yao kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye ujenzi wa madaraja pamoja na ujenzi wa maboti na kuwapatia watu maboti, kwenye eneo hilo naamini tutapata usafiri kwa ajili ya kuwanusuru wanafunzi wale ili wasiweze kufa wakati wanavuka pale kwenda Mchinga II kutafuta elimu yao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini elimu ni haki ya msingi kwa kila mtu, nilisema Jimbo la Mchinga ni Jimbo pekee ambalo halina barabara ya lami hata kidogo, wengine wanasema tuna nusu kilomita, wengine kilometra moja, wengine sijui kilometra 10, lakini Mchinga hakuna, labda lami utaiona pale sehemu inayoitwa Rutamba kuelekea Rondo na ile nafikiri ni *private* haikuwekwa na Serikali

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hili Jimbo la Mchinga nalo wale watu wanataka waione hiyo lami sasa lini watatuwekeea hiyo lami. Naomba tufanye hima hata kidogo tupate, Jimbo la Mchinga ni Jimbo gumu, Jimbo la Mchinga linataka lifunguliwe, Jimbo la Mchinga linazalisha mazao mengi ya chakula na biashara, korosho zinatoka Mchinga, ufuta unatoka Mchinga, tuna kila sababu ya kuiangalia Mchinga kwa jicho la aina yake.

Mheshimiwa Naibuu Spika, nilisema nitasema machache tu, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kusema, naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, basi mtupatlie angalau majibu ya matumaini kwa Jimbo letu la Mchinga na Wanamchinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana na nawatachia Wizara kila la heri. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Asenga atafuatiwa na Innocent Sebba Bilakwate na Mheshimiwa Timotheo Mzava ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ili nichangie katika Wizara ya Ujenzi. Kwa ukweli kabisa kwa dhati ya moyo wangu japokuwa nina mgogoro kidogo na barabara yangu kubwa kule iliyopelekea mpaka nikaa kwenye matope, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri Injinia Chamuriho, mwezi Januari mapema kabisa alitenga muda wake, akaenda jimboni kwangu kwa dhati ya moyo, namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Kaka Emmanuel Tutuba kwa kweli kuna vitu ambavyo vilikwama kuhusu barabara yetu ya Ifakara - Kidatu na juzi nilikuwa kule *síté* amezungumza na yule mkandarasi, kwa hiyo naona dalili njema. Kwa kweli kwa dhati nimpongeze sana Katibu Mkuu huyu, nina imani atatusaidia kutatua changamoto za barabara yetu ya msingi sana kutoka Ifakara kwenda Kidatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua mgogoro huu Waziri wangu wa Ujenzi anafahamu fika kwamba barabara hii ni miongoni mwa barabara ambazo zimesainiwa na Wizara ya Fedha. Najua watu wangu wa ujenzi inawezekana kwenye miyo yao hawajaridhika sana kwamba barabara hii imekuwajekuwaje Wizara ya Fedha wakasaini mikataba na wakati utaalalm uko kwenye Wizara ya Ujenzi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na wataalam wake na watu wa *TANROAD* wa Mkoa wanafanya kazi nzuri, wanafanya vizuri, watusaidie kuendelea kuifuatilia barabara ya Ifakara - Kidatu kwa sababu ndio barabara ya ajenda yetu kubwa ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikaa chini kwenye matope kwa sababu nilikaa na wananchi kuanzia saa tano usiku barabara ilikuwa haipitiki mpaka saa tano asubuhi. Ukiiniuruhusu hata hapa Bungeni nitakaa endapo Waziri kwenye majumuisho yake ataniambia kwamba barabara hii

itakamilika kwa kiwango cha lami kama Naibu Waziri alivyowahi kujibu Bungeni hapa kwamba Oktoba safari hii itakamilika, ijapokuwa ni muda mfupi sana. Kwa hiyo ukiniruhusu nitakaa hata hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza nikae?

**NAIBU SPIKA:** Hapana hapana Mheshimiwa.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni msisitizo kwamba barabara hii tangu 2017 mpaka sasa hivi ni mvutano...

**NAIBU SPIKA:** Tutaweka utaratibu mzuri, usiwe na wasiwasi wale wanaotaka kumwonyesha Mheshimiwa Waziri kwa vitendo; kuna mzee wa sarakasi, kuna wewe unataka kukaa, kuna Mheshimiwa anataka kugalagala, tutafanya hilo jambo nje pale, tutaweka utaratibu. (*Makof/Kicheko*)

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika zangu zilindwe, kwa sababu dakika tano ni chache, ili nishike shilingi na naomba uniweke kwenye orodha ya watu watakaoshika shilingi. Mgogoro huu tumeujadili wilayani, tumeujadili mkoani kwenye kikao mpaka cha RCC na Wabunge wa Mkoa wa Morogoro na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, ikaonekana kwamba mjenzi *contractor* na *consultant* wana mvutano mkubwa kuhusu barabara hii na unachangia kuchelewesha barabara hii. Sababu gani? Kuna nje ya nchi huko, walipata tenda pamoja wakagombana na wamekuja *site* wanagombana.

Sasa tukashauriana, mmoja yule hasa *consultant* anatakiwa aondoke apishe ili kutafuta mtu mwингine wa kusimamia barabara ile ili iweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia, inaonekana *consultant* kuna mkubwa huyo anamtetea na sitaki kumtaja jina lake hapa, lakini Mheshimiwa Waziri tumezungumza naye jambo hili na ameniahidi kwamba bado muda mfupi huyo *consultant* amalize mkataba ili twende vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano, kwa mfano barua ambayo mkandarasi ameandika kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ambaye ameifanyika kazi kwa kiwango cha asilimia 90. Anasema kuchelewa kwa *GNna Exemption* ndani ya miezi 40 wamepata *GN* mara tisa, barabara hii haiwezi kukamilika na barabara hii ina mgogoro mkubwa sana na imeahidiwa na viongozi wa chama akiwepo Spika alipokuja jimboni kwetu kuomba kura. Sasa hili tusishikiane shilingi nataka majibu ya huyu *consultant* anaondoka lini? (*Makof*)

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, amefanya kazi miezi mitano. Nilindie dakika zangu.

**NAIBU SPIKA:** Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika nampa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na mambo mengine, kilichofanya mradi huu uchelewe kwa muda mrefu ni kitendo cha Wizara ya Fedha kusaini mkataba na ikashindwa kujiombea *exemption* kitu ambacho kwa mujibu wa sheria hakiwezekani. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, unaipokea taarifa hiyo

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa murua, taarifa bora kabisa. Kama nilivyosema nimewaomba watu wa Wizara ya Ujenzi waridhike kwenye miyo yao japokuwa barabara hii ilisainiwa na Wizara nyiningine na nina imani chini ya Katibu Mkuu mambo mengi yataenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine, ndani ya miezi mitano *consultant* amemwongezea *contractor* makalavati karibu kumi na tano, anazidi kutengeneza ucheleweshaji. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa

Injinia Chamuriho, anisaidie, alibebi hili, awashauri watu wa Wizara ya Fedha, awashauri kwa sababu Waziri ni mtaalam, ameingia kwenye mikataba na ujenzi wa reli ya kisasa, viwanja vya ndege, kununua ndege, hii kilometra 66.9 itamshindaje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwenye barabara hii, namwomba Mheshimiwa Waziri, angalau kule kijijiini kwetu kila tarafa ina vituo vile vikubwa ambavyo vinafanywa kama masoko, watakavyoendelea na dizaini na marekebisho, watusaidie kuweka vile vituo na taa angalau za barabarani ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu wanakuja barabarani kuja kuuza ndizi, kuuza karanga kwa hiyo barabara hiyo ikidizainiwa ikawa na maeneo makubwa ya vituo itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii katikati ina kituo kinaitwa Mang'ula Kona. Hii Mang'ula Kona ni kona hatari sana pale ajali zinatokea mara kwa mara. Kwa sababu gani kuna kona? Ni kwa sababu kuna mita 50 kwa 100 za eneo la *TANAPA* zimeingia barabarani. Nimemwomba Waziri wa Maliasili na Utalii ameniambia anaweza kutusaidia, tunaomba atusaidie Injinia achonge apanyoshe pale ili kuondoka ile kona ambayo imeitwa kona, kona na inasababisha ajali za mara kwa mara. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kugusia kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Ifakara. Kuna Kiwanja cha Ndege, ndege zinatua kwenye kiwanja kile cha vumbi, Mji wa Ifakara una mzunguko mkubwa wa pesa, wafanyabiashara wale wanaambiwa zikija ndege mara kwa mara, kwa mfano laki moja, laki mbili, waende Dar es Salaam watapanda, wataenda na mji wetu utaendelea kuboreka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mzava Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, bajeti yake ni nzuri na naamini hii ndio bajeti ya kwanza kuwasilisha. Ninachoomba kwa Mheshimiwa Waziri, Wabunge wamekuwa wakisema kumekuwepo na upendeleo na ukweli nakiri, ukiangalia huu upendeleo umekuwepo kwa sababu kuna maeneo mengine unaona ndio yanayotajwa kila mara. Sasa tumwombe Waziri kwa sababu ni bajeti yake ya kwanza ajitahidi sana huu upendeleo usiwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la barabara, barabara ni uchumi na ndio kila kitu. Niombe nzungumzie barabara ambazo ni za kiuchumi; nlongelee barabara ya Murushaka kwenda mpaka Murongo, hii ni barabara muhimu sana kiuchumi. Kwenye Nchi ya Tanzania hakuna wilaya ambayo inalima kahawa nyingi kama Wilaya ya Kyerwa, lakini ukija kuangalia hizi barabara ndizo barabara ambazo zimeachwa kwa muda mrefu na imekuwa ni ahadi ya muda mrefu lakini hazitengenezwi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine nimekuwa nikishangaa, wanasema Mikoa wa Kagera ni mionganoni mwa mikoa maskini. Lakini jambo ambalo linasikitisha ni kwamba hii mikoa ambayo imenyimwa miundombinu lazima itaendelea kuwa mikoa maskini lakini kwa upande mwingine ninajiuliza, Serikali hili hailoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mikoa ambayo ina uzalishaji mkubwa wa kahawa, hii mikoa ambayo ndiyo ina uzalishaji mkubwa wa ndizi, hata ukienda Ulaya watakwambia ndizi ya Bukoba. Lakini nenda uangalie barabara zake zilivyo! (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo niombe, nimeona umeweke pesa kidogo, nimesema hiki ni kama kishika uchumba, hii pesa bilioni tatu ambazo

umeweke, Biblia inasema kila mtu aseme kweli na Jirani yake, na ndio yenu iwe ndiyo na hapana iwe hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swalı langu kwako Mheshimiwa Waziri; hii bilioni tatu uliyoitenga barabara hii unanihakikishia utanza kujengwa! Na ni ahadi ambayo Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliahidi na akatoa maelekezo kwamba ijengwe kilometra 50 kwa kuanzia. Sasa nimeona mmeweke bilioni tatu, kwa kweli niseme hili jambo sijaridhika nalo lakini wewe nikuombe wakati unajumuisha hapa utuambie hii barabara unaijenga lini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mgakorongo kwenda mpaka Mrongo. Hii ni barabara ambayo ni muhimu, inaunganisha Nchi jirani ya Uganda. Ukiangalia upande wa wenzetu ni jambo ambalo linasikitisha, kule kwa wenzetu ni kama Ulaya lakini huku kwetu ni kama uchochoroni. Sasa hizi barabara ambazo zinaunganisha nchi na nchi lazima tuzipe kipaumbele. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nikuombe sana barabara hizi ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, ni jambo ambalo linasikitisha unapita kwenye barabara unaona bado ni nzuri lakini wanakwambia tunaondoa hii lami kwa sababu muda wake wa kuishi umekwisha. Kule kwetu tunatamani hata hiyo mliyoondoa mngetupa sisi, lakini hatuipati. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri hili uliangalie sana na huu upendeleo uondoche kabisa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshalia Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKATWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilisemee...

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mwanakamatii wa Miundombinu...

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimshukuru sana Mwenyezi Mungu anayetupa uzima na aliyetuweka kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa kabisa, tangu nimekuwa Mbunge inawezekana leo ikawa mara ya kwanza kuchangia bajeti nikiwa na masikitiko, na ninaomba Mungu anisaidie isirudie tena iishie kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni muhimu sana kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu. Kule Korogwe tunayo barabara ya kutoka Korogwe – Dindira – Bumbuli – Soni, ni barabara ya kilometra 74. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2010 kwenye ukurasa wa 48 ilitoa ahadi kwa watu wa Korogwe kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii, ikaenda miaka kumi hatukufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwaka 2015 tukahuisha ahadi hii kwenye ilani ya Uchaguzi ya CCM, na tukasema baada ya upembuzi kukamilika tutakwenda kuanza ujenzi, kwenye ukurasa wa 49 na ukurasa wa 56 wa ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015. Tukafanya usanifu kwenye kilometra 21 za kutoka Soni mpaka Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2015 kuja 2020 tukaahidi kwenye ilani, lakini pia na fedha zikawa zinatengwa. Na kwenye ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020, juzi tumetoka kwenye Uchaguzi, ukurasa wa 66 tumewapa taarifa

Watanzania kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu wa barabara ile. Na kwenye ukurasa wa 77 tukatoa ahadi ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kwenye bajeti za Serikali kwenye Wizara hii. Bajeti ya mwaka 2018/2019 hii ninayo hapa, tulitenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Bajeti ya 2019/2020, hii hapa, tulitenga fedha; bajeti ya mwaka 2020/2021 kwenye ukurasa wa 98 Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba kwenye bajeti ile tunatenga shilingi milioni 840 kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwenye bajeti ya mwaka 2021/22 Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, ukurasa wa 12, anasema:-

*"Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2021, mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74), ulikuwa umesainiwa. Aidha, fedha za mradi huu mara baada ya Mhandisi Mshauri anayefanya kazi hii kuwasilisha hati za malipo."*

Mheshimiwa Naibu Spika, imeishia hapo. Hiki ni nini? Naomba Waziri akija atuambie, tumesema upembuzi yakinifu umekamilika na kwenye bajeti iliyopita ambayo tunaimalizia mwaka huu tumetenga fedha ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Leo unakuja kuniambia kwamba tunakwenda kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu; kipi ni kipi? Watu wa Korogwe waelewe kipi? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Korogwe wameumia kwa muda mrefu, wamekuwa na ahadi hii kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri nakuomba, kwanza mtuambie ssa *status* ya barabara hii ni ipi? Lakini mpango sasa wa kutekeleza llani hii ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2020 kama tulivyoahidi ukurasa wa 77 ni upi? Ili watu wa Korogwe wajue. Ni barabara muhimu, ni barabara ya kiuchumi. Mazao

yetu yanaharibika kwa sababu ya barabara hii. Ninakuomba Waziri akija kwenye majumuisho atuambie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kaka yangu, Mheshimiwa Kitandula, kuhusu barabara ya Mabokweni – Bombomtoni – Kwashemshi – Korogwe, ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ni maombi ya kwetu Wanakorogwe, ni maombi ya viongozi wetu wa dini, ni maombi ya wadau wengi wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ni barabara muhimu sana kwa uchumi. Na hii ni barabara mbadala kama mtu anatoka nchi jirani siyo lazima aende Tanga Mjini, anaweza kupita barabara hii akaenda Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na mikoa mingine. Lakini kwenye bajeti hii jambo hilo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri sasa ni lini mpango wa barabara hii, ni lini barabara hii itatengenezwa ili kuweza kuleta maendeleo kwa watu wa Jimbo la Korogwe na Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Waziri, tunao utaratibu wa kupandisha hadhi barabara zetu kutoka kuwa barabara za wilaya kule kwenda kuwa barabara za mikoa na Kitaifa. Na tunafanya hivi kwa sababu tunaamini *TANROADS* ina uwezo mkubwa wa kifedha na wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka karibu mitano hatujafanya jambo hili. Sisi Tanga tumepitisha barabara na kwenye Wilaya ya Korogwe tunazo barabara nne muhimu; iko barabara ya kutoka Mombo – Mzeri, barabara ya kutoka Msambiazi – Rutindi, Kwetonge – Bombomtoni na Makuyuni – Zege – Mpakanani. Tumeshamaliza taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, wewe ndio Mwenyekiti wa kamati ile. Tunaomba mtupandishie hadhi barabara hizi zifanyiwe ukarabati vizuri, wananchi wetu wapate maendeleo. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami nizungumze machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nkasi Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na usafiri wa majini wa Ziwa Tanganyika. Ni vizuri kama Wizara, pamoja na changamoto za kibajeti na vitu vingine lazima tuwe na vipaumbele. Na Serikali yoyote makini lazima iwe na vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba kuna ilani, kuna mpango wa miaka mitano, lakini lengo la mpango, lengo la ilani na mambo mengine, pamoja na kutenga bajeti ndani ya Bunge ni kupeleka huduma kwa wananchi wetu. Sasa kama hilo ndilo lengo, kipaumbele chetu ni nini kwa Wizara?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ambao tunategemea Ziwa Tanganyika tukianza Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Kigoma pamoja na Songwe kule tuna wakulima, wakulima hawa Serikali imewekeza fedha za kutosha kwenye bandari. Sasa hizo bandari wakifikisha bandarini wanapelekaje tukizungumzia maeneo ya nchi za Jirani kwa mfano Kongo na Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea Serikali ilivyowekeza kwenye Bandari ya Kabwe, kuna kitu nilikuwa nataka kukipata kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, tunategemea kama tumewekeza kiasi cha kutosha kwenye bandari tukiwekeza zaidi upande wa *MV Liemba* wananchi wana uhakika wa kusafirisha mazao yao kupeleka nchi za Jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia pamoja na kwamba Nyanda za Juu Kusini tunaongoza kwa Kilimo,

tunatumia njia gani ya uhakika kuweza kusafirisha mazao yetu? Bado kuna shida. Kwa hiyo, tunapenda katika mgao wa hii miradi kuwe na vigezo vinhavyoolewaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Nyanda za Juu Kusini tunajua kuna kilimo lazima tutengeneze mazingira rafiki ya usafirishaji wa mazao yetu. Na njia rafiki ni pamoja na kurekebisha upande wa *TAZARA*. Kama hatujarekebisha *TAZARA* bado tunataka wananchi waendelee kulima kilimo cha mazoea ambacho hakiwezi kuwasaidia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha *TAZARA*, tuzungumzie pia hiyo *MV Liemba* toka imeanza kuzungumzwa. Bunge liliopita tulielezwu hapa kwamba wanasubiri huyu mnanihii asaini, lakini mpaka leo hapa nimeangalia kwenye kitabu cha Waziri anazungumzia kwamba mzabuni alikosa vigezo. Yaani toka Bunge liliopita mnazungumzia vigezo kama mnazungumzia habari ya kusaini, leo mnasema vigezo. Haya mambo hayafurahishi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba kuna maeneo mengine yana vivuko, wana vitu gani lakini sisi kama hatuna *speed boat*, hatuna meli, lakini tunapozungumzia *TAZARA* bado tunahitaji ukarabati wa kutosha. Kwa maana hiyo kama kwenye ziwa imeshindikana usafiri wa uhakika, bado kwenye reli tunazungumzia ni changamoto. Tunataka kuwasaidia nini wananchi wa Mkoa wa Rukwa pamoja na Nyanda za Juu Kusini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, utakapokuja tunaomba kujua hatma ya Meli ya *MV Liemba* imefikia wapi na hivyo vigezo vitakamilika lini, na kwa nini muda wote huu mmechukua halafu mmegundua kwamba huyu mzabuni hana vigezo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia barabara ya Namanyere – Katongolo – Kipili. Huku kote ambako wameelekeza hizi fedha kuna bandari lakini cha ajabu hii barabara ina kilometra 64.8. Wamezungumzia kwenda

bandarini lakini wameacha kilometra nane ambako kunatoa mpunga kupeleka bandarini. Sasa unashangaa tunataka kufanya nini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nashauri wakati mnazungumzia kilometra 64 kama ndiyo lengo la kuwasaidia wananchi wale wavuvi pamoja na wakulima, ongezeni kilometra nane ambazo mtafika Kilando ambako ndiko wanakovuna na ndiko wanakotoa mpunga ili wapeleke bandarini, tutakuwa tunajua kwamba tumemaanisha kuwasaidia wananchi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilometra 64 za kutoka Lyazumbi – Kabwe; hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, na ni vizuri mkawa mna rekodi nzuri za ahadi za viongozi wa Kitaifa. Haiwezekani viongozi wanaahidi lakini mambo hayo hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya kawaida hizi kilometra 64 za Lyazumbi – Kabwe hauwezi kuwekeza bandari pale ukaweka fedha zako za kutosha halafu hakuna lami ya kutoka pale kwenda bandarini. Sasa huyo mtu atakayepita kwenye hiyo bandari anataka kufanya nini? Kwa hiyo, ni vizuri kama Serikali imetangulia kuweka kitu tujue kabisa tunataka wananchi wafanikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia tena barabara ya Chala – Mpalamawe, kilometra 40, ambayo inaunganisha Mkoo wa Rukwa na Mkoo wa Katavi. Kwa kuwa ilikuwa ni ahadi na mkaingiza na kwenye ilani, sina shida na maandishi, shida yetu sisi watu wa Nkasi tunataka utekelezaji wa ahadi hizo ambazo tumewaahidi wananchi wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Sumbawanga Mjini kuja Namanyere ambayo imekwenda Katavi imetengenezwa vizuri, tena ikazinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano. Tunashukuru kwa mambo hayo ambayo Serikali imefanya. Lakini unawezaje

kutengeneza barabara hii halafu hakuna taa? Hivi inawezekana kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nizungumzie changamoto za barabara zilizopo katika Jimbo langu la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mchache, itifaki ya shukrani na pongezi naomba izingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda moja kwa moja kwenye mchango wangu, nizungumzie barabara mbili, tatu, ambazo ni muhimu kwelikweli kwa maisha na uchumi wa wananchi wa Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na barabara hii ya kutoka Singida – Haydom kupitia Mji mdogo wa Ilongero ambao ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya na inapita katika Mji mdogo wa Mtinko na Kata ya Modeda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni ahadi toka Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi. Nakumbuka wakati huo niko darasa la tatu, mzee Mwinyi alikuja pale Ilongero akaombwa barabara hii akaahidi akasema nitaijenga. Amemaliza amekuja aliyefuata mzee Mkapa naye alifika Ilongero pale akaahidi hii barabara, lakini hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati tunaomba kura, Rais, Hayati Dkt. Magufuli, alifika Singida Mjini na akaahidi hii barabara. Kama haitoshi, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, alifika Ilongero na akaahidi kwamba hii barabara

tunajenga kwa kiwango cha lami. Na kwa matokeo hayo kura zilipigwa nyingi kwelikweli kwa CCM.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo, kuna taarifa; Mheshimiwa Kuchauka.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampa taarifa mzungumzaji kwamba pamoja na Waziri Mkuu kutoa hiyo ahadi, lakini Waziri Mkuu kwenye Jimbo lake kuna barabara tatu zote hazifikiki, kwa maana ya kwamba Liwale – Ruangwa, Nachingwea – Ruangwa na Nanganga – Ruangwa; zote hazifikiki kwa lami.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda mfupi ambao kila Mbunge anao wa kuchangia tujitahidi taarifa tunazozitoa basi ziwe za kumuongeza kile anachochangia; Mheshimiwa Ighondo, malizia mchango wako.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na masikitiko hayo ambayo nimeyaeleza naomba basi hii barabara sasa itengenezwe kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa uchache kwamba angalau imeonekana kwenye hotuba ya Waziri, ukurasa wa 42, kwamba inakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu. Basi niombe sana kwa heshima na taadhima, nitaongea kwa lugha ya upole sana leo, sitafanya sarakasi kama alivyosema Mheshimiwa Flatei, lakini ninaomba hii barabara itengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hizi fedha kwanza ni kidogo, niliona ni shilingi milioni 100, milioni 100 kwa kilometra 93 kusema kweli siyo haki, siyo sawa hata kidogo. Barabara

ambayo imeahidiwa na viongozi wote wa Kitaifa tangu uhuru mpaka leo tunaipa kamilioni 100, hili kwa kweli naomba litazamwe na ninamuomba Waziri nitaishika shilingi yako hapa; ongeza fedha hapa, fedha ziongezeke kwenye eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza barabara hii inakwenda Makao Makuu ya wilaya, lakini pili, ndiyo roho ya uchumi wa Wanasingida Kaskazini; vitunguu, mafuta ya alizeti mnayoona, asali na maziwa yote, hii barabara ndiyo roho ya uchumi wao. Niombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa nipe majibu sahihi, vinginevyo hatutaelewana hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nyingine ya llongero – Ikhanoada – Ngamu; hii barabara iliua. Kuna daraja pale la mchepuko, maji yalizidi baada ya mvua kunyesha yakafunika daraja likajengwa daraja la dharura, daraja lile iliua mtu, sasa naomba daraja hili na lenyewe lijengwe. Tuhakikishe linainuliwa ili kupusha vifo vinavyotokea kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ile ambayo nilisema kwenye swalii la nyongeza ya Singida – Kinyeto – Sagara ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais aliye madarakani. Naomba hii barabara nayo ijengwe kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja lakini Kiwanja cha Ndege cha Singida hakionekani kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba na chenyewe akisimama akisemee. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mheshimiwa Priscus Tarimo ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Naibu Mawaziri wake wawili. Lakini pia nimpongeze sana Mtendaji Mkuu wa *TANROADS*, Eng. Mfugale, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa nchi hii katika ujenzi wa barabara katika sehemu mbalimbali za nchi yetu; nampongeza sana mzee Mfugale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mkurugenzi wa *SUMATRA* kwa kudhibiti usafiri wa majini na nchi kavu. Ajali nchini zimepungua sana, kwa hiyo, nampongeza sana Mr. Gilliard Ngewe kwa kazi nzuri hapo *SUMATRA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu katika Wizara hii. Hayati Dkt. Joseph Pombe Magufuli alitufundisha kwamba msemaekweli ni mpenzi wa Mung na mimi naomba nisema ukweli kwenye jambo hili. Waziri wetu wa Ujenzi na Uchukuzi bajeti hii imeanza vibaya na haina matumaini kabisa kwa Watanzania walio wengi. Huu ni ukweli ulio wazi, Wabunge wote wanalalamika na nimekuwa nikimtzama Waziri wangu pale na yeze mwenyewe amekata tamaa, bajeti hii haina matumaini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Jimbo la Lupembe viongozi wa Serikali tangu wakati wa Mheshimiwa Mkapa wamekuja Lupembe kutoa ahadi ya barabara ya Kibena mpaka Madeke kilometra 125. Wananchi wamekuwa wakifurika mara kwa mara kwenye kampeni wanapiga makof, wanashangilia kwamba barabara ipo Kibena inakuja. Mwaka jana Wizara hii ya ujenzi wameitengea barabara hii shilingi bilioni 5.9 wakatuambia wapo mbioni kutangaza *tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ndiye alikuwa Katibu Mkuu akatupatia shilingi bilioni 5 leo Wizara

ileile imepunguza fedha kutoka shilingi bilioni 5 mpaka shilingi bilioni 2. Mheshimiwa Waziri hebu nisaidie kujua nini kimekusibu kupunguza kutoka shilingi bilioni 5 mpaka shilingi bilioni 2? Wananchi wa Lupembe tumekosa ni nini? Fedha hii umeiondoa Lupembe umeipeleka wapi na kwa nini? Hilo nitaomba kwenye majibu yako utusaidie kujua ili tujue kwa nini fedha imepunguzwa, imepelekwa wapi kwenye umuhimu zaidi kuliko wananchi wa Lupembe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, sisi watu wa Mkao wa Njombe kwenye llani tumeahidiwa ujenzi wa uwanja wa ndege. Mheshimiwa Rais alipokuja Njombe tulifanya maombi, tukapiga na magoti tukaahidiwa kujengewa Uwanja wa Ndege Njombe. Nimeangalia kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri uwanja wa ndege hakuna lakini kwenye llani upo. Mimi nashindwa kujua mpango huu unatekeleza llani au hii bajeti mpya, siwezi kujua. Naomba Mheshimiwa Waziri utuambie ule mpango wa kujenga Uwanja wa Ndege Njombe umeishia wapi ili watu wa Njombe waweze kujua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu na la mwisho, naomba kushauri Serikali, tumeona kuna kazi kubwa inaendelea ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, bila shaka mizigo itaanza kuwa mingi na mizigo mingi ya bandarini inakwenda Mikoa ya nyanda za Juu Kusini hasa kwenda Zambia, Malawi na kadhalika. Naiomba Serikali wawekeze jitihada kubwa kufanya upanuzi wa barabara ya kutoka Igawa kuelekea Tunduma. Mimi napita Mbeya mara nydingi, barabara ya Mbeya ina msongamano mkubwa, haipitiki, kuna malori, bajaji na daladala. Kama tunapanua Bandari ya Dar es Salaam kuongeza mizigo hatupanui tunakopeleka mizigo kazi hii itakuwa ni bure. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Jamani watu wanaokumbuka barabara za Mbeya Mheshimiwa Waziri anasikiliza hapo kwa makini kabisa. Naona Mheshimiwa

Jenista ananiangalia sana naye ana barabara yake moja kule Peramiho. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mheshimiwa Dkt. Aloyce Kwezi ajiandae. Naona Mheshimiwa Issaay hayupo, Mheshimiwa Priscus Tarimo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Aloyce Kwezi na Mheshimiwa Ahmed Salum ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote kwa kutuletea bajeti nzuri, lakini ombi langu tuweze kuweka nguvu katika kutafuta fedha ili mipango hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kupongeza, nimeiona barabara ya Tengeru – Moshi – Himo ipo kwenye bajeti ambayo inasababisha msongamano mkubwa sana pale Moshi. Pia nimeuona Uwanja wa Ndege wa Moshi ambaao ni muhimu sana katika utalii na biashara, niwapongeze sana Wizara. Vilevile katika bajeti nimeona barabara za Chuo cha Polisi au Shule ya Polisi Moshi, nipongeze sana na kushukuru. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kuhusu barabara kuu hizi zinazojengwa na *TANROADS*, haswa barabara ya Moshi – Arusha, katika maeneo mengi haziwi na mitaro. Sasa maji yale ambayo wanayajengea makalvati na madaraja na kwa sababu ya *nature* ya Mkoa wetu wa Kilimanjaro na Manispaa ya Moshi huwa ni mteremko, kuna Kata za Ng'ambo, Msaranga, Mji Mpya na Miembeni zinaathirika sana na maji haya ambayo yametengenezewa makalvati lakini hayajawekewa mitaro kuyaelekeza katika mito. Niombe sana Serikali iangalie uwezekano wa kutengeneza mitaro ili maji haya yasiendelee kuleta maafa kwenye makazi ya watu (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara ambayo kwa muda mrefu tumeiombea *upgrade* na tulishaipanua na

tayari watu walishavunja nyumba zao kupisha upanuzi wa barabara hiyo. Barabara hiyo ni ya Sokoine ambayo inaanzia katika *roundabout* ya YMCA kwenda mpaka KCMC inaenda kuungana na barabara ya Mwika. Barabara ile inaunganisha barabara mbili za *TANROADS*, kwa sababu tulishaiombea ije *TANROADS* ili iweze kuunganishwa na kupanuliwa basi tunaomba tafadhalii sana Serikali iangalie umuhimu wa kui-upgrade barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara nyingine ambayo haipo moja kwa moja kwenye Jimbo langu lakini ni ya muhimu sana kwenye Jimbo la Moshi Mjini. Barabara ya *TPC* – Mabogini – Kahe na baadaye itaenda kuungana mpaka Chekereni. Barabara hii ina umuhimu kwanza kwa sababu ndiyo inayoleta chakula katika eneo la mjini, lakini pia hatuna maeneo kwa ajili ya *bypass*. Barabara hii ikiweza kutengenezwa inaweza kutusaidia illi iwe ndiyo *bypass* kwa ajili ya kuhamisha malori na kuondoa msongamano mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara iliyokuwa ya Arusha ya zamani inaitwa *Old Arusha Road* barabara hiyo ilikuwa ya *TANROADS* lakini baada ya *TANROADS* kuhamisha barabara kupeleka kwenye barabara hii mpya ya Arusha barabara ile imeteklezwa, lakini ina umuhimu sana iwapo lolote linatokea kwenye barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuitengeneza barabara ya *Old Arusha Road* ambayo inaanzia Moshi inakwenda Moshi Vijijini mpaka Jimbo la Hai. Barabara hii inaumuhimu sana katika maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisimalize bila kuongelea kidogo kuhusu *TARURA* ambayo ni sehemu ya bajeti hii. Tunayo matatizo mengi sana katika maeneo yetu na yalizungumziwa sana. Lipo lile suala la kupata fedha, mimi niendelee kusisitiza ni muhimu sana *TARURA* waongezeweh fedha ili angalau waweze kusimamia barabara za mijini na vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu wangu wakati fedha hizi zilipokuwa zinaletwa, halmashauri tulikuwa tunanunua mitambo, magreda na mashindilia kwa hiyo gharama za kurekebisha barabara haswa hizi ambazo siyo za lami inakuwa ni rahisi. Nitoe ushauri TARURA wawezeshwe kununua mitambo ili kazi iwe rahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Aloyce Kwezi atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara hili ya Ujenzi kwa kazi nzuri ambazo wanalfanyia Taifa letu na hususani Mkao wa Tabora ambao kwa kweli sehemu kubwa tunakwenda vizuri. Nisisite kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wake pamoja na Meneja wetu wa Mkao wa Tabora. Meneja yule kwa kweli ningeomba Wizara pengine hata mmuandikie barua ya pongezi kwa kazi nzuri ambazo anaziendeleza katika Mkao wetu wa Tabora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu maombi tu, pale Kaliua barabara ya kutoka Urambo imepita Kaliua na sasa ipo mpaka karibia na Usinge, lakini *bypass* ya kwetu pale ni kilometra 5.5. Kwa sababu barabara imepita kulia, imeacha Kata za Ushokola, Kaliua Mjini pamoja na Kasungu, maeneo haya yote naomba hili barabara ambayo inapita katikati ya Mji na Stendi na wafanyabiashara wakubwa wa Kaliua pale tuwasaidie tuweze kujenga ile *bypass* ili waone faida nzuri ya utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo naomba ni kuanzia Usinge, wanapojenga ile barabara ya Kazilambwa – Chagu, kutoka pale ni kilometra 4 kuingia Usinge Mjini. Naomba na penyewe wasije wakasahau kuhakikisha kwamba hata kama siyo mwaka huu, wakianza mwaka huu

Kaliua hizo kilometra 5.5 basi kwa Usinge mwakani wanaweza wakaweka kuingia mjini kwa sababu Usinge ni sehemu kubwa na ina kata karibu tatu na karibia asilimia 23 ya wakazi wa Kaliua wanapatikana Usinge pamoja na Kata ya Usenye. Kwa hiyo, tunaomba hizo lami kilometra 5 waweze kutusaidia pale Kaliua MJini na kule kilometra nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naendelea kuwashukuru, kuna barabara nimeona kubwa kweli ya kutokea Kahama – Ushetu – Igwisi – Kazaroho – Kaliua – Zugimbole kilometra 60 mpaka Mpanda, tumeona pale mmetuwekeea daraja. Kwa awamu hii mimi naunga mkono kwa kweli tujengeeni kwanza daraja, mmetuandikia hapa mnatutafutia fedha, hizo fedha mhakikishe mnazipata ili barabara hii ya kiuchumi ya kutokea Mpanda kupita Kaliua mpaka Kahama iweze kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, pale Kaliua ni *junction* abiria wanaotumia treni kutoka Kigoma wakifika Kaliua wakishuka wanatumia treni inayokwenda Mpanda; eneo lile naomba waongeze muda wa treni kwa sababu muda wa kusimama treni Kaliua ni mchache, ni dakika kumi na ile ni *junction* ina abiria wengi sana. Kwa hiyo, naomba waboreshe pale kwa kuongeza muda ili uwe wa kutosha. Jambo la pili pale pale ni tiketi, Kaliua tiketi hazitoshi, naomba watupe tiketi za kutosha sisi bado tunatumia sana usafiri wa treni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu hapo hapo, ni usimamizi kwenye vile vituo vidogo, kituo kama kilometra 34, kilometra 48 mpaka Mpanda. Naomba maeneo hayo toeni muda wa kutosha kwa sababu treni inasimama dakika moja unaona imeondoka, mnasababisha ajali. Kwa hiyo, naomba wananchi wa maeneo hayo waweze kuongezewa tiketi na muda wa kutosha kwa ajili ya kuhakikisha wanasafiri vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Wizara pamoja na kazi nzuri walizofanya, ile reli ya kutoka Kaliua kwenda Mpanda ni mbovu mno, wanatumia saa kumi. Sasa saa 10

kwa kilometra chache hizo karibu kilometra 180, naomba waiboreshe wakati tunasubiri hiyo *Standard Gauge* ambayo inakuja, waikarabati reli hiyo vizuri tupunguze hata muda wa kusafirisha mazao yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nirudie kuipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya lakini nawaomba wasisahau kurekebisha zile kilometra 5 za Kaliua mjini pamoja na taa za barabarani, maana wale wananchi wakifika tu Urambo, wanaona Urambo *bypass* yao ipo safi na taa za barabarani wanaauliza Mbunge yupo wapi nami napenda nirudi awamu ijayo. Ndugu zangu chondechonde nawaomba kabisa kwenye bajeti hii muendelee kuwa wasikivu na kunihakikishia mmeniwekea hizo kilometra 5. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nawashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Salum atafutatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja ya Wizara yetu ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza michango mingi sana ya Waheshimiwa Wabunge ambayo ni mizuri sana. Moja katika mambo ambayo ni muhimu sana huko tunakokwenda ni suala zima la barabara zetu. Katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi barabara ambazo zipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 nadhani hizo zipewe kipaumbele namba moja na barabara ambazo ziliahidiwa na Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na zenyewe ziwe katika vipaumbe vya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, kwa mfano, katika Jimbo la Swola kuna barabara inayotoka Manawa - Misasi - Swola - Mwakitolyo - Kahama imefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka

2010 na ilikuwa ndani ya Mpango wa *Millenium Challenge Funds*. Baada ya zile fedha kuondoka barabara hii imesahaaulika mpaka leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa barabara hii inaunganisha Majimbo ya Mwanza Mjini, Misungwi, Solwa na Msalala kwa maana ya Jimbo la Kahama. Majimbo matano au sita yanaunganishwa na barabara moja hii. Wafanyabiashara wa Rwanda, Burundi na nchi zote jirani huwa wanakuja mpaka Solwa na Nyabukande kwa ajili ya biashara ya mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni ya Solwa - *Old Shinyanga* na yenyewe imo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi yenye urefu wa kilometra 60. Mimi nipo kwenye Kamati ya Miundombinu na nilimueleza Waziri jambo hilli, tupo pamoja sana katika utekelezaji wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwenye hotuba ya Waziri nimeona *airport* ya Shinyanga Ibadakuli, zimewekwa shilingi bilioni 3.6. Mwaka huu *airport* ya Shinyanga inakwenda kujengwa baada ya kuilalamikia kwa muda mrefu. Naishukuru sana Serikali kwa kutusikiliza awamu hii. Sasa hivi wananchi wa Shinyanga watakuwa hawaendi tena Mwanza baada ya kukamilika *airport* hii tutakuwa tunapandia hapo hapo Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongelee suala zima la bandari. Tanzania hii kuna bandari 89 lakini 66 zipo kwa mujibu wa Sheria Na.17 ya mwaka 2004 na zinasimamiwa na Wizara moja kwa moja. Kati ya bandari hizi, bandari 12 zipo kwenye Bahari ya Hindi, bandari 24 zipo Ziwa Victoria, bandari 19 zipo Ziwa Tanganyika, bandari 11 zipo Ziwa Nyasa na kuna bandari nyingine ndogo ndogo. Bandari ni kitu kikubwa sana, Bandari ya Dar es Salaam inachangia kwenye Pato la Taifa zaidi ya asilimia 30. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua tani milioni 9 alizosema Mheshimiwa Waziri, ukatoa mizigo ya *transit* ukaacha mizigo ya ndani, kodi ya bidhaa ni zaidi ya kontena

laki moja na elfu arobaini mpaka kontena laki moja na elfu sitini ni *2.5 trillion to 3 trillion per year* bandari peke yake inaisaidia *TRA* kukusanya mapato ya nchi. Kwa hiyo, bandari siyo jambo la mzaha mzaha hivi, ni jambo kubwa lakini ipo kama idara ndani ya Wizara ya Uchukuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua Bandari ya Durban wanahudumia tani milioni 31, Bandari ya Beira wanahudumia tani milioni 7 na *target* yao ni kwenda tani milioni 11 kwa mwaka, ukichukua Bandari ya Mombasa wanahudumia tani milioni 12 kwa mwaka na hizi bandari ni washindani wakubwa sana wa Bandari yetu ya Dar es Salaam.

Nakumbuka wakati ule tuliongea sana hapa ilikuwa kuna tatizo kubwa sana tulilingiza sheria ya kutoza *VAT on auxilliary goods* kwa maana ya *transit* ikatusababishia matatizo makubwa mno nchi jirani wote wakaondoka wakaenda kutumia Bandari ya Mombasa. Tulipoongea hapa Serikali yetu ilikuwa sikivu ikaondoa na sasa hivi wateja kutoka Rwanda na Zaire wamerudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nataka kumalizia, naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu afikirie bandari iwe Wizara Kamili ili tuweze kutoka kwenye milioni 9 twende kwenye milioni 12, 15 mpaka 20 ili iweze kuchangia kwenye asilimia zaidi ya hamsini ya Pato la Taifa. Bandari siyo jambo dogo, Singapore asilimia 80 ya mapato yao yanatoka kwenye bandari.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza umeniongezea dakika moja ungenipa dakika mbili ningeshukuru sana. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Hassan Mtenga ajlandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika bajeti iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia kuhusu fidia kwa viwanja vya wananchi wa Kata ya Mkonze lile eneo la Miganga *West* na Miganga *East* ambapo kunapita njia ya reli ya *SGR*. Mara ya kwanza walitathmini wakalipa watu lakini wametathmini mara pili mpaka sasa hivi tayari barabara zimeanza kupita katika viwanja vya watu lakini fidia kwa wananchi ambao wametathminiwa mara ya pili hajifanyika.

Kwa hiyo, tunaomba Wizara ituambie ni lini wananchi hawa watalipwa ili waweze kununua viwanja vingine hasa kwa kuzingatia kwamba viwanja hapa Dodoma ni ghali sana. Kwa hiyo, wanapocheleweshewa fidia watashindwa kununua viwanja vingine ili waweze kuendelea na maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili, napenda kuongelea Bukoba Vijijini Jimbo ambalo nimegombea mimi na nimesema ni lazima nitasaidia wananchi hawa ambao kwa muda mrefu wamekosa mtu wa kuwatetea. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bukoba Vijijini ni Jimbo ambalo limetelekezwa kwa muda mrefu tangu uhuru. Wananchi wa Bukoba Vijijini ni wakulima wa migomba, ni wakulima wa kahawa na sasa hivi wamepanda miti sana. Kwa hiyo, kuna mazao mengi sana, kabisa kabisa ya mbao. Tangu uhuru hatujawahi kupata barabara ya lami. Bukoba Vijijini imezungukwa na Jimbo la Bukoba Manispaa, Misenyi, Muleba Kaskazini na Karagwe. Kwa hiyo, hakuna mahali popote ambapo pamefunguka ili watu waweze kupitisha mazao yao waweze kuendeleza uchumi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia katika kitabu cha ...

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** ...cha Waziri ukurasa wa 167.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ritta Kabati.

## TAARIFA

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa nataka tu nitoe taarifa kwa mchangiaji kwamba Jimbo la Bukoba Vijiji halina mtetezi wakati kuna Mbunge wa Jimbo ambaye siku zote huwa tunamwona anauliza maswali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipokei kwa sababu Mbunge amekuwepo zaidi ya miaka 15 na hatuna barabara. Kwa hiyo, sasa mnataka niseme nini? Hebu niachie nitetee wananchi, ndiyo kazi ya Wabunge iliyotuleta hapa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Waziri ukurasa wa 167 kuna barabara zimeandikwa hapo, naomba Waziri anisikilize, muda ni mchache. Kuna barabara ya kutoka Mutukula – Bukoba – Mtwe – Kagoma, wametenga fedha, shilingi bilioni moja kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Sasa naomba niulize, hii barabara ipo ya lami, unafanya upembuzi gani? Mnapembua nini, barabara ambayo imeshatengenezwa? Pale katika hiyo shilingi bilioni moja, kuna barabara ambayo inatoka Bukoba Mjini – Businde – Maruku

– Kanyangereko; pia, kuna barabara ya Kanazi kutoka Kyetema – Ibwera – Katoro – Kyaka; naomba niulize, hii barabara ambayo inafanyiwa upembuzi usioisha, inakamilika lini? Kwa sababu watu wa Bukoba Vijijini tunaumia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee kitu kingine; kuna daraja linaitwa Karedé. Daraja hilo haliwezi kupidisha mizigo tani 40 na watu wote ambao wanafanya biashara ya mbaو wanapaswa kuzunguka sasa, kutoka eneo hilo la Ibwera, hawawezi kupidisha mizigo katika daraja lile, wanapaswa wazunguke mpaka Kyaka kwenda Misenyi, yaani wanakwenda kwenye Jimbo lingine halafu warudi Bukoba Manispaa halafu waje kuelekea njia ya Biharamulo. Unaweza kuona adha tunayoipata. Kwa hiyo... (*Makofî*)

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Rweikiza Mbunge wa Bukoba Vijijini, anataka kukupa taarifa.

## TAARIFA

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kama ifuatavyo: kwamba barabara ya Kyetema – Ibwera – Katoro hadi Kyaka imo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka huu; na hivi ninavyozungumza, tumepata shilingi bilioni moja za upembuzi yakinifu. Barabara ya Busimbe kupita Rugambwa kwenda Maruku hadi Kanyangereko imo kwenye llani ya uchaguzi na hivi ninavyozungumza ina fedha ya upembuzi yakinifu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kuanzia Bukoba Mjini kupita Kata tano hadi Rubafu imejengwa kwa asilimia 51 kwa kiwango cha lami katika miaka hii mitano tunayoendelea nayo. Barabara ya kuanzia Kyetema - Katerero hadi Kanyinya ina lami na kazi zinaendelea kwa

kiwango kikubwa katika Jimbo la Bukoba Vijijini. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, unapokea taarifa hiyo kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini?

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipoeki, lakini ninachosema, mnaona ushindani wa kisiasa ulivyo mzuri! Kwa hiyo, tunashindana na wananchi watafute maendeleo; na ndiyo kazé ya kisiasa. Kwa hiyo, sasa mwenzangu, mtani wangu wa jadi na wewe sasa umetoa maneno leo ili watu wasije wakakuita bubu. Kwa hiyo,...(*Makofi*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Usiseme uongo.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka ni Jimbo la Bukoba Vijijini liweze kupata barabara.

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa. (*Makofi*)

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka ni wananchi wa Bukoba Vijijini waweze kuendeleza maisha yao. Kwa hiyo, hapa haya mambo hili Bunge tunaweza kusema *is a political policy*, lakini lazima tuseme na lazima tuseme. Naye akisema, aseme yake, mimi nasema yangu. Kwa hiyo, niliyoyaona kama anaona udhaifu, ni lazima niuseme na lazima ziwepo ajenda. Kwa hiyo, lazima Bukoba Vijijini tuisemee kuhakikisha kwamba Jimbo hili linapata maendeleo yake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kwa *TARURA*. Barabara nydingi za Kata katika Jimbo la Bukoba Vijijini ni mbovu na *TARURA* haina uwezo wa fedha. Sasa Halmashauri kwa Sheria ya *TARURA* wanapashwa na wao kuchangia katika kutengeneza barabara, lakini uwezo wa kutoa michango haupo. Mimi napenda kushauri kwamba sasa Serikali ifikirie namna ya kurejesha baadhi ya mapato, yaani

vile vyanzo vya mapato viliviyowekwa na Serikali, vinaweza kurejeshwa ili na Halmashauri yenyewe iweze kupata pesa za kusaidia *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye Kata za Kibirizi; na ninaomba huyu mtani mwenzangu anisikilize. Kibirizi...

**MBUNGE FULANI:** Ehe!

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** ...Ruhunga, Chamlaile, ndugu yangu ukipita na gari unatengeneza barabara wewe mwenyewe kwa gari yako. Anajua, kwa mfano nimwambie kutoka Kibirizi kwenda Kamuli...

**MBUNGE FULANI:** Ehe!

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** ...kwenda Akashalaba, wewe ulipitaje pitaje? Lazima utengeneze barabara wewe mwenyewe kwa gari yako. Kwa hiyo, ninachoomba kusema ni kwamba Jimbo la Bukoba Vijijini halijakaa vizuri, barabara siyo nzuri na hazipitiki kwa mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi/ Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Wao wao! (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Msongozi atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Mtenga na Mheshimiwa Teckla Ungele ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia namshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa uzima hatu niweze kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kupongeza ushindi wa kishindo wa Majimbo mawili ya

Kigoma; Jimbo la Buhigwe na Jimbo la Muhamwe. Kwa kifupi sana napenda niwataje makamanda ambao walikwenda kwa niaba ya Wabunge wengine wote kufanya kazi. Hawa walikwenda *front line*. Napenda kumtaja *Major General Shangazi*; Mheshimiwa Shangazi, pia *Major Aeshi, Major Jacqueline Msongozi, Captain Bupe Mwakang'ata, Captain Mariam Ditopile* na Afande Santiel, ambao walishiriki kikamilifu katika Jimbo la Buhigwe na kuhakikisha ushindi wa asilimia 83. Hongera nydingi sana kwao. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka sasa niende kwenye mchango wangu. Napenda kuzungumzia Daraja la Mkenda ambalo linakwenda Mitomoni...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline hivyo vyeo vya kijeshi sijajua kama mmetunukiwa kule au ndiyo unatunuku sasa hivi humu ndani! (*Kicheko*)

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hii ni katika shughuli mahususi, inaruhusiwa. Daraja la Mkenda kwenda Mitomoni Wilaya ya Nyasa kuna kivuko kinaitwa Limonga. Kivuko hiki kimekuwa na changamoto kubwa sana. Kivuko hiki kina upana wa karibia mita 100 kama sijakosea, lakini pia napenda tu kusema, Serikali hii badala ya kuweka tu kile kivuko cha kuwabeba wale watu na kuwavusha, basi lijengwe daraja moja kwa moja kwa sababu tayari imeshaleta maafa makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kivuko hicho tarehe 1 Julai, 2016 wananchi 10 walipoteza maisha akiwepo Zuhura, Awetu, Fadhili, Rajabu, Bahati, Khadija, Saidi, Selemani, Omari na Juni. Kana kwamba haikutosha, mwaka 2020 mamba alipindua mtumbwi. Sasa itoshe tu kuona kwamba Watanzania wenzetu wanapoteza maisha sana katika kivuko kile. Naiomba sana Wizara, ione umuhimu wa kwenda kuweka mikakati mizuri ambayo itasaidia na itaondoa adha hii ambayo imekuwa ikitababisha wananchi hawa wanapoteza maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie Bunge lako Tukufu hili kumwomba Waziri mwenye dhamana aongozane nami baada ya Bunge hili, pamoja na Mbunge wa Jimbo la Nyasa na Mbunge wa Jimbo la Peramiko, twende kwa pamoja kwenye kivuko kile kuhakikisha kwamba mikakati mizuri inawekwa kwa ajili ya kuokoa ndugu zetu hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia barabara ya kutoka Mtwara Pachani kuelekea Tunduru kuititia Ruchiri – Rusewa – Magazini – Narasi – Mbesa – mpaka Tunduru. Barabara hii ina urefu wa kilometra 300 ni barabara ya kimkakati ambayo itasaidia kurahisisha usafirishaji lakini kuchochea kasi ya uchumi katika Mkoa wa Ruvuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, napenda nizungumzie mpango mzuri wa Serikali wa kuhakikisha kwamba mijii mikuu inapokuwepo basi barabara za pembezoni zinawekwa, barabara ambazo haziingiliani na mambo ya malori katikati ya mijii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kuizungumzia barabara ya *bypass* ya kutoka Mretele kwenda Ruwiko ya Songea Mjini yenye urefu wa kilometra 11. Barabara hii imekuwa na msongamano mkubwa wa magari, bajaji na pikipiki. Imekuwa ni rabsha na ajali zimekuwa nyingi sana. Vilevile ni barabara ambayo ni ya muda mrefu sana; siku zote tumekuwa tukiambiwa upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu, jamani ni urefu wa kilometra 11. nikuombe Mheshimiwa Waziri funga macho, hebu nenda kajenge ile barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii niseme tu, huu ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba hakuna msongamano katikati ya mijii. Tunaangalia katika Mji wa Iringa, hakuna msongamano, barabara ile kule chini inapita malori. Vile vile ukiangalia Mwanza na Dar es Salaam, hakuna msongamano wa malori.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie barabara ya *bypass*; nimekwenda Mbeya tukiwa ziara na Wabunge, tukafika Mbeya...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...Taarifa amekataa Naibu Spika. Mnani potezea muda bwana! (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

## T A A R I F A

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika... (*Kicheko*)

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, anataka kukulisha maneno mdomoni huyu Mheshimiwa. Namshangaa anasema Mwanza hakuna msongamano; lini umetoka Mwanza wewe! Mwanza kuna msongamano wa kutisha kama Mbeya ilivyo na Dar es Salaam na Dodoma sasa hivi kuna msongamano. Majiji yote yana msongamano. Jiji huwezi kulinganisha na mkoa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam!

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Ngoja kwanza. Kaa tu.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani nilieleza jana wakati tunafunga Bunge hapa. Misongamano inatofautiana. Kuna msongamano wa magari kushindwa kupita kabisa kwa sababu ya utelezi, kuna msongamano unaoweza kusababishwa na mvua kama Dar es Salaam ambako wanahitaji mitaro. Kwa hiyo, misongamano inatofautiana. Nadhani tuelewane hapo. Mheshimiwa Mbunge ukiwa na hoja, huwezi kumwuliza Mbunge, yaani unakuwa unampa taarifa, usimuulize swalii kwa sababu siyo kazi yake yeye kujibu.

Wewe unampa taarifa kwamba, unaanza ukisema, naomba kumpa taarifa kwamba Mwanza kuna

msongamano barabara moja, mbili, tatu; moja, mbili, tatu. Huwezi kumwuliza swali kwamba wewe umepita lini; na msongamano upo?

Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, malizia mchango wako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tabasam hiyo siyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kama ifuatavyo. Mwezi wa Tatu, Wabunge...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, muda wako umeisha Mheshimiwa, nakumbushwa hapa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...tulipata fursa ya kwenda Mbeya...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...na nilikuta kule kuna msongamano wa hatari sana. Kilometra 48.9 kutoka Uyole kwenda Songwe, sasa mimi niombe...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Hassan Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Kwanza nilikuwa namwangalia hapa Waziri wa Ujenzi, mara nyngi amekuwa anajishika kichwa, anajishika shavu, kwa kweli tunapaswa tumsaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu Mtwara tuna barabara ya Mnivata ya kilometra 160; Mnivata - Mtwara mpaka Masasi. Barabara ile kwenye bajeti humu tumetengewa shilingi bilioni tatu. Kwa hali ya kawaida ukipiga mahesabu ya kilometra moja kujenga barabara ya lami, lami *standard* nadhani ni zaidi ya shilingi bilioni moja na *something*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi shilingi bilioni tatu tunakwenda kutengenezewa kilometra tatu. Barabara hii sasa ina miaka takribani 10. Katika bajeti zote za miaka 10 tumetengenezewa kilometra 50. Naomba kwamba sasa kuna kila sababu, kwa kuwa barabara hii inaunganisha baadhi ya barabara zinazokwenda kwenye wilaya nyngine, pia ni barabara ya kibiashara. Kwa hiyo, tunakosa kufanya biashara zile za kisasa hasa kwa kutumia barabara hiyo kwa sababu barabara siyo nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna barabara ya kutoka Mtwara kuelekea Mahurunga; barabara hii hatujaona kwenye bajeti kama imetengewa fedha. Barabara hii toka imeanza kutengenezwa sasa hivi ina kiwango cha lami kilometra ambazo hazizidi sita au saba, takribani ina miaka zaidi ya 15 na iko *TANROADS*. Naomba barabara hii sasa itengewe fedha za kutosha ili tuweze kupata barabara ya lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kule inakokwenda ndiyo kwenye mpaka baina ya Msumbiji na Tanzania, lakini kumekuwa kuna matukio mengi ambayo yanatokea, watu wetu, watu wa Idara, watu wa usalama na watu wengine wanashindwa kufika kwa wakati kwenye maeneo hayo, kwa sababu barabara ni mbaya hazipitiki. Tunaomba Serikali mtusaidie kwenye hii barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie barabara ya Kibiti – Lindi – Mtwara. Barabara hii kwa sasa hivi haipitiki, ni barabara ambayo tayari imeharibika, imekufa kutokana na malori ambayo yanabeba ufuta, korosho, na mahindi yanayopelekwa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwako, tunayo Bandari ya Mtwara; bandari hii imetumia shilingi bilioni 157 na fedha zile tumeziwekeza pale ili bandari ile ifanye kazi. Nataka nitoe angalizo, leo kuna makampuni yanayoleta mafuta, Serikali imeelekeza kwenye makampuni yanayoleta mafuta kwamba kwa watu wa mikoa ya kusini, itumike bandari ya Mtwara wa kubeba mafuta. Ni kitu gani kinashindikana sasa tukaelekeza kwamba korosho zote za Mtwara zipitie Bandari ya Mtwara; ufuta wote unaolimwa Lindi na Mtwara upitie Bandari ya Mtwara; na mahindi yote yanayolimwa yapitie bandari ya Mtwara? Kuna nini hapa? Naomba kufanya *maintenance* kwenye barabara yetu ya lami kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam *a lot of shillings* tutazitumia pale. Hivyo *maintenance* hizi tunazozifanya za kila siku kama tungeamua sasa fedha hizi tuzielekeze kwenye ujenzi wa barabara tungkuwa hatulalamiki hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo barabara ya Mtwara – Kibiti – Lindi, kila ukipita barabara ile, kila baada ya miezi miwili unakutana na shida. Mkandarasi yuko barabarani na anatengeneza barabara ile kwa ajili ya *service*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na Mheshimiwa Agness Hokororo, ajiandae.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Awali ya yote, napenda kushukuru Wizara hii, kwa ajili ya ujenzi unaoendelea, sasa hivi mkandarasi yupo pale kwenye barabara ya Nanganga

kwenda Ruangwa. Ila ombi langu naomba ujenzi uende na viwango, lakini pia uende kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nachingwea kwenda Liwale, kilometra 130; Nangurukuru – Liwale, kilometra 230; na Kiranjeranje - Namichiga – Ruangwa, kilometra 120. Hizi zote zipo kwenye hatua za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ufikie wakati zijengwe kwa lami. Kwa nini naomba hivyo? Barabara hizi kuwa katika kiwango cha lami ni muhimu sana kwa sababu usafirishaji wa watu, lakini usafirishaji pia kwa wagonjwa, lakini usafirishaji wa mazao ya korosho na ufuta ambayo ni mazao ya biashara kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposhindwa kusafirisha mazao haya Maisha ya watu kule Mkoa wa Lindi yanakuwa duni. Naamini kabisa siku moja ukipata bahati kwenda Liwale utaona kabisa huku ulipo ni kugumu sana, lakini kule kunapatikana korosho na ufuta kiasi kwamba unaweza kukwamua wananchi wa kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ni mfanyabiashara gani atakayehangaika kwenda kununua korosho kule, badala ya kwenda kununua kwenye maeneo ambayo yanapitika. Naomba ufike wakati kuwepo na barabara ya lami kwenda Liwale na kwingineko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea pia habari ya Uwanja wa Ndege wa Nachingwea. Nimeona kwenye Randama kunataka kuwekwa lami, naomba hilo lifanyike kwa umuhimu wake sana. Uwanja wa Ndege wa Nachingwea una umuhimu sana kwa sababu pale ni *center* mtu wa Liwale, Ruangwa, Masasi anaweza kusafiri kupitia Nachingwea kuliko kwenda Mtwara kilometra 200 kutoka Masasi. Pia itarahisisha wawekezaji, kule kwetu sasa hivi kuna madini, kuna madini Nditi, kuna madini Ruangwa, ni rahisi kwa wafanyabiashara wawekezaji kupitia kuanzia Nachingwea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na-share tu *experience* nilioipata wakati wa mazishi ya Mzee Mkapa. Ndege nyingi, viongozi wengi walitua katika Uwanja wa Ndege wa Nachingwea, lakini uwanja ule kwa sababu ni wa vumbi adha iliyopatikana wanaifahamu mmojawapo akiwa Mheshimiwa Spika mwenyewe wa Bunge Ietu, Mheshimiwa Ndugai, anapafahamu Nachingwea. (*Makofii*)

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ungele kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamida Abdallah.

## TAARIFA

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza hivi sasa kwamba Uwanja wa Ndege wa Wilaya ya Nachingwea, atambue kwamba tumerithi kutoka kwa wakoloni kikiwemo pia Kiwanja cha Lindi Mjini. Kuna umuhimu mkubwa sasa Serikali kuona namna bora ya kuboresha uwanja ule, tena kwa haraka zaidi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, napokea kwa mikono miwili taarifa hiyo. Uwanja ule pia ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama. Nachingwea tuna vikosi vya jeshi, kwa hiyo kunavyokuwa hali yoyote ya kuhitajika usalama ndege pale zitatua na mambo mengine yataendelea. Ufikie wakati Wizara iiangalie Nachingwea na Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa ujumla. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Daniel Pallangyo ajiandae.

Mheshimiwa Pindi Chana hayupo, Mheshimiwa Agnes Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Pallangyo na Mheshimiwa Twaha Mpembenwe aijandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii. Kwanza niungane na mzungumzaji aliyetangulia, Mheshimiwa Ungele kusitiza barabara ya Masasi – Nachingwea ambayo ndio pia inakwenda mpaka Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyininge huwa hatueleweki, lakini pia nina maswali madogo ambayo ninajiliza na pengine Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa ufanuzi atuambie. Sera ya barabara inasema ni lazima kuunganisha mkoa kwa mkoa, hivyo watuambie wameunganisha kwa kiwango cha lami Mkoa wa Mtwara na Lindi kutoka Liwale – Nachingwea na Masasi Lami imepita hewa gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu wakati mwagine hata tunajichanganya wenyewe, kama Serikali hii hii inasema masuala ya uvezeshaji wananchi kiuchumi, moja ya kigezo ambacho kinapaswa kuzingatiwa ni uimarishaji wa miundombinu ikiwemo barabara.

Sasa maeneo ambayo yanatoka mazao ya korosho, huko Nachingwea, huko Liwale ambayo inapaswa sasa kuja kusafirishwa huku Bandari ya Mtwara na kipande cha Masasi – Nachingwea ni kilometra 45 tu. Nimepata bahati ya kusikia ahadi za viongozi, lakini pia kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tangu mwaka 2010 - 2015 na 2015 – 2020, lakini mpaka sasa barabara hiyo haijaguswa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hokororo, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nataka nimpe taarifa mzungumzaji. Barabara ya Nachingwea – Masasi imefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2014, lakini mpaka leo bado inatafutwa fedha ya kujenga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea na tena imeniwahi, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama upembuzi yakinifu ulikamilika tangu 2014 pamoja na kwamba ahadi ilikuwa ni ya miaka 20 sasa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie maana kwenye taarifa yake inasema Serikali inatafuta fedha na ikisema Serikali inatafuta fedha, hilo jambo ni kama halipo.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI amekwenda Nachingwea, kimsingi hata sasa hivi kama ungenipa nafasi niongozane na Naibu Waziri ama yoyote kwenye Serikali. Ukiwa mjamzito kwenye barabara ile ya Masasi – Nachingwea unapata, sijui nisemeje?

**WABUNGE FULANI:** Unazaa.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, unazaa kabla ya wakati. Ile barabara nikiongea kwa lugha ya kikwetu si dhani kama nitaeleweka, lakini ni kwamba unakuwa unatingishika kuanzia unapoanza mpaka, hapa wiki iliyopita niliuliza swalii, wakasema fedha imetengwa lakini tuendelee kusubiria. Jamani! Mkoaa wa Mtwara na Mikoa hii ya Kusini niwakumbushe tu, kwamba iliusika kikamilifu katika kuziletea ukombozi Nchi za Kusini mwa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda Serikali ama Waziri aje kutuambia, hivi ile barabara haitengezwi kwa sababu kuna vikosi vya majeshi kule? Kwa hiyo wananchi wote waendelee kuishi nao kijeshi! Sasa unasemaje

uwezeshaji wananchi kiuchumi, miundombinu hajakamilika, ni kwa miaka 20 iko kwenye ahadi, upembuzi umekamilika, nini kikwazo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tunajua kwamba Nchi hii ni kubwa na Serikali ina mzigo mkubwa, lakini iko haja ya kuangalia maeneo ambayo kimsingi yameachwa nyuma kwa muda mrefu. Hawa wananchi sehemu ambayo na nilisema hapa uliponipa nafasi ya swalil ya nyongeza, sehemu ambayo nauli ilipaswa kuwa shilingi 750 wanalipa shilingi 6,000, huu mzigo unakwenda kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Waziri atakapokuja hapa bila kutupa maelezo ya kutosha, mimi siwezi kupiga sarakasi kwa sababu najua, lakini tunakwendaje kwenye bajeti hii bila ya kuwa na matumaini kwamba angalau hicho kipande tutatengenezewa. Kwa sababu hili habari ya kutengenezwa kila mwaka ndio kila siku mvua ikija inaosha, mvua ikija inaosha, lini Serikali itaanza kutekeleza kipande cha kilometra 45 kuunganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Mpembewenwe na Mheshimiwa Kasalali Mageni ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo kwenye hii bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ambayo ni Wizara nyeti kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Watendaji wote, Katibu Mkuu pamoja na Wakuu wa Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara, kwanza kwa kazi nzuri sana ambayo wanafanya kutandika barabara za lami nichini, lakini pia na hotuba nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo ina walakini, kwa sababu nimeipitia yote sijaona Arumeru Mashariki ikipewa hata mita moja ya barabara. Kwa hiyo nasema ina kasoro pamoja na kwamba nimempongeza Waziri lakini bado hotuba yake ina kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja na kuchangia na nianze na ukarabati wa kawaida (*routine maintenance*). Kwa muda mrefu nimekuwa na-observe, natazama ukarabati wa barabara zetu ambazo zimejengwa kwa fedha nyingi sana, lakini ukarabati unachelewa na baadaye kama unafanyika, unafanyika kwa utaratibu ambao ndivyo sivyo, kiholela holela tu. Wanafanya *part works*, wanarudia *part works*, mwisho barabara zetu zinakuwa nundu, uendeshaji unakuwa ni mgumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wwizara, irudie utaratibu wa zamani. Ilikuwa ukifanya *part works* miaka miwili unafanya *surface dressing*, unapiga *layer* moja ya lami barabara inakuwa mpya. Turudie kama tulivyokuwa tunafanya zamani kwenye ukarabati wa barabara zetu baada ya kuzijenga, maana yake tunatumia fedha nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wananchi wetu wengi wanaoishi kwenye miteremko ya milima mirefu, hususani Nyanda za Juu Kusini, Nyanda za Juu Kaskazini wameachwa, hawajapelekewa barabara nzuri, maisha yao yanaendelea kuwa duni. Tunaishauri Serikali sasa ichukue hatua mahsusii ifanye *special program* ya kujenga barabara za lami kwenda milimani kwenye wananchi wengi ili waweze kuishi maisha ya kawaida na wao waweze kupata neema ya barabara nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo langu, kuna barabara inaitwa Barabara ya Mbuguni, inaanzia Tengeru kwenda Mererani inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara. Barabara hii ni muhimu sana kwa maana ya kwamba inafungamanisha uchimbaji wa *Tanzanite* kule Mererani na masoko ambayo yapo Mjini Arusha. Barabara

hii ina kilometa 27, ikijengwa kwa kiwango cha lami itafupisha safari ya sasa hivi kutokea Mererani kupitia K/A kwa ajili ya kupeleka *Tanzanite* sokoni ni kilometa karibia 80. Badala ya kwenda kilometa 80 kupitia barabara ya Mererani – Tengeru – Arusha unakwenda kilometa 30 na itachochea sana biashara ya madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya King'ori; barabara hii huwa naiongea mara kwa mara. Barabara hii iko kilometa tatu kutoka kwenye mpaka wa Kilimanjaro na Arusha. Barabara hii inazunguka mlima Meru kwa upande wa mashariki, Mto Meru pamoja na Hifadhi ya Arusha inapandisha Kaskazini inakwenda kutokea Oldonyo Sambu kuelekea Namanga. Barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami itakuwa kama *by-pass*. Kwa hiyo niishauri Serikali ifanye kama mradi mkakati ijengwe kama *by-pass* kwa kiwango cha lami. Itainua kiwango cha maisha ya wananchi wanaoishi eneo lile hususani Kata nane za Malula, King'ori, Maruvango, Leguruki, Ngarenanyuki, Uwilo, Oldonyo-Wass, Angabobo. Pia itakuwa kichocheo itafanya *accessibility* kwenda Hifadhi ya Arusha kuwa rahisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo letu limesahaulika sana. Mheshimiwa Waziri aki-*check* kwenye kumbukumbu zake atakuta kwamba kwenye barabara Arumeru Mashariki haijaguswa kwa zaidi ya miaka 10 iliyopita. Bahati mbaya kwenye mpango, kwenye llani ya Uchaguzi hatukupata hata mita moja ya lami, lakini Mungu akatukumbuka, Marehemu aliyekuwa Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipokuja kwenye kampeni alituahidi kujenga ile barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Waziri kwamba, maneno ya Rais ni *decree*, maneno ya Rais ni kama sheria, lakini bahati mbaya rais huyo ameondoka, tunaye rais mwingine ambaye amesema kwamba yaliyosemwa na ambaye yalikuwa yamedhamiriwa na marehemu tutayatenda, ni wosia. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akumbuke hili jambo na kuhakikisha kwamba safari hii, hii barabara inajengwa, tunaomba sana, sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata hizo barabara mbili, Arumeru Mashariki nchi itabadilika ile. Wananchi watafanya kazi zao vizuri, wananchi watatulia, wananchi walitupa kura nyingi sana kwa sababu tulisema habari ya barabara na kwa Wabunge wote mnasema kwamba barabara ndio bidhaa ambayo ilikuwa inatuuza sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Godwin Kunambi ajiandae.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ambayo ni muhimu sana. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa wasilisho zuri la bajeti ambayo walikuwa wamelileta mbele yetu ambalo linaweza kuleta matumaini kwa namna moja ama nyingine, ukizingatia kwamba kuna changamoto Wabunge wote tunafahamu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja kwamba leo, nimeomba Mwongozo, imekuwa bahati kubwa sana kwasababu nimeweza kupata meseji kutoka kwa Meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa akisema kwamba ndani ya wiki mbili zijazo ile Barabara ya Bungu – Nyamisati sasa inakwenda kutangazwa. Kwa tafsiri hiyo tunakwenda kumpata mtaalam kuanza hatua za awali za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri hiyo hiyo, japokuwa ulikuwa umetoa ushauri mzuri sana kwamba nibaki na mmoja, sasa kwa haya ambayo yameweza kufanyika naona wazi kabisa kwamba jambo lile la kupata mke wa pili linaanza kusogea karibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali hasa katika miradi mikubwa mikubwa hii. Naomba niishauri Serikali kwa tafsiri kwamba miradi mikubwa mikubwa jana Mheshimiwa Reuben alikuwa amejaribu kuzungumza mambo ya *finance model*, ni jinsi gani tutakavyoweza kui-*finance* hii miradi mikubwa mikubwa. Ni ukweli uliokuwa wazi Watanzania tunahitaji maendeleo, ni ukweli uliokuwa wazi, Watanzania wana matumaini makubwa sana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwani mengi makubwa yameweza kufanyika katika awamu zote hasa katika Wizara hii. Makubwa sana yameweza kufanyika na sina shaka Awamu ya Sita vilevile inakwenda kuyafanya mambo makubwa na mazuri hasa katika Sekta nzima ya mambo ya Uchukuzi na Usafirishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri hasa katika Mradi wetu wa *SGR*. Katika mradi huu tuangalle *financing model*, kwa sababu mradi utakapokuwa umeweza kukamilika tafsiri yake pana ni kwamba tunakwenda kuhuishaa matumaini upya ya Watanzania, sio tu katika maeneo ambayo yanapitiwa na mradi huo, lakini kwa Watanzania wote kwa ujumla wake. Kwa sasa tuweze kujaribu kuangalia, ndio maana naanza kurudia tena neno langu hili, lile suala la *PPP* lina shida gani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lilizungumzwa hapa Bungeni mwaka 2018 wakati sisi wengine tulikuwa hatua hata ndoto za kuja hapa Bungeni. Sasa shida iko wapi? Tujaribu kuangalia masuala haya kwa sababu tunapokwenda kukopa masharti yanakuwa mengi na Mheshimiwa Reuben amezungumza kwa kirefu sana na sidhani kama atakuwa ameeleweka vizuri. Alizungumza kwamba tunapokwenda kukopa tunapewa na masharti, wanatupa fedha na wakandarasi wanakuwa hao hao. Sasa sisi kama Serikali tujaribu kuweza kuangalia ni jinsi gani tunakwenda kuangalia suala zima la *PPP* na kuweza kukamilisha hii miradi mikubwa mikubwa. Huo ni ushauri wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili kwa Serikali, naiomba sana Serikali, bahati mbaya sana ama

bahati nzuri Wabunge sisi tunasoma hizi bajeti. Sio tu kwamba tukija hapa tunapiga makofi tunaondoka, hapana. Bajeti iliyokuwa imesomwa mwaka juzi, kuamkia mwaka jana, mwaka jana kuja mwaka huu kuna mambo yanakuwa yanaainishwa mle ndani. Wanavyosema kwenye bajeti hii kwamba upembuzi yakinifu umekamilika tunasubiri ujenzi, inasikitisha sana ukija tena katika mwaka huu tunaanza kumtafuta mtalaam wa kuweza kufanya upembuzi yakinifu. Tukifanya hivi tuna-*send wrong signal*/kwa wananchi ambao wana matumaini makubwa sana na Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba sana kwa wale wataalam wetu ambao wanaandaa bajeti hizi, naomba twende tukatoe tahadhari kule kwamba Bunge hili la Kumi na Mbili, hawa watu wanasoma. Tunasoma hizi bajeti zinavyokuwa, tunapitia nyaraka moja hadi nyingine. Kwa hiyo, tukija hapa na majibu tunayoyategemea sio majibu ya kisiasa siasa. Tunategemea tupate majibu ambayo yanakwenda kwenye uhalisia ili sasa wananchi wale waliokuwa wametupigia kura kwa kishindo na Chama Cha Mapinduzi kikawa kimeingia madarakani waendelee kuwa na matumaini na nchi yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naomba nzungumze, pamoja na uhalisia kwamba tayari nanyemelea kupata mke wa pili kwa sababu ya ile barabara ya Bungu – Nyamisati, pale kwetu vile vile kuna barabara ya kutoka Kibiti – Demani kwenda kule Mloka. Hii ni barabara muhimu sana kwa sababu kule ndiko mradi ule wa Mwalimu Nyerere unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, najua pamoja na mambo makubwa na mazuri ambayo tayari tumeshayafanya kama Serikali katika Sekta nzima ya Mambo ya Ujenzi na Uchukuzi lakini vile vile tuangalie. Nimewasifia hapa kwamba imefanya vizuri, sina maana kwamba eti kwa sababu Kibiti haikuwekewa bajeti ile nisiseme kwamba mmefanya vizuri, hapana! Mmefanya vizuri sana lakini tuweze kuangalia vile vile uwezekano wa kuweza kupatikana fedha za dharura ili pale watu wa Kibiti

na Demani kule ambako wananchi wangu wanakohoaa sana kwa vumbi na malori yanayopita pale kwa kupitia mizigo ile inayokwenda kule kutengeneza mradi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ikiwezekana Mheshimiwa Waziri ungekaa na wataalam wako kama kuna ka-emergency kule pembeni basi kaweze kutoka kale kafedha uweze kwenda kufanyika hatua za awali za upembuzi yakinifu ili sasa tuweze kuangalia jinsi gani tutakavyoweza kuokoa wananchi wale kuondokana na matatizo ya kifua wanayoyapata. Magari mengi sana yanapita pale, na haya mambo ukiona mtu mzima anapiga piga kelele, kuna jambo, Mheshimiwa Aweso huwa anasema hivyo. Ukiona mtu mzima anapigapiga kelele, kuna jambo, Mheshimiwa waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza hapa jana, alisimama kwa mara ya kwanza sikutegemea. Alisema kutoka pale Mbeya kwenda Tunduma kapata kilometra tano ndani ya miaka 6. Haya mambo ya kuona sana, sasa mtu mzima akiwa amesimama hivi, kuna jambo. Ninavyozungumza kwamba jamani nawataka wale wake wanenye, liko jambo! Wazee wameniahidi wale kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sitaki wewe mchawi wangu. Najua utalifanya hilo na nina imani sana na Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi hasa Serikali ya Awamu ya Sita kwa mambo makubwa na mazuri ambayo yanakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mheshimiwa Kassim Iddi Kassim ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii adhimu. Kwanza kabla sijazungumza naomba niunge mkono hoja ili nisije nikasahau. Siungi tu mkono hoja, ninayo sababu. Sababu ya msingi kabisa ni kwamba ile barabara ambayo nilikuwa ninasema, leo ni mara ya nne naizungumzia hapa Bungeni. Barabara

inayotokea Magu – Bukwimba – Ngudu mpaka Nhungumalwa yenyе urefu wa kilometa 71 sasa nimeona kwenye *Vote* namba 4162 imepangiwa kujengwa kilometa 10. Hiyo ndiyo sababu nimeunga mkono kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu tunaheshimiana sana, wewe ni kama kaka yangu na watu wa Kwimba wanakushukuru kwa hili. Lakini, wanao ushauri kwako. Katika *Vote* hii namba 4162 ambayo tumehangaika mimi na wewe mpaka naiona hapa umetupangia bilioni 1.5 nadhani mimi na wewe ni mashahidi kwamba bilioni 1.5 haiwezi kutosha kuanza kutujengea kilometa 10 kwenye hizi kilometa 71. Sisi tunataka kwa kweli tumeshaomba sana, sasa sasahivi tunataka mtujengee, msikomee kutuandikia hapa kwamba mnajenga kilometa na mmetenga billioni 1.5 halafu ujenzi usitokee katika Mwaka huu wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wazungumzaji wa mwanzo wamesema, ni lazima ifike wakati sasa vipaumbele hivi vitolewe kwa maeneo yote. Tumekuwa tukiona maeneo ya mjini ambayo yanaonekana kwa urahisi, ikitokea foleni kidogo tu naona zinajengwa *ring roads, fly overs*, lakini sisi watu wa vijijini inawezekana foleni zetu Mheshimiwa Waziti hauzioni, foleni zetu ni za mazao yanayoharibikia shambani kwa kushindwa kusafirishwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, foleni zetu sisi ni watu wanaolala njiani siku mbili kwa barabara kuharibika. Hamyaoni haya, lakini nchi hii ili uchumi uende vizuri na watu waache kuhamia mijini wabaki vijijini wazalishe ni lazima na vijijini huduma ziende. Barabara za vijijini zipitike, kule ndiko tunakolima mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Sumve mazao yakilimwa mfano kwenye Kata kama ya Mwandu, ukilima mazao wakati wa mvua ni mpaka usubiri kiangazi uje uyasafirishé na tela ya ng'ombe. Mkokoteni ule ndiyo unasafirisha. Sasa, na sisi tunayo haki kama watu wengine wanaobanduliwa lami na kuwekewa lami mpya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano natoa barabara ambayo haipitiki kabisa iko kichwani tu lakini haipitiki. Yaani ukitokea Goroma unaenda Shushi, unaenda Mwakaluto, uende mpaka Ngudu kupitia Ilumba, ile barabara ni ya kichwani, haipitiki wakati wa mvua lakini kule ndiko tunakozalisha mazao mengi ya mpunga. Ukitaka kwenda kutokea kwenye mnada mkubwa kabisa kwenye Wilaya ya Kwimba Wabungurwa, unaenda Ng'undya, barabara ile haipitiki lakini kule ndiko mazao yanazalishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa waziri, tufike wakati uangalie hii barabara ya kwetu ya msingi kabisa ambayo inatokea Magu kwenda Ngudu mpaka Nhungumalwa kupitia stesheni ya Bukwimba ni lazima sasa muijenge kwa kiwango cha lami. Maombi tumeomba sana. Tunaomba sasa hizi kilometra 10 zilizoandikwa kwenye bajeti tuzione. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini iko barabara ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Flatei Massay alitaka kupiga sarakasi hapa. Barabara hii inaanzia, ye ye alishia Maswa lakini ukitoka Maswa inakwenda mpaka Malya. Kutokea Malya inaenda mpaka Nyambiti. Kutokea Nyambiti inaenda mpaka Fulo, barabara hii imeahidiwa kwenye ukurasa wa 77 wa llani ya CCM kwamba itafanyiwa upembuzi yakinifu na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii itamsaidia mtu anayetoka Mwanza akapita Jimbo la Sumve akaenda mpaka Maswa – Meatu, akaenda mpaka Hydom Mbulu akasafirisha mazao yake na inarahisisha sana usafiri. Barabara hii ni ya kimkakati kwenye kuinua utalii wa Serengeti. Sasa barabara hii imekuwa ikiandikwa na kuachwa na kwenye bajeti sijaona ule upembuzi yakinifu niliuona kwenye llani kwenye bajeti sijaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa waziri, naomba sasa Wizara iipe kipaumbele barabara hii. Ijengwe kwa kiwango cha lami ili na sisi tupate kama wanavyopata wengine. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kassim Iddi Kassim, Mheshimiwa Jasson Rweikiza ajiandae.

**MHE. GOWDIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, pia, niipongeze Wizara kuanzia Waziri mwenyewe mwenye dhamana ya Wizara na Manaibu wake lakini pia na *Chief Executive* wa *TANROADS* mzee wetu Mfugale. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Kwa Mkoa wangu wa Morogoro pale Meneja wa *TANROADS* Mkoa Mhandisi Ntije, Mheshimiwa Waziri ikikupendeza aendelee kubaki na sisi Wanamorogoro tunamuhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepongeza Wizara kwa lengo kuu moja kwa sababu nimeona ukiangalia bajeti ya Waziri aliowasilisha imeelezwa tunakwenda kuanza ujenzi wa barabara sasa ya kiwango cha lami ya kilometra 50 kutoka Ifakara kwenda Mlimba – Kihansi. Tumetengewa kwenye bajeti bilioni 7. Ukitanya hesabu ya kawaida unaona kama kuna kilometra saba au nane hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini itoshe kusema kilometra 50 kwa bilioni 7 kwa kweli Waziri hebu tafakari tuone namna gani tunaweza kufanya ili wananchi wa Mlimba waone wanakwenda kupata barabara hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nimeona kwenye hotuba yake tunakwenda kufanyiwa upembuzi yakinifu wa kilometra 220. Barabara hii inaitwa Morogoro – Njombe – Boda yenyeye urefu wa kilometra takriban 220, hilo ni jambo jema na sisi tunataka kusema tu kwamba wana Mlimba wamesikia hakika tunaipongeza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kuhusu upembuzi wa yakinifu wa barabara hii ya kilometra 220 ya Kihansi – Mlimba – Taweta – Madeke. Tangazo la kutafuta mkandarasi mshauri lilifanyika miezi mitatu iliyopita. Kwa hiyo, unavyokuja kuhitimisha bajeti yako jieleze tu ni lini sasa kazi hii ya upembuzi yakinifu inakwenda kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo lingine ni suala zima la reli yetu ya *TAZARA*, ni mdau wa reli ile kwa sababu inapita Jimboni kwangu. Inaunganisha Dar es Salaam mpaka kule kwako Mbeya. Tumekuwa na vituo vidogo vinaitwa *Hot stations* na wananchi wa Mlimba ni wadau wazuri kwa sababu ni biashara na wanakuwa wanasafiri na watu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *hot station* inaitwa Chisano *hot station*, mpaka leo walifunga. Mheshimiwa Waizri, unavyokuja kuhitimsha bajeti, tusaidie ni lini wananchi wangu wa Tisano kata ya Tisano wanakwenda kupata *Hot station* hii ili nishike shilingi yako na nitakusudia kushika shilingi kwa sababu *hot station* ni jambo la kuamua tu na ni biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe *hot station* zote kwenye reli hii ziboreshe kwa sababu wananchi hawa wanaotumia reli hii ya *TAZARA* wakati wa mvua wananyesewa na mvua kwa sababu wanakwenda wanasisimama tu njiani wanasubiri treni. Lakini jua likiwaka, wanawakiwa na jua. Kwa hiyo, kwa sababu ni biashara, kujenga mahusiano mazuri na wadau hawa wa hii reli ya *TAZARA* ni muhimu sasa Wizara muelekeze *TAZARA* wajenge vituo hivi vidogo kuboresha mazingira walau nyakati za mvua waweze kujistiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema tutafakari kwa kina ni namna gani tumegawanya miundombinu ya barabara Kitaifa. Leo hii kuna wenzetu wengine wanajadili barabara za Kata na Kata lakini kuna Watanzania hawafahamu tunavyozungumzia tumejenga barabara za lami Watanzania hawaijui lugha hii. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali, hebu kipaumbele kianze kuunganisha mikoa yetu yote tumalize, twende kwenye wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wenye barabara za kutosha mpeleke fedha za *maintenance*, sisi wengine tujengewe barabara kwa sababu wananchi wa Mlimba hii barabara ya Morogoro – Njombe – Boda ni barabara

ambayo inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Njombe. Nadhani ipewe kipaumbele cha kwanza halafu wengine wafuatie kwa sababu nchi ni moja, walipa kodi ni Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii maeneo mengine sitaki kuyataja, kuna Mbunge mmoja alikuwa anzungumza hapa anajadili barabara kitongoji na kitongoji, jamani nchi hii ni ya kwetu sote! Nchi ya Watanzania wote, wale ambao wameshajengewa barabara wakarabatiwe zile zilizojengwa ndiyo zijengwe mpya, hatuwatendei haki Watanzania wengine. (*Makofi*)

*Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wasiwas wangu kule kwenye Wizara tuwatazame wale wataalam wetu. Nina wasiwas wanatoka mikoa fulani. Kwa hiyo, wanavyoandaa bajeti wanaandaa kwa makusudi ya kuangalia kwao wanakotoka, hii sio sawa sawa. Mheshimiwa Waziri katika hili naomba mkatafakari kwa kina, mchunguze hata kuangalia ukabila kabila kidogo. Samahani sisemi ukabila...[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**NAIBU SPIKA:** Hayo ondoa sasa hivi. Ondoa tu sasa hivi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** ... sizungumzii hiyo, sisemi hiyo...

**NAIBU SPIKA:** Ah! Wewe yafute ili yasiwepo kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niiondoe hiyo. Ninachotaka kusema ni kwamba watafakari kwa kina katika uandaaji wa bajeti tunazingatia vigezo gani? Yamkini kuna mambo fulani ambayo sisi wengine tunaamini ah! Sitaki kuendelea kusema maana nitaharibu huu mchango wangu. Itoshe tu kusema kwamba nashauri Serikali tujikite kwenye vipaumbele hasa barabara zinazouanganisha mikoa na mikoa, twende kwenye wilaya. Tumalize kwanza hizi! Mkoa wa Morogoro unaunganishwa

na Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Morogoro unaungana na Mkoa wa Songea. Tukamilishe kwanza barabara hizi. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, tutamalizia na Mheshimiwa Rashida Shangazi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala. Nami naomba nichangie hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niende moja kwa moja kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika Taifa letu hili la Tanzania. Pia, niende moja kwa moja kuipongeza Serikali kwa kufikiria na kuanza ujenzi wa *standard gauge* kwa maana ya kwamba reli ya kati na kufikiria kujenga bandari kavu katika Kata ya Isaka ambayo matumaini yetu kama wana Msalala ni kuhakikisha ya kwamba bandari hii itakapokamiliika itaenda kukuza uchumi wa Jimbo la Msalala katika kata ya Isaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja kwa kuipongeza Wizara na hasa bandari kwa kutupatia mabati 300ya *CSR* kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo cha afya katika Kata ya Isaka. Ahsanteni sana, kwa niaba ya wana Msalala tunawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja nizungumzie suala la barabara katika Jimbo langu la Msalala. Hali za barabara katika Jimbo langu la Msalala ni mbaya sana. Nimekuwa nikipiga kelele hapa suala la barabara inayotoka Bulyanhulu – Kahama. Barabara hii ni muhimu sana katika uchumi wa Tanzania kwani wote ni mashahidi ya kwamba Serikali yetu inapokea fedha nydingi sana kutoka katika Mgodi ule wa Bulyanhulu lakini barabara hii inahudumia wakazi wengi sana wa Jimbo la Msalala lakini pia wa Mkoa wa jirani wa Geita. Lakini, ndiyo *shortcut*

ambayo mtu anaenda Geita, ni rahisi kwake kupita pale katika Jimbo la Msalala kuelekea maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii kama nilivyosema hapo mwanzoni kwamba kuna fedha imetengwa na nikaomba Wizara ya Ujenzi, Madini na nikamuomba Waziri wa fedha wakae kwa pamoja waone namna gani fedha hizi zinaweza zikatoka kwenda kukamilisha barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hapa kama Wabunge wenzangu walivyochangia kwamba ni ukweli usiopingika kwamba tunaona kabisa kama Mbunge mwenzangu Kunambi amesema kwamba anashangaa ni vigezo gani vinatumika Wizarani katika kugawa fedha hizi. Nimeona hapa barabara hii Geita – Bukoli – Kahama imetengwa kwenye *route* tatu na *route* tatu hizi ukiangalia Geita kwa maana ya kwamba *Bulyanhulu junction road* wametenga kiasi cha shilingi bilioni 1.5 lakini hivyo hivyo *junction road to kahama wametenga bilioni 1.5.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia hapa barabara nyine ambayo inaenda Uyoga – Nyamilangano, barabara ile ile *route* ile ile, wametenga kiasi cha shilingi bilioni 3, usawa uko wapi? Mmetenga kiasi cha shilingi bilioni 6 kwa maana ya kwamba mmetenga *route* tatu. Kwanini *route* ya kwanza mmempa bilioni 1.5, *route* ya pili mmetupa bilioni 1.5, halafu *route* ya tatu mkampa bilioni 3? Basi toeni hiyo bilioni 1 mtugawanyishe huku milioni 500, 500 ili wote twende sawa bilioni 2, 2 Mheshimiwa Waziri, nadhani unanisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri, barabara hii japo ina urefu wa kilometra 160 lakini kilometra zilizotengwa hapa ukiangalia ni jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 6 ambayo ni kilometra 6 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niendelee kuwapongeza na kuwaomba barabara muhimu naona hapa tumetengewa barabara ambayo inatoka Ntobo – Busangi –

Ngaya – Buluma – Jana mpaka Didia mmeitengea kiasi cha shilingi milioni 170 kwa kutengenezwa kiasi cha kilometra 4.8 lakini mmeenda tena mnatutengea kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kilometra 2.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina urefu wa kilometra 85 lakini ukiangalia hapa ni kilometra kama saba ndio mmetutengea hapa. Barabara hii ni muhimu katikauchumi wetu huu wa Jimbo la Msalala. Barabara hii inahudumia Kata ya Ngaya, Kata ya Jana, Kata ya Kashishi na maeneo yote haya ni wazuri wa kuzalisha mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha mpunga, unapozungumzia mpunga asilimia 85 ya mpunga unaopatikana Kahama unatoka katika Jimbo la Msalala kwenye kata hizi. Matumaini yangu ni kwamba barabara hii ikienda kuimarika itainua uchumi wa Jimbo langu la Msalala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, barabara hii muendelee muichukue moja kwa moja. Muimiliki, namaanisha kwamba muiingize kwenye matengenezo ya kila mwaka ili wananchi...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jasson Rweikiza, tutamalizia na Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi kuchangia nami kwenye Wizara hii muhimu na awali ya yote nipende kumshukuru sana Waziri na kumpongeza kwa kazi nzuri na niishukuru Serikali ya CCM ambayo ni sikivu na imekuwa ikifanya kazi kubwa kuwapatia wananchi wake maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Bukoba linaathiriwa na mvua, tuna mvua nyngi sana miezi karibu kumi kwa mwaka. Kwa hiyo, barabara zinakuwa mbovu mara nyngi kutokana na mvua kuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo niendeleze shukrani zangu kwamba Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa kwenye Jimbo langu. Hapa nina barabara kadhaa nitazitaja moja baada ya nyagine taratibu ambazo zinajengwa na zimejengwa huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo mwanzoni barabara ya Kanyinya – Kanazi hadi Ketema ina lami. Niishukuru Serikali ya CCM kwa kazi hiyo kubwa. Barabara kuanzia Katoma – Gera kilometa 8 inajengwa lami na imekaribia kukamilika. Imejengwa, tumefuatilia tumepata lami. Sasa hivi ninavyozungumza pale Kyabalamba katil ya Kata ya Izimbya kulijifunga kutokana na mvua kubwa ambayo nimeisema. Mvua kubwa sana zikawa zimeziba ile njia, magari yakawa hayapiti. Wamejenga *TANROADS*, wamejenga caravat na barabara sasahivi inapitika, ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara kuanzia pale mjini Bukoba kwenda Jimboni kwangu hadi mpaka na Uganda pale Kabango Bay, barabara ya Bugabo inavuka Kata za Nyakato, Bwendaagabo, Kagya, Kishanje hadi Lubafu pale mpakani na Uganda inawekwa lami hivi ninavyozungumza. Ina kilometa 42 lakini kilometa 22 zimeshawekwa lami naishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza barabara moja pale Katokoro ilijifunga kutokana na mvua nyngi ambazo zimezisema. Ilifunga ikawa haipitiki karibu mwaka mzima. Hapa ninapozungumza, juzi mwezi wa nne nimepata shilingi milioni 570 na hapo wapo kazini. Wakandarasi wanajenga njia hiyo ili ndani ya mwezi mmoja barabara hiyo iweze kuitika na kuwa inasaidia zile za jirani pale ambazo zinaizunguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna barabara kubwa inaanzia Chetema inakwenda Kanazi, Ibwera, Katoro hadi Kyakambili, kilometra 60.2. Kama nilivyo sema, iko kwenye llani na sasa hivi tuna shilingi bilioni moja ya kufanya upembuzi yanikifu. Kazi inaendelea na ninaomba barabara hii kasi isipotee, iendelee mpaka mwisho. Upembuzi yakinifu ukamilike na ujenzi uanze. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo ina kilometra 60.2 inahudumia kata 18 kati ya Jimbo zima ambalo lina kata 29. Kwa hiyo, asilimia 62 ya Jimbo linahudumiwa na barabara hii. Naomba kasi isirudi nyuma, tuendelee na barabara hii hii, ijengwe na ikamilike. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya Busimbe – Kyamnene – Maruku hadi Kanyangereko, nayo pia iko kwenye llani. Serikali imeiweka kwenye llani na ninaomba baadaye ujenzi na yenye uanze. Tuna barabara ambayo ilijifunga pia kutokana na mvua nyngi za Bukoba ambazo nimezisema, miezi kumi kwa mwaka. Pale sehemu za Kyaytoke ambayo inaenda eneo la Kibirizi. Iljifunga ikawa haipitiki, leo imetengenzwa, daraja lipo, barabara inapitika vizuri na inakwenda vizuri.

Kwa hiyo, naomba shukrani hizi ziifikie CCM lakini kazi iendelee na tusirudi nyuma, tuongeze mkazo barabara hizi ziweze kupidika muda wote pamoja na mvua kuwa ni kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naona Mheshimiwa Conchester Rwamlaza alikuwa anafurahi hapo. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru dada yangu Jacqueline Msongozi kwa kunitunuku cheo ambacho amekitamka muda si mrefu hapa Bungeni. Nami naahidi nitatenda mema kulingana na ukubwa wa cheo alichonipatia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo ndiyo imekipatia chama hiki ushindi ukurasa wa 177 tunayo barabara yetu ambayo imewekwa pale kwa ajili ya upembusi yakinifu na usanifu wa kina kilometra 278 kutoka Same – Mkomazi – Umba Junction ambapo unaipata Tarafa ya Umba kwa Kata za Lunguza, Mng'aro na Mnazi kwenda Mabokweni kwa ndugu Kitandula, kufika Maramba kuunganisha na barabara inayokwenda Horohoro kwenda Mombasa na kurudi Tanga Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Nailbu Spika, barabara hii ni muhimu sana na ni barabara ya kimkakati. Kwanza iko pembezoni mwa mpaka wa Tanzania na nchi jirani ya Kenya. Lakini pia iko pembezoni kabisa inazunguka hifadhi ya Taifa Mkomazi. Na huku ndiko kule kwenye mazalia pekee ya vifaru ambao tunawatumia katika Taifa letu hili kama kielelezo mionganoni mwa vielelezo vya urithi wa Kitaifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamuomba sana Waziri mwenye dhamana kwamba wakati tunajadili barabara hii huko nyuma ulikuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara unayoiongoza sasa. Sasa unakwenda kusimamia Sera na Chama Cha Mapinduzi kitakuja kukuuliza ni kwa namna gani umezitekeleza sera zinazotokana na Ilani ya Chama chake. Kwa hiyo, tuanomba uweke msisitizo sana katika hili eneo la upembusi na usanifu wa kina ufanyike kwa haraka ili tangawizi kutoka Mambamlyamba, tangawizi kutoka Mbaramo, na Mnazi ziweze kwenda kwenye masoko ya Mombasa na Tanga Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mombo – Lushoto kilometra 36 na wewe umeipita lakini ninafaharika pia kusema kwamba na Mheshimiwa Rais wa Awamu hii ya Sita amepita katika barabara hii alivyokuja Mlalo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, barabara hii ni nyembamba mno na sasa hivi Wilaya ya Lushoto imekuwa na magari mengi sana ya usafirishaji wa mboga mboga na matunda lakini pia na mabasi. Kwa hiyo, barabara hii magari lazima yapishane kwa kusimama kwenye makona ili anayeshuka na anayepanda aweze kupishana vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa, tumeshazungumza mara nyingi kwenye vikao vyetu vya RCC na tunavyopitisha bajeti katika RCC, tunavyopeleka Serikali Kuu, *Engineer Mfugale* mara zote alikuwa anaziondoa hizi bajeti zetu. Tunaomba sasa zisimamiwe. Barabara hii ni barabara muhimu sana. Watanzania wanajua kwamba ukiondoa Ikulu ya Dar es Salaam kabla ya hii tulijojenga Chamwino juzi, Ikulu kubwa nyingine tangu wakati wa mkoloni wa Kijerumani ni ile illyoko Lushoto. Kwa hiyo, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu hapa ndipo penye Ikulu kubwa ukiondoa Dar es Saalm kabla ya hii ya Chamwino. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Lushoto – Magamba – Mlalo kilometra 33. Hii imekuwa na ahadi nyakati zote lakini pia ikiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu hii ya Sita aliviyokuja Mlalo alituahidi kwamba barabara hii tutahakikisha kwamba inajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wameshaanza lakini walikuwa wanafanya awamu ya kilometra tano, tano. Mwaka jana yalitokea mafuriko ambapo Naibu Waziri mwenye dhamana hiyo ambaye sasa hivi ni Waziri wa Ulinzi Mheshimiwa Kwandikwa alikuja pale na akaahidi kwamba Mwaka huu wa Fedha angalau ataijenga kwa kiwango cha kilometra 10. Ninaomba sana kwamba bajeti hii kabla haijapita lazima eneo hili mliangalie kwa kina. Tunapozungumza mazao yanayolimwa Lushoto ni mazao yanayoharibika kwa wepesi. Viazi, karoti, matunda na mboga mboga. Hivi viazi ambavyo vinafanya wale wa mjini wanaitwa ‘*baby*’ japo ni wazee wazima vinatoka Lushoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo. *Engineer* tunakuomba sana kwamba uende ukatenge hii fedha kama ambavyo ilikuwa ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Tano lakini kazi inaendelea. Tunaamini kabisa kwamba Serikali ya Awamu ya Sita itatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha uchangiaji. Tutaendelea na wachangiaji waliobaki mchana. Tutakuwa na wachangiaji wafuatao kwa hiyo, wajitayarische. Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, Mheshimiwa Omary Kigua, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mheshimiwa Vincent Paulo Mbogo, Mheshimiwa Kennel Nolo, Mheshimiwa Aloyce Kamamba, Mheshimiwa Stella Fiyao na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyokwenda.

Baada ya kusema hivyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni.

(*Saa 07.08 Mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

(*Majadiliano Yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano na tutaanza na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, atafuatiwa

na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze na Mheshimiwa Omari Kigua ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Miundombinu. Kwanza kabisa, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri na Manaibu wake wawili kwa uchapakazi wao mzuri wa kuhakikisha kwamba barabara zetu zinaunganika karibia Tanzania nzima. Hongereni sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda naomba niingie sasa kwenye hoja zangu za msingi. Hoja yangu ya kwanza ni kwamba pamoja na kazi nzuri ambayo Serikali inafanya kwenye miundombinu lakini kuna changamoto ya wakandarasi. Wakandarasi wanalalamika sana wanapokuwa wamefanya kazi wanacheleweshewa sana malipo yao lakini pia wakifanya kazi kabla hata hawajalipwa wanakatwa pesa zao kwenye akaunti zao na kufungiwa bila utaratibu. Kwa kweli hilo Wizara iliangalie kwa makini na ilifanyie kazi. Wakandarasi wetu ni wazalendo na ni Watanzania na wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba barabara zetu ni nzuri pamoja na changamoto ya mvua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Rukwa, Sumbawanga Mjini. Uwanja huu wa ndege umezungumziwa muda mrefu sana, zaidi ya miaka minne tunapitisha bajeti ya Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga lakini hakuna kinachoendelea. Tunaishukuru Serikali mwaka juzi iliweza kuwalipa wananchi waliokuwa wanauzunguka uwanja ule wa zamani mdogo lakini baada ya hapo kumekuwa kimya kabisa, hakuna kinachoendelea na wakati Mkoa wa Rukwa una fursa nyingi ikiwemo na utalii wa aina mbalimbali; *Kalambo Falls*, mbuga za wanyama na madini ya kutosha. Pia kuna wafanyabisahara wakubwa

ambao wangeweza kutumia usafiri wa ndege kuja Dar-es-Salaam na kurudi Dodoma na kwenda Sumbawanga. Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hapo atueleze Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini utajengwa lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni barabara. Kuna barabara moja ambayo ni uchumi kabisa wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Songwe na Mbeya. Barabara hiyo inatoka Kibaoni – Maji Moto - Muze - Iremba – Kilyamatundu - Mloo. Barabara hii nayo imezungumziwa muda mrefu sana, Serikali imekuwa ikitengeneza vipande, utakuta imetengenezwa daraja baada ya muda linaacha mto Serikali inarudi tena kutengeneza. Nachoweza kuishauri Serikali, barabara hii muarobaini wake ni kuweka lami. Barabara hii imepita kwenye Bonde la Rukwa ambapo mazao mengi yanalinwa kule. Mpunga, ufuta na mazao ya kila aina yanastawi kwenye Bonde hilo la Rukwa. Kwa hiyo, tunaiomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda niongelee tena suala la bandari. Mkoa wa Rukwa tumekuwa na bandari kama tatu lakini hazifanyi kazi yoyote. Serikali imewekeza pesa za kutosha kwenye bandari hizo lakini mpaka sasa hivi hakuna bandari hata moja inayofanya kazi. Kwa maana hiyo, naishauri Serikali iweke nguvu kwenye bandari hizi ikiwemo Bandari ya Kipili na Bandari ya Kabwe; bandari zile Serikali imeweke pesa nyingi kwa hiyo, irudi kwenda kuzifanyia kazi ziweze kufanya kazi na kuingiza pato la Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya mafupi, naomba Serikali iwakumbuke wakandarasi kwa kuwalipa pesa zao kwa wakati. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi ajiandae.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu, Wizara ya Miundombinu. Naomba nilete masikitiko yangu kwa barabara kubwa hii ambayo inatoka Tabora kwenda Kigoma. Kwanza, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze na kumshukuru Rais wa Awamu ya Nne, ndiye aliyetuunganisha na mikoa mingine sisi Kigoma pale alipotutengenezea Daraja la Mto Malagarasi na likaitwa Kikwete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipo kipande kilibaki cha kilometra 51 ambacho kinatokea Mpeta baada ya kuvuka Daraja la Mheshimiwa Kikwete mpaka Uvinza ni kilometra 51, hili eneo limekuwa ni tatizo kwa muda mrefu sana. Unatoka Dar-es-Salaam, Dodoma, Tabora, unakwenda mpaka Kigoma lakini eneo hilo ndilo limebaki na vumbi, ni jambo la ajabu sana. Wananchi wanajuliza hivi kuna nini? Kwa hiyo, naomba Waziri pamoja na kwamba nimeona kwenye bajeti yake ameitaja, lakini naomba nisisitize na wananchi wasikie kwamba barabara hiyo nimeitaja, ni kero kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ipo barabara nyingine ya Uvinza kwenda Kasulu nayo ni kero sana na ni barabara fupi sana. Kwa kweli, naomba katika bajeti hii hii barabara nayo iweze kuangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ipo nyingine inatoka Uvinza kwenda Mpanda kupita Mishamo. Hii nayo ni barabara ambayo kwa kweli ni ya kimkakati, ikiwekwa lami na sisi Kigoma tutakuwa tumeondokana na lawama na malalamiko kama ya wale wenzetu waliokuwa wanasema wametengwa. Sisi tumetengwa kwa sababu tumetengenezewa barabara za lami lakini vipande vimebaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Kigoma Kusini, wewe ni shahidi, ulipokuwa ukitokea kwenye msiba wa marehemu Mbunge wetu ambaye alitangulia mbele ya haki, Mheshimiwa Nditiye, wakati unarudi kutoka

Kigoma kwenda Mbeya ulipotea. Ulichukua barabara ambayo sio yenewe, ile barabara ni ya Simbo – Kalya, ulikwenda kurudia kwenye kivuko cha pale kwenye Mto Malagarasi, pale ndiyo uliposhtuka kwamba barabara ile sio yenewe, nakupa pole sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuja kuambiwa kwamba Naibu Spika alipotea alidhani hii barabara inakwenda Mbeya. Ukweli barabara ile kama itajengwa vizuri inayo access ya kwenda Mbeya, ulikuwa hujakosea, sema kule mbele ungepata shida sana. Barabara ambayo ungepita badaye ni kutoka Rukoma kwenda Ikuburu na Rubalisi baadaye inapita Mwese halafu ndio ungeingia sasa Mpanda kwenda sasa Kalya. Hii barabara ni muhimu sana kwa sababu ni barabara ya mkoa lakini inakwenda kuishia Kalya peke yake. Ni barabara nzuri bado tunatumia changarawe na kwa kweli kupitia nafasi hii nimpongeze Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Kigoma Bwana Eng. Choma, hii barabara anaingalia sana lakini bado kuna vipande ambavyo vina shida.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema tu kwamba Daraja la Mto Malagarasi pale ulipokwamia ni tatizo, lakini nashukuru Wizara imetenga shillingi milioni 250 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Nina imani daraja hilo litaenda kujengwa. Naomba niunge mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri kweli nilipotea, halafu hizo ni kilometra kama 110 hivi kwa hiyo, siyo masihara. Nilipotea nikawaza hawa watu wa Kigoma badala ya kunikarimu wanani poteza tena. (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo ajiandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi iliyopo mbele yetu. Mimi nitajikita kwenye eneo moja tu nalo ni barabara ambayo inaunganisha mikoa minne ya Tanga, Manyara, Dodoma na Singida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi upo toka Bunge la Kumi na Moja, kila nikisimama hapa hoja yangu ilikuwa ni moja tu kuizungumzia barabara hii. Cha kushangaza Mheshimiwa Waziri kwa makusudi kabisa ameamua kutenga shilingi bilioni 3 mwaka huu ambayo haiwezi kutosha hata kujenga kilometra tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii mwaka wa Bunge liliopita au mwaka huu wa fedha tulio nao zilikuwa zimetengwa shilingi bilioni 6 za kitanzania, lakini leo hii nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu barabara hii hajatangazwa kwa maana bado mwezi mmoja, kwa hiyo, matarajio ya barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami yanazidi kupotea. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri aniambie barabara hii inatangazwa lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini naizungumzia barabara hii? Ni kwa sababu ni barabara ambayo Wabunge takribani sita wamezungumzia; Mbunge wa Singida Kaskazini, Mashariki, Chemba (Dodoma), Kiteto, halikadhalika Mbunge wa Handeni na mimi wa Kilindi tumezungumzia barabara hii. Kwa nini Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu wa barabara hii? Haoni kwamba Watanzania wa kwenye maeneo haya wanahitaji na wao kuwa na afya ya maendeleo ya barabara ya kiwango cha lami? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ndipo bomba la mafuta ambalo nchi ya Tanzania na Uganda linaenda kupita ambapo Mheshimiwa Rais anakwenda kusaini mkataba keshokutwa. Wenzetu wa Uganda tayari

miundombinu iko vizuri, sisi wa eneo hili la Tanzania ambapo sehemu kubwa barabara hii inapita hajijengwa kwa kiwango cha lami. Tunataka kuwaambia nini wenzetu ambao wameamua kuitisha bomba hili la mafuta kwenye nchi ya Tanzania? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, ni mgeni kwenye Wizara hii lakini naamini watendaji wake wanafahamu umuhimu wa barabara hii. Hata Mpango wa Maendeleo ulioishia mwaka jana umeitaja barabara hii kwamba ina umuhimu sana kwa ajili ya uchumi wa nchi hii, kwa nini Mheshimiwa Waziri ametuwekea hela ndogo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huwa sipendi kuzungumza kwa hali ya kukasirika lakini kwenye hili Mheshimiwa Waziri amenikwaza. Ni lazima niseme Wanakilindi, Dodoma, Singida wanahitaji barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami. Tunazungumzia kudumaa kwa uchumi, leo unapokuwa huna barabara ya kiwango cha lami; barabara ambayo haipitiki maana yake uchumi wa wananchi wa maeneo hayo unadumaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ndilo ambalo linasafirisha kwa kiwango kikubwa mazao kwenda Kenya, Kilimanjaro, Arusha, yote yanapita kwenye njia hii. Sasa iweje Mheshimiwa Waziri usitenge fedha ili barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami? Sitegemeli kushika shilingi lakini naomba unipe maelezo ya kutosha ni lini ataitangaza barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyininge ambayo napenda kuizungumzia ni ya kanzia Songe - Gairo ambayo Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Gairo ameizungumzia jana. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba mwaka juzi ilitokea Daraja la Kiyegeya lilitatika wiki nzima magari yanayoenda Rwanda, Burundi yalikuwa hayapiti. Njia ilio rahisi ambayo inaweza kuwa ni suluhu wakati barabara hii ikiwa imepata tatizo ni njia hii ya kutoka hapa Dodoma - Kilindi - Tanga ni takribani kilometra mia tatu na zaidi. Barabara hii

itasadia kwa sababu tunatarajia kujenga Bandari ya Tanga, ili bandari hiyo iweze kuwa na faida ni lazima tujenge barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo na Mheshimiwa Kenneth Nollo ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kushukuru na kuwapongeza sana Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya. Niwapongeze sana kwa mara ya kwanza kabisa barabara yetu ya kutoka Nata – Mugumu sasa imeingizwa katika ujenzi kwa kiwango cha lami, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunawashukuru kwa ajili ya kuonesha mpango wa kuanza kujenga barabara ya lami kutokea Tarime kuja Mugumu. Vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza *TANROADSM*ko wa Mara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha barabara zetu zinapitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuiomba sana Wizara ya Ujenzi kutoa kipaumbele na *commitment* ya kutosha katika barabara ya Makutano – Nata - Mugumu. Barabara hii ni ya muda mrefu sana, imeanza kulimwa toka mwaka 2013 tayari kulipelekwa pale makampuni ambayo ilikuwa ni *joint venture* ya makampuni kumi. Ujenzi wake umeanza lakini umeendelea kusuasua sana, sasa hivi ni takribani miaka kumi barabara ile haikamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hata pesa ambazo zimekuwa zikiendelea kutolewa bado haituridhishi kama kuna *commitment* ya kutosha, hakuna *priority* katika barabara ile. Ukiangalia mwaka 2014/2015 kulitengwa shilingi bilioni 5.6 tu, 2015/2016 kukatengwa shilingi bilioni 2.2, mwaka

2016/2017 kukatengwa shilingi bilioni 12, mwaka 2017/2018 shilingi bilioni 9 na ukiendelea bado bajeti ile imeendelea kupungua kutoka shilingi bilioni 12 mpaka bajeti ya mwaka huu 2021/2022 kumetengwa shilingi bilioni sita tu, barabara ya kilometra 125.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ikumbuke barabara hii ya Makutano – Nata – Mugumu ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha. Barabara hii kwa mujibu wa Mpango na Dira ya Maendeleo ya nchi yetu tulikuwa tumejiwekea kwamba lazima kipaumbele kitolewe kuunganisha barabara zote za mikoa. Sasa barabara hii ya kuunganisha Mkoa wa Mara pamoja na Mkoa wa Arusha bado haijajengwa lakini barabara za mikoa mingine tayari wamejenga. Tunaomba sana Wizara iongeze *commitment* kubwa ya fedha katika barabara hii ili kuhakikisha kwamba sasa inakamilika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kuna mkandarasi yuko pale sasa hivi lakini kuna shida ya menejimenti. Mimi nimewatemebelea mwezi huu wa tano mwanzoni, pesa imetolewa tofauti na sehemu zingine pale watu wale bado hawajaanza kupambana kuhakikisha kwamba wanajenga barabara ile. Niombe sana Wizara muweze kupita pale na kusimamia mradi ule kwa karibu sana ili uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile wameanza kuilima lakini bado fidia hajatolewa. Niombe sana Wizara iende kuhakikisha kwamba fidia zinatolewa na watu wale wanaweza kupata nafasi tena ya kuchukua maeneo mengine wafanye kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Uwanja wa Ndege wa Serengeti sasa uingizwe katika upembuzi yakinifu. Pia naomba Wizara hii, kuna barabara ambazo zinapaswa kufanyiwa *review* tena ziingiwe katika barabara za *TANROADS*; tayari Wabunge wengi wamelalamika kwamba fedha haitosheleza katika *TARURA*, sasa ni vema tupeleke barabara nyingine zinazoweza kufaa kutohana na umuhimu wake katika uchumi, ziingizwe katika barabara za *TANROADS*.

Katika Jimbo langu, barabara ya Mesaga – Masinki; barabara ya Mugumu - Mbalibali mpaka Machocho mpaka Nyansurura ni muhimu sasa zilingie kuwa barabara za *TANROADS*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba barabara inayotoka Musoma kwenda makutano ya Nyakanga mpaka Rung'abure, ujenzi wake wa lami unasuasua. Mheshimiwa Waziri tunashindwa kuelewa kuna mpango gani pale? Mbona barabara ile inajengwa kidogo kidogo sana na barabara ile inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti pamoja na Mji wa Musoma ambao ni Makao Makuu ya Mkoa? Tunaomba barabara ile iongezewe fedha ili ikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba kuwepo na msukumo mkubwa wa ujenzi wa barabara hizi. Pia namwomba sana Waziri pamoja na Wizara yote kwa ujumla, waangalie sasa uwezekano wa kuzifanyia upembuzi yakinifu barabara mpya ambazo zina umuhimu mkubwa sana kiuchumi ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara inayotoka Nyansurura ikipita Majimoto mpaka Iramba mpaka Sorisimba ni muhimu sasa ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Nollo na Mheshimiwa Aloyce Kamamba, ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kuwapa pongezi Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi hii yapo majimbo yaliyokatwa kutoka Majimbo mengine kutokana na ukubwa wa eneo pamoja na Mikoa. Hii Mikoa ambayo ni michanga inatakiwa hii Wizara ya Uchukuzi iwaone kwa jicho la kipekee kwa sababu miundombinu bado. Ille mikoa

ambayo ni mama ikagawiwa ikatoa Majimbo mapya ambayo bado machanga, inatakiwa hii Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ifanye tathmini, iende ikaangalie barabara ambazo ni *main road* za Majimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *TARURA* au *TANROADS* imebaki kwenye yale Majimbo mama. Ukichukua sisi watu wa Rukwa, Songwe, Kigoma Nyanda za Juu Kusini, Mtwara, Lindi, Wizara ya Uchukuzi inatakiwa ikae chini iangalie hii Mikoa ambayo kidogo ilikuwa imesahaulika. Nirudi kwenye Jimbo langu; Jimbo langu limekatwa kutoka Jimbo la Nkasi Kaskazini. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini. Ukiangalia Jimbo la Nkasi Kusini halina barabara ya *TANROADS* ina kilometra sita tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kata nne ambazo toka mwezi wa 11 mvua imeanza, sasa hivi ni miezi sita au saba, wala magari hakuna, hakupitiki barabara zina miaka karibu 10, 20, sasa unakuta barabara huku wametenga *maintenance*; tena barabara ile ya *TANROADS* kupitia hiyo *maintenance* wanatengeneza barabara ambayo tayari inapitika. Sisi kule ni lami, hiyo hiyo moram ni lami wakati kuna barabara huko kata nydingine hazipitiki, magari hayaendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni wananchi, *TANROADS* na *TARURA* wote wanahudumia wananchi. Kwa hiyo, wanatupa wakati mgumu sisi majimbo ambayo yapo pembezoni. Mfano Jimbo la Nkasi Kusini, kuna bandari mbili Wilaya ya Nkasi ambazo zimejengwa kwa fedha nydingi sana za Serikali, lakini miundombinu ya barabara ambazo zinakwenda kwenye bandari hiyo hakuna. Barabara ya kutoka Paramawe kwenda kwenye bandari ya Kipili na barabara ya Kabwe ziwekwe lami ili kuweza kuinua uchumi wa mwambazo mwa Ziwa Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara ya Ninde – Wampembe; Wampembe ni *main feeder road*. Wanasesma *feeder roads* hazikidhi vigezo, lakini kila Jimbo lina barabara zake. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inatakiwa iwasiliane na

sisi Wabunge tunaowakilisha Majimbo tuwaambie barabara zipo ziingizwe *TANROADS*? Kwa sababu mwanzo ilikuwa ni mfumo, kuunganisha Mkoa na Mkoa, tayari Mikoa mingine imeshaunganishwa. Sasa tuje kwenye barabara za vijijini. *TANROADS* hata ikiweka barabara za lami, hizi barabara za vijijini ambako ndiko mazao yanazalishwa, hivi barabara za *TANROADS* itabeba nini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za vijijini ndiyo viwanda ambako mazao yanazalishwa. Huko barabara ziboreshwé, zikishaboreshwá, hizi *main roads* ndiyo zitakuwa zina umuhimu zaidi. Kwa sababu tunatengeneza barabara ya lami, lakini mazao hayafigi, ni kazi bure. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika mji wangu mdogo wa Kijiji cha Chala *TANROADS* barabara imepita wamebomolewa nyumba miaka 10 sasa wale wazee hawajapata fidia. Piga mahesabu, mtu wa kijijini amebomolewa nyumba yake ambayo alikuwa anategemea kupata fidia, hajapata fidia na wale wengi ni wazee.

Naomba Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, njoo ni katika Wilaya ya Nkasi katika Kijiji cha Chala mje mtoe tamko la kuwapa fidia wale watu waliobomolewa nyumba zao. Wengi wanalamika, wengine wamesha-*paralyze*, maisha ni magumu. Yote haya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi nawaomba njoo ni muwape fidia wale watu, muwalipe haki zao, wanalamika. Sisi Wabunge tunapata shida, tunawajibia nyie majibu ya Wizara ya Ujenzi wakati haupo Wizara ya Ujenzi, inabidi ujibu tu kwa niaba ya Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, hizi kata tatu ambazo toka mwezi wa 11 magari hayaendi, naomba kwa namna ya pekee Wizara jie ijenge zile barabara. Sasa hivi namkabidhi hizi barabara ziingizwe *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, mhudumu aje amkabidhi barabara Waziri wa Ujenzi.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kamamba na Mheshimiwa Dennis Londo, ajiandae.

**MHE. KENETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Nilitaka nichangie katika maeneo mawili. Kwanza nichangie kuhusu bandari yetu ya Dar es Salaam na vile vile nitachangia kuhusu suala zima la barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari yetu ya Dar es Salaam ni bandari inayohudumia nchi sita katika ukanda wetu huu, lakini bandari yetu hii imekuwa na changamoto nydingi kwa maana ya *efficiency* ya vitu vinavyokuja kuweza kutoka sasa kwenda kwenye nchi wanazotegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Benki ya Dunia, inasema nchi majirani wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam, kwa ujumla wanapata hasara ya dola milioni 830 *collectively* kutokana na; niite ni uzembe unaotoka kwenye bandari yetu, kwa maana ya kuchelewa kwa muda wa vitu kutoka na hata urasimu usio wa lazima pamoja na udkozini unaofanyika bandarini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *World Bank* wanasema bandari yetu ukilinganisha na bandari washindani katika ukanda wetu, ya kwetu inaonekana iko *expensive* kwa vigezo vyote hivyo. Vile vile wanasema Tanzania ikiamua kusimamia bandari yake, inaweza kuondoa *loss* ya shilingi *almost* bilioni 175 ambayo ni *total loss* kwenye *economy* pamoja na *loss* ya *revenue* tunazozikosa kwenye bandari yetu. Kwa hiyo, ninachotaka kusema kwa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ipo haja kubwa sana ya kusimamia bandari yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia, sijui kuna kigugumizi cha nini? Tumeona nchi kama *Singapore* wanatumia bandari na viwanja vya ndege, wameendelea, sisi tunataka tupate miujiza ya aina gani? Pamekuwa na mizengwe mikubwa sana kwenye bandari yetu. Kwa hiyo, nataka Wizara hii na Mheshimiwa Waziri anasikiam hebu wakijite kwa ajili ya kuiboresha bandari yetu kwa kuondoa tu urasimu ambavyo ni vitu vya kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la barabara, Wizara hii imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kutumia *agency* ya *TANROADS*, lakini hawapati fedha ya kutosha. Kwa miaka mitano mfululizo, bajeti hii hajaongezeka, lakini kazi walioifanya ni kubwa. Sasa tunategemea miujiza gani kama chombo hiki kinachotusa idia kwa kuunganisha nchi yetu katika barabara, lakini bado wanapata fedha kidogo? Kwa hiyo, hili tulialangalie, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iongezewe fedha za kutosha na hata bajeti yenye basi iweze kutekelezwa kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, alipokuwa kwenye kampeni pale Manyoni, aliahidi kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami kutoka Manyoni kuja Itigi - Heka - Sanza - Chali kwenye Jimbo langu la Bahi Kijiji cha Chali; na barabara hii ni muhimu sana, maana yake ukija Halmashauri ya Manyoni na Bahi, tunaitegemea sana kwa maana ya shughuli za kiuchumi katika Mji huu wa Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, barabara hii ikitengenezwa kwa kiwango cha lami kama nilivyotaja, kuanzia Manyoni - Itigi - Heka kuja - Chali Igongo - Chali Makulu - Chali Isanga, unakuja unatokezea Chipanga unakuja Mpalanga – Bihawana, utakuwa umetengeneza *link* kubwa sana ambayo itachochea uchumi katika Mkoa wa Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi barabara zimeonyeshwa, lakini kuna vitu vingine ambavyo ukiangalia huwezi ukaelewa.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KENETH E. NOLLO:** Naunga Mkono hoja Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Londo na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Uchukuzi. Moja, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi, lakini kwa nafasi hii kwanza nikutaarifu kwamba Mkoa wetu wa Kigoma ndiyo pekee katika Mikoa yote 26 ambao haujaunganishwa kwa kiwango cha lami. Nitaarifu kwamba barabara ni uchumi na barabara ni maendeleo. Kutokuwa na barabara maana yake mazao yanayozalishwa katika Mkoa wa Kigoma hayana uwezekano wa kupelekwa kwenye soko. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujaunganishwa Tabora kwenda Kigoma, hatujaunganishwa Mpanda kwenda Kigoma, lakini hatujaunganishwa Kagera kwenda Kigoma. Kwa nafasi hii tu nishukuru kwamba kuna makataba umesainiwa wa ujenzi wa barabara ya Kakonko – Kibondo – Kasulu hadi Buhigwe, lakini ujenzi wake unakwenda taratibu sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hebu fika uangalie ujenzi unavyoendelea sasa. Nimetoka kule kwa shughuli ya kampeni, naona kama vifaa viro, lakini ujenzi sasa ni mwaka mmoja na nusu, kama unawenza kuhesabu ni kama kilometra 10 tu basi. Sasa naomba atakapokuwa anawasilisha taarifa yake ya mwisho lini barabara hii itakamilika? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo barabara katika Jimbo langu inaanzia Kakonko kwenda Kinonko kwenda Bwarama - Kabale hadi Muhange. Inapofika kwenye mpaka wa Muhange, pale kuna soko kubwa limejengwa zaidi ya shilingi milioni 583 ziko pale, lakini soko lile halifanyi kazi kwa sababu hatuna barabara. Naomba sana na bahati nzuri Mheshimiwa

Rais Hayati Dkt. Magufuli aliahidi ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni kilometra 40, ili kuhakikisha kwamba shughuli zinafanyika, naomba atakapokuwa anawasilisha taarifa yake, lini barabara hiyo sasa itajengwa ili iunganishe nguvu ya huku kwenye Makao Makuu ya Wilaya hadi pale kwenye mpaka wa Muhange?

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wananchi ambao barabara hii inapo jengwa katika Vijiji vya Kasanda - Kaziramihunda hadi Kabingo, hawa hawajapewa fidia kwa majengo yao. Naomba nayo atakapokuwa analeta taarifa yake ya mwisho tujue wananchi hawa watalipwa fedha zao lini? Zipo fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Ukurasa 321, Mkoa wa Kigoma katika mikoa yote, haijapangiwa kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakwenda sambamba na ukurasa 335 mpaka 336, fedha za matengenezo ya muda maalum kwa ajili ya barabara, Mkoa wa Kigoma nao kwenye eneo hilo haikupangiwa. Sijajua, kwa nini Mkoa wa Kigoma kama Mikoa mingine ilivyopangiwa haujaweza kupangiwa fedha? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo bandari; pale Bandari ya Kigoma ya Kigoma kuna Meli ya Liemba, ina zaidi ya miaka 100. Wakati Mikoa mingine au kwenye bandari nyingine wanunua meli mpya. Kigoma wanasema kwamba wanakarabati ile ya zaidi ya miaka 100, kwa nini tusinunuliwe na sisi meli mpya, kama wanavyofanya kwenye bandari nyingine? Kwa hiyo, naomba sana Serikali ili langalie hili na sisi katika bandari ya Kigoma tuweze kupata meli mpya kama inavyofanyika kwenye Ziwa Victora kama inavyofanyika kwenye ziwa Nyasa na maeneo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uwanja wa ndege. Kigoma ipo jirani na Kongo, Kigoma ipo jirani na Rwanda, Kigoma ipo jirani na Burundi, lakini kuitia Ziwa Tanganyika kuna muunganisho kwenda Zambia. Naomba uwanja uweze kujengwa, uimarishwe kwa ajili ya kuhakikisha kwamba

wananchi wetu wa Mkoa wa Kigoma wanapata usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dennis Londo atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa John Constantine Kanyasu, ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Bajeti ya Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa hilli kwa sababu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ndiyo roho ya kile ambacho tunaita mapinduzi ya nne ya viwanda ama uchumi wa kati ama uchumi wa viwanda. Hatuwezi kuzungumzia uchumi wa viwanda bila kuzungumzia miundombinu hasa ya barabara ambazo zinapitika mwaka mzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya nchi yetu bado barabara ni changamoto. Ni muhimu wakati tunajadili bajeti ya Wizara hii, kuangalia ni jinsi gani Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inakuwa na mafungamano ya karibu sana na Wizara zote ambazo tunazitegemea katika *ku-transform* uchumi wetu hasa Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Afya, Uvuvi na Mifugo; hizi zote zinategemea sana mipango ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ili ipange mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na dhana nyininge ya kuwa na mafungamano ya karibu na Idara nyininge ama Wizara nyininge, zina umuhimu sana wa kuangalia ni jinsi gani inaenda kuunganisha wananchi wa Tanzania hasa wanaoishi katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna kasi ambayo inaendelea katika ujenzi wa *standard gauge*. Pembeni ya *standard gauge* kuna barabara ambayo inahudumia ujenzi wa reli hizi ambazo imeunganisha vijiji vingi sana katika nchi yetu. Barabara hizi sasa hivi ukipita zimesahaulika, ni barabara ambazo zinaokoa maisha ya watu, lakini zinakuza uchumi sana katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, ni muhimu Wizara hii ikaziangalia barabara hizi kwa jicho la pekee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kule Wilaya ya Kilosa kila mwaka tunakuwa na mafuriko. Kuna mabwawa yanaitwa mabwawa ya punguza, mabwawa haya yalitengenezwa enzi ya Mjerumani na miaka yote yalikuwa chini ya Shirika la Reli, tangu yamepelekwa katika Wizara ya Kilimo yamejaa na maji ya Mto Mkondoa yanashindwa kuwa na mahali pa kufikia, matokeo yake yanasaababisha maafa kwa wananchi wetu siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia dhana ya mafungamano kati ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi hapa ndipo ninapoanzia. Kuna umuhimu wa Wizara hii kukaan na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji kuona ni jinsi gani maji ya mito kama haya ambayo yanachukua reli kila siku, reli ya kati kule Godegode inabebwa kila siku kutokana na mafuriko ya mto huu. Ni lini Wizara hii itakaa pamoja na Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo kuona kwamba maji haya badala ya kuwa dhabama na balaa kwa reli yetu ambayo ni miundombinu tunayotegemea inakuwa baraka kwa kutengeneza mabwawa ambayo yanaenda kuhifadhi maji, hivyo kuepusha vifo vya wananchi katika Wilaya ya Kilosa na maeneo ya Jimbo la Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati Waziri anahitimisha hoja atuelezee Wizara yake imejpanga vipi kuhakikisha kwamba inazungumza na Wizara nyininge kuhakikisha mabwawa haya ambayo yalikuwa chini ya Shirika la Reli yanarudi huko na yanatunzwa na kuangalia ni jinsi gani maji yake yanaenda kuzuiwa yasiletie athari kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusiana na suala zima la uwezeshaji wa wakandarasi wetu wazawa. Kuna miradi mingi mikubwa ambayo tunaigharamia kama *Standard Gauge*, lakini kuna bwawa la Mwalimu Nyerere na miradi mingine mikubwa ya barabara. Ni kwa jinsi gani miradi hii tunaitumia kama fursa ya kuwafundisha vijana wetu kuiba teknolojia ama kutumia teknolojia ambayo wenzetu wanaitumia katika ujenzi huu kama sehemu ya masomo ama mafunzo kwa vijana wetu wa ndani. Hii itasaidia miradi hii inapokamilika, basi vijana wetu wanatoka na ujuzi ama wanatuachia ujuzi ambao kesho hautatulazimisha kuagiza ama kuwapa *tender* makampuni ya nje kwa kisingizio kwamba wakandarasi wetu hawana ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jitihada za makusudi ambazo Wizara ya Ujenzi inafanya katika kuwawezesha wakandarasi wetu wazawa. Pale Kilosa kuna Barabara ya Kilosa - Mikumi ambayo Kampuni ya Umoja ambayo ni ya wazawa wamepewa kama sehemu ya majaribio ama sehemu ya kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Tabora kuna Barabara ya Kaliua - Urambo ambayo wamepewa wakandarasi wazawa. Pamoja na kuwawezesha wakandarasi hawa wazawa, bado mradi huu ambao tunauona ulikuwa ni sehemu nzuri ya wao kujifunza unakwazwa na nia njema ya baadhi ya watu. Pamoja na kwamba nia ni kujenga barabara hii, lakini vijana hawa unaweza kuona kwamba wanashindwa kutekeleza mradi wao kwa wakati kwa sababu ya *GN*, fedha haziji kwa wakati, malipo yao hayaji kwa wakati na hivyo kupelekea faida ndogo ambayo ingeweza kutumika kwa wao kuongeza uwezo wa kudai miradi mingine unapotea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafatiwa na Mheshimiwa John Constantine Kanyasu naMheshimiwa Michael Mwakamo ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwa sababu dakika tano ni chache, napenda niseme yaliyomo ndani ya moyo wangu, bajeti hii haikugusa kabisa maeneo ya Nyang'hwale hata sehemu moja. Kuna ahadi za Viongozi Wakuu kuanzia Mheshimiwa Rais Kikwete alikuja 2010 akatuahidi Barabara ya kutoka Kahama - Nyang'hwale kwenda Busisi itajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2013 Mheshimiwa Jakaya alikuja kwa mara nyininge akatuahidi vile vile. Mwaka 2015 mgombea mwenza ambaye sasa hivi ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan alikuja kwenye kampeni na akatuahidi kwamba barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami. Mwaka 2015, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwenye kampeni zake alipokuja, alituahidi ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu kuanzia mwaka 2010 mpaka leo hii 2021 hajawahi kuwekwa ndani ya mpango hata siku moja, hata bajeti hii nimeangalia hakuna mpango wowote ambao umewekwa ujenzi wa lami wa barabara hiyo. Wakati barabara hiyo inaunganisha Mikoa mitatu Shinyanga Geita na Mwanza. Barabara hiyo itafungua uchumi wa Nyang'hwale kwa sababu Daraja letu la kutoka Busisi - Kigongo Feri litakapokuwa liko tayari, kutoka Busisi kwenda Kahama ni kilometra chache sana kuliko kuzunguka Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema kama mwakilishi wa Jimbo la Nyang'hwale, kwa kweli sijaridhika,

naomba bajeti hii tuwaondoshe hawa Mheshimiwa Waziri na timu yake ikajipange upya. Kwa sababu kila Mbunge amesimama hapa anamlalamikia Mheshimiwa Waziri na Wizara yake hakuna hata Mbunge mmoja aliyeridhishwa na bajeti hii. Kwa hiyo naomba nitoe hoja, Wabunge wenzangu mniunge mkono, Wizara hii iweze kuondoka wakajipange upya Wizara hii

Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Amar kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASK. JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nimpe taarifa ndugu yangu na rafiki yangu kwamba Urais siyo mtu Urais ni taasisi. Anapoahidi Rais imeahidi taasisi ya Urais, kwa hiyo namshauri kwamba kama vile mimi nilivyoahidiwa pale Wazo, Mheshimiwa Rais alipopita pale akaahidi bilioni tano kwa ajili ya mafuriko, naamini Taasisi ya Urais itayatimiza hayo kwa hiyo namtaarifu avute subira tutatimiziwa tu nampa taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa yake Mheshimiwa siwezi kuipokea kwa sababu wananchi wangu hawatanielewa, niunge ama niache, ninachoomba ni kwamba mniunge mkono Wizara hii ikajipange upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamevunja kanuni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmeelewaka. Mheshimiwa Amar malizia mchango wako.

Ngoja kwanza Mheshimiwa Amar nifafanue jambo moja, maana, ngoja kidogo.

Waheshimwia Wabunge, naona mmesimama hapa kwa wingi baada ya kusikia neno Mheshimiwa Amar alikuwa anasema anataka kutoa hoja ili Bunge limtume Mheshimiwa Waziri akajipange upya ndo aje humu ndani. (*Makof!*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge taratibu tulizojiwekea sisi wenyewe haziruhusu hiki ambacho anasema Mheshimiwa Amar. Kwa hiyo malizia mchango wako Mheshimiwa.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji na wengine wote waliozungumza kama yeye, kwamba sisi Wabunge tunapaswa tunapochangia tumweleze Waziri na Serikali kwamba hizo pesa za barabara zote wakazipate wapi, kwamba Serikali sasa ingeamua iende ikope tujenge barabara halafu sisi tutalipa na watoto wetu hata kama ceiling itazidi. Naomba kumpa taarifa. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nilimpa fursa amalizie muda wake mjadala anaousema Mheshimiwa Mwijage yuko sahihi, lakini siyo katika mjadala ngazi hii, siyo mjadala wa ngazi hii. Ngazi zinazofuata hapo baadaye Waheshimiwa Wabunge yale aliyoyasema Mheshimiwa Mwijage tutaweza kuyatumia huko mbele. Kwa hiyo tuanje kutafakari wale Wabunge ambao wanatamani mambo yabadilike kutokana na haya yaliyowekwa humu basi waanze kutafakari namna ya kuishauri Serikali ipate wapi hizo fedha, lakini siyo kwenye mjadala wa ngazi hii ambapo tunajadili bajeti za kisekta.

Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe jana umelalamika sana jimboni kwako na wengine wote tunalalamika hivyo hivyo, lakini pia tukumbuke kwamba tunapowakusanya wananchi na kuwaeleza mipango ya Chama na Serikali itafanya nini mtakapotupa ridhaa, ni haya sasa ya kuwatengenezea yale ambayo tuliwaahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mimi kama Mbunge mwakilishi, kazi za Mbunge ni tatu; kuishauri Serikali, kuisimamia Serikali pamoja na kutunga sheria. Sasa leo hii mimi kama mwakilishi wa Jimbo nakuja hapa nakaa naunga tu mkono wananielewaje mimi wale kule?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane vizuri, nitaruhusu hii taarifa lakini Mbunge atakayesimama kwenye taarifa asiwe anachangia kwamba na Jimboni kwangu kunafanana na wewe, awe anampa huyo taarifa juu ya kile anachokichangia.

Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mchangiaji kwamba barabara hii ya Busisi - Nyang'hwale Kahama haina umuhimu tu kwenye Jimbo la Nyang'hwale isipokuwa ina umuhimu mkubwa sana katika Jimbo langu katika Kata ya Chela, Kata ya...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo niliyokuwa nayasema sasa, yaani Mbunge hujapata nafasi ya kuchangia unataka utumie kwenye taarifa kuchangia. Sasa kuanzia sasa hivi nitakuwa nawakata tu, Mheshimiwa Iddi kaa chini. Kuanzia sasa hivi ukisimama ukataka kuchangia unamkosea yule anayechangia kwa sababu kwenye Taarifa Rasmi za Bunge zitaonekana ulimpa taarifa

halafu unazungumzia mambo ya kwako wewe, tafuteni fursa ya kuchangia Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010 nilipata kura nyingi sana na Chama na Kiongozi Mkuu wa nchi alipata kura nyingi sana. Mwaka 2015 hivyo hivyo, 2020 hivyo hivyo kwa imani kubwa ya kwamba tutawatengenezea barabara wananchi hawa. Mwaka 2025 nitaenda kusimama niseme nini, lakini pia Wabunge wote wamelalamika kwa nini wasitoke wakajipange upya?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii si mara ya kwanza mimi ni awamu yangu ya tatu, tuliwahi kuiondosha Wizara ya Maji ikaenda ikajipanga upya, leo hawa vipi? Wabunge wote wamelalamika, mimi sina hata kilomita moja leo miaka 12, nitawaeleza nini wananchi. Naomba sasa kwamba Mheshimiwa Waziri safari hii sijui niunge mkono, sijui namna gani, lakini akajipange upya.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwitwa Mheshimiwa John Constantine Kanyasu atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo na Mheshimiwa Stella Fiyao ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa hotuba nzuri ambayo ameisoma. Kwa mara ya kwanza Tanzania imeweza kuuza dhahabu nje yenye thamani ya dola bilioni tatu na mauzo ya thamani ya dola bilioni tatu ya dhahabu sehemu

kubwa zaidi ya 60% karibu 70 ya dhahabu hii, inatoka kwenye Jimbo la Geita Mjini kwenye mgodi wa Geita *Gold Mine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mauzo kama haya ya dola bilioni tatu yaweze kuendelea lazima uchimbaji wa madini ambao kuna mgodi mkubwa kule wa *Barrick* na mgodi mkubwa wa *GGM* uwe *supported* na miundombinu ambayo tumekuwa tukiizungumza. Sasa iko Barabara ya kutoka Geita kwenda Kahama ambayo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema ameiweka kwenye mpango wa kujengwa, lakini ametenga bilioni sita kilomita karibu 140. Ni barabara muhimu sana katika mchango wa uzalishaji huu wa dhahabu lakini katika mawasiliano kwa sababu hii ndiyo barabara inayounganisha Mkoa wa Geita pamoja na Mji wa Kahama ambapo magari makubwa yote ya mizigo mikubwa yanayokwenda kwenye Mgodi wa *GGM*na Mgodi wa *Barrick* yanapita kwenye barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii iliombwa kwa mara ya kwanza mwaka 2007 na Mbunge anaitwa Mheshimiwa Mabina. Alikaa miaka yake 10 akaondoka, akaja mwenzangu marehemu Donald Max naye akaiomba naye akaondoka, nilikuja mimi mwaka 2015 nimeionba sasa mwaka 2021 kuna dalili za kuanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yangu kwa Mheshimiwa Waziri barabara hii ina umuhimu mkubwa sana, siyo tu mkubwa kama ambavyo watu wengine wanafikiria, ni kwa sababu ni *strategic*, hii barabara ina umuhimu mkubwa kutokana na mizigo mikubwa ambayo inapita kwenda kwenye Mgodi wa Dhahabu wa GGM, kwenda kwenye Mgodi wa Dhahabu wa Kakola, lakini kuna Mgodi mwengine mkubwa wa Dhahabu wa Nyanzaga ambao unaanza Sengerema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipitisha malori makubwa yenye mitambo mikubwa ukayapitisha kwenye daraja linalojengwa hili daraja halitadumu, ndiyo maana Wabunge wote waliotangulia waliomba barabara hii ya Geita kupitia Kakola kwenda Kahama iweze kujengwa, na ni barabara

ambayo mchango wake kwenye uchumi unaonekana wazi, kama leo tumefikisha dola bilioni tatu. Mwanzo nchi hii mapato makubwa ya *forex* yalikuwa kwenye utalii, sasa hivi mapato makubwa ya *forex* yako kwenye dhahabu. Dhahabu kama ndiyo madini tunayoyategemea, matarajio yangu ni kwamba barabara hii itapewa umuhimu mkubwa, tutaweka pesa za kutosha siyo bilioni sita ambazo zimewekwa sasa hivi ambazo naona ni kama vile bado tunafanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, jana Mheshimiwa Mbunge mmoja alizungumza kuhusu *performance* ya ATCL na akasema unaweza kwenda kukata tiketi ukaambiwa ndege imejaa, lakini baadaye ukiingia kwenye ndege ukashangaa ukakuta ndege iko nusu. Sasa jambo hili linafanana kidogo na jambo hili. Tumejenga Uwanja wa Ndege wa Chato, wananchi wanataka kuutumila uwanja huo, lakini ili uweze kutoka pale kwenye uwanja wa ndege kwenda Katoro kwenda Chato kwenda Biharamulo kwenda Geita ni lazima kwenye mipango ya Wizara wakati wanajenga uwanja ule wangefikiria jambo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kwenda China tulipelekwa na Bunge, tukateremka kwenye Uwanja wa Ndege wa Fuzhou, kutoka uwanja wa ndege huu kwenda kwenye mji tunaopelekwa ilikuwa ni kilometra 120, lakini *facility* zimetengenezwa na wenyewe uwanja, kuna mabasi pale ya kupeleka wale watu. Sasa mtu anajjiliza nikate tiketi ya laki sita kwenda nikatue Chato, halafu nitafute gari ya kunitoa kilometra 110 kunipeleka Geita au kilometra 100 kunipeleka Chato, haiwezekani! Sasa lazima Wizara ije na mpango wawe na *airport shuttle* ambazo ni za kwao, ambazo zitarahisisha watu wanaopanda ndege kwenda kule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ndege zetu zina bei kubwa sana sababu ni nini? Ndiyo maana haziwezi *ku-perform*. Bei ya ndege ni sawa na kwenda Dubai. Sasa kwanini tusitengeneze bei ambazo zinafanana na *network* na nchi yetu wenywewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Michael Mwakamo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao na Mheshimiwa Mwita Boniface Getere ajiandae.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara. Kwanza kabisa naomba nianze na kuieleza Serikali kwamba matumaini makubwa ya Watanzania wakiwemo Wanajimbo la Kibaha Vijiji ni kwenye llani yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia matumaini mengine katika hao wananchi, yapo kwenye hotuba na ahadi mbalimbali za viongozi. Vile vile naomba nileleze Serikali, sote tunafahamu kwamba hakuna kitu kibaya ambacho kinakwenda kumfanya mtu afedheheke kama ambavyo Imani yake ikapotezwa pasipo utaratibu na ndiyo maana waumini wengi na viongozi wengi wa dini wanawachukia sana vijana au yoyote anayetokea kuinajisi au kukiharibu au kutokuwa na imani na kitabu cha dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaombe Viongozi wa Serikali msisababishe wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiji wakashindwa kuiamini llani yao kwa sababu ya ahadi ya muda mrefu ya utengenezaji wa barabara ya kutoka Bagamoyo pale Makofia mpaka Vikumburu. Nalisema hili kwa nini? Kwa sababu nilipokuwa nimeuliza swali langu la msingi hapa Bungeni, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kwamba barabara ile inafanyiwa mchakato wa kutafutwa fedha kwa ajili ya matengenezo. Hata hivyo, nimekuja kupitia sasa hivi kwenye randama ya kitabu cha bajeti nakuta wameweka kilometra 39 ya kutoka Makofia mpaka Mlandizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuweka kilometra hizo, ukiangalia kwenye bajeti fungu la fedha liliowekwa ni kama kamewekwa kapessa kadogo kakushikia tu kifungu, lakini hawana mpango wa kuendelea nayo. Sasa

nataka ieleteweke, sisi sote tunapopitia vitabu hivi tunajua kuitafsiri namna gani kimewekwa. Namna walivyoweka fedha kwenye vile vifungu vya barabara ni kana kwamba wametuwekea mazingaombwe na hakuna kitu kitakachokwenda kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka niifahamishe Serikali kwamba tunapokwenda kufanya mchakato wa utengenezaji wa barabara, Waziri siku ile alithhibitisha mwenyewe kwanza kuna hatua mbalimbali za kufanya, sasa mpaka sasa hivi, hatua za awali hazijafanywa. Kwa mfano kutoka hapo Makofia mpaka Mlandizi ambako wao ndiyo wamekutaja kwenye bajeti kwamba wanataka kwenda kushughulika napo, mpaka leo watu wale hawajaanza taratibu za kupata utaratibu wa kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mara baada ya kujibiwa swalii lile, wananchi wengi wamepiga simu, wananchi wengi wa Kibaha kutoka Bagamoyo kuja pale Mlandizi wamelalamika na wamefika sehemu wamesema niwaulizie kwamba hivi hii Serikali kama wameshindwa kuutekeleza ule mradi wawaruhusu maeneo yao waendelee kuyatumia, kwani yana muda mrefu, yana miaka mingi, lakini fidia ile haijapata kulipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lipo jambo ambalo kwa kweli linasikitisha sana Serikali hii inafahamu kwamba Mkoo wa Pwani ni mkakati mkubwa sana wa viwanda na miundombinu kadhaa ikiwemo barabara ni msingi ili iweze kutoa bidhaa za maeneo yale, lakini pia inafahamu pamoja na kuwepo kwa utaratibu wa kupatikana barabara hizo tunahitaji kuziimarisha bandari zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika Mkoo wa Pwani tunayo bandari moja ya Kisiju, Kisiju ni bandari ya muda mrefu ni bandari kongwe ya miaka mingi, haitajwi popote, inapotezwa hivi hivi. Lakini kama yote hayo hayatoshi ndugu zangu inawezekana inaonekana labda Mkoo ule hauna uchumi, lakini hivi kweli hatukumbuki kwamba Mkoo ule umemtoea Rais Mstaafu ambaye ameitendea Taifa hili

shunguli kubwa kubwa sana nchi hii, kwanini tusimpe hata faraja ya kuona baadhi ya barabara za mkoa zinawekwa lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mtu amelitumikia Taifa kiasi hiki leo hii mtu wa kutoka Mzenga akiamua kutaka kumsalimia Mheshimiwa Kikwete pale Msoga hawezi kufika, hivi tunamtendea busara ya kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu spika, kwa hiyo, niombe kwamba Serikali itafakari naogopa kusema kama alivyosema mzee wangu kwamba wakajipange upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwakweli inatia uchungu na hii dalili ambayo Wabunge wameionyesha wizara inatakiwa ijuwe kwamba wabunge wanakerwa na taratibu za barabara hebu waongeze nguvu tumechoka kuwa na ilani ndefu yenye maadili mengi lakini hayatekelezeki matokeo yake tutawafanya watanzania wachoke kuisikia ilani yetu jambo ambalo hatupendi itokee na tunauhakika chama chetu kinauwezo wa kuisimamia Serikali na kama Serikali inaona kwamba ahadi zile ni nyngi wafanye utaratibu wa kupunguza ahadi zile ili tutowe ahadi zinazotekelzeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hili, lakini pia naomba nzungumze jambo moja, naungurumiwa huku nashindwa kuendelea. Lakini nataka kukiongezea hapa upo mradi wetu wa *Standard Gauge* unaendelea nilzungumza na waziri, nilzungumza na viongozi mbalimbali pamoja na mradi ule unafaida kubwa lakini wapo wananchi wa Ruvu *Station* wapo wananchi wa Kwara mradi umewapita fidia zao hawaajapewa mpaka leo sasa hivi vitu kwa kweli vinasikitisha na vinapoteza nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona umewasha basi niseme tu naunga mkono hoja lakini kwakweli atakapokuja kutoa maelekezo atoe utaratibu ni namna gani tuaendelea. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Fiyao, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Boniface Getere, Mheshimiwa Leah Jeremia Komanya, ajilande.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonyesha wazi kabisa kuna changamoto kubwa sana ya miundombinu ya barabara katika nchi yetu, na hii changamoto inaikabili nchi yetu kwa Kiswahili chepesi tunaweza tukasema hili ni Janga la Taifa kwa sasa, kwa sababu karibu kila Mbunge aliyesimama hapa ameweza kuzungumzia changamoto ambayo inamkabili kwenye Jimbo na kwenye Mkoa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inaonekana ni changamoto kubwa sana na tuseme tu wazi uchumi wa Taifa letu kwa asilimia kubwa pia unategemea miundombinu mizuri ya barabara. Ili uchumi uweze kukua ni lazima kuwe na miundombinu ilio mizuri, wawekezaji hawawezi kuja kuwekeza mahali ambapo pana miundombinu mibovu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni katika Mkoa wetu wa Songwe, katika Mkoa wetu wa Songwe tuna ardhi nzuri yenye rutuba ya kutosha, lakini changamoto kubwa ambayo inasababisha wawekezaji washindwe kuja kuwekeza ndani ya Mkoa wetu ni kutokuwa na miundombinu ilio mizuri ya barabara. Muwekezaji kwa namna yoyote anapokuja kuwekeza eneo lolote lile kitu cha kwanza anaangalia miundombinu imekaaje, je, kama atalima mazao, atavuna atayafikishaje eneo la soko? Mwisho wa siku tumekosa wawekezaji kwa sababu kubwa tu ya miundombinu kuwa mibovu ya barabara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Jimbo la Tunduma, ndani ya Jimbo la Tunduma tuna barabara ambazo wananchi walipisha kutoka mwaka 2016/17 walipisha kwa hiari yao wenyewe wakavunja zile nyumba ili

kupisha barabara, lakini mpaka leo hili jambo la barabara limekuwa ni stori kwa wananchi wa mji wa Tunduma na badala yake wameishia kuambulia vumbi na kuugua mafua yasiotibika kila kunapoitwa leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anasimama atuambie ni lini atawenza kukamilisha barabara hizi ambazo wananchi wamepisha kwa hiari yao wenye we pia kulipwa fidia ya aina yoyote ile ni lini atawenza kuzijenga barabara hizi, ili mwisho wa siku wananchi wa Tunduma wasikatishwe tamaa kwa jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi. Ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi umekuwa ukilisababishia Taifa kupata hasara kubwa sana. Kwa mujibu wa ripoti ya CAG ya mwaka 2021, ripoti ya CAGimezungumza wazi kabisa katika ujenzi wa reli ya SGR hasara namna tulivyopata kwa sababu ya wakandarasi kucheleweshewa kupata fedha zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti inasema kipande cha kwanza cha ujenzi wa Reli ya SGR wakandarasi walicheleweshewa kupata fedha zao ndani ya muda walokubaliana ndani ya muda wa siku 56, lakini baada ya kuchelewesha Mhandisi Mshauri aliweza kupokea nyaraka za madai na vielelezo ambavyo wakandarasi walikuwa wakiidai Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho wa siku riba iliyotozwa kwa ucheleweshwaji wa wakandarasi ilikuwa ni dola za kimarekani milioni moja na laki mbili na elfu themanini na sita na pointi tisini na moja (\$1,286,000.91) ambazo kwa fedha za Kitanzania ilikuwa ni takribani bilioni mbili na milioni mia tisa themanini na tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inaonyesha namna gani ambavyo Serikali tunapata hasara za kizembe na fedha hizi ziliidhinishiwa na hao wakandarasi wakalipwa fedha hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata wasiwasi ni hasara ngapi ambazo tunazipata kutokana na wakandarasi kucheleweshewa kulipwa fedha zao kwa wakati, wakati huo fedha zote hizi zingetusaidia kutekeleza miradi mingi ambayo wabunge wamekuwa wakiipigwa kelele ndani ya Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuepusha mianya ya ufujaji fedha za umma tunaomba Serikali ilisimamie jambo hili kuhakikisha wakandarasi wanalipwa fedha zao kwa wakati ili kuepukana na kuiletea Serikali hasara zisizokuwa na msingi. (Makofi)

**MHE. RIDHIWANI J.M. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante sana muda wake umekwisha Mheshimiwa

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RIDHIWAN J. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tumsaidie tu Mheshimiwa Mbunge anaofoka sana anatumiza masikio.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Nakula vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Jamani hizo ni ishara kuonyesha kwamba akinamama tukikutana huko nje mambo yatakuwa mazuri.

**MBUNGE FULANI:** *Covid- 19* hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Amandus Chinguile, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Lakini naomba nianze kwa kuunga hoja bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, lakini niishukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti liliologharimu shillingi bilioni 34.5. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hilo liko kwenye barabara inayotoka Kolandoto – Lalago, Mwanuzi – Sibiti, Matala mpaka Junction ya Karatu. Barabara hii ni barabara ambayo jana Mheshimiwa Flatei alitaka kuirukia sarakasi, Mheshimiwa Mbunge alikuwa na haki kwa sababu barabara hii ni ahadi ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, nikushukuru na niishukuru Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza daraja hilli la Sibiti na barabara unganishi yenye km 25 kwa ujenzi wa lami.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Flatei.

## TAARIFA

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Leah, barabara hiyo haipiti kule inapita Singida kuja Haydom kwenda Mbulu kwenda Karatu, kwa hiyo siyo hiyo anayosema.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Leah Komanya unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LEAH J. KONANYA:** Naipokea taarifa ni hiyo hiyo nilifupisha kwa ajili ya kuokoa muda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha daraja la Mto Sibiti na

barabara unganishi. Barabara hii ya km 25 ni muhimu sana, nimuombe Mheshimiwa Waziri aje kuionna kutokana na changamoto ya eneo Ililopo, eneo hilo ni mbuga kali sana na ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe umechukua miaka mingi sana mpaka kukamilisha, nimuombe aje aone ili ajue ni wakati gani aanze kujenga barabara hiyo kwa sababu sasa imeanza kuliwa na mvua ambayo inaweza ikapelekea hasara nyingine kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa kuanza kuonyesha nia kujenga hii barabara niliyoitaja angalau kwa kutenga bilioni 5, angalau imeonyesha nia ni zaidi ya miaka 25 hii barabara imekuwa ikiwekwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, angalau sasa shilingi bilioni 5 zimetengwa. Mimi kama Mbunge niliomba kipaumbele kipelekwe katika ujenzi wa madaraja katika mito iliyo karibu na daraja la Sibiti ambayo ni Mto Itembe, Mto Chobe, Mto Nkoma na Mto Liusa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kujengwa kwa madaraja katika Mito hii kutaleta tija katika daraja la Mto Sibiti kwa sababu daraja hili limekuwa mara nyingi likitumika tu wakati wa kiangazi wakati limechukua shilingi bilioni 34. Na matumizi ya barabara hii ni makubwa kutokana na magari ya mizigo yanayotoka Musoma, Mwanza, Simiyu kuelekea Iguguno. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali imeonyesha pia katika kipande cha kutoka Mkalama mpaka Iguguno ambayo ni barabara ya kutoka Bariadi, Kisesa, Mwandoya, Mwanuzi, Sibiti mpaka Iguguno kwamba wako kwenye hatua ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wanafanya hiyo niiombe *TANROADS* Singida, kipande cha kutoka Mkalama hadi Nduguti, Gumanga hali ni mbaya sana, hakuna changarawe inayoweka ya kutosha na kufanya magari haya kudidimia. Ninaungana na Mbunge wa Wilaya ya Mkalama ambaye alichangia jana, magari yamekuwa yakizama

kutokana na barabara hazijatengenezwa vizuri kwa kiwango cha changarawe na ili hali fedha hizi zinatoka kwenye mfuko wa *TANROADS* ambao sisi tunaamini *TANROADS* ina fedha za kutosha kuliko mfuko wa *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe ombi katika jimbo langu, nitoe ombi la kuipandisha hadhi barabara ya Mwanuzi – Mwabuzo. Barabara hii inatengenezwa na *TARURA* na kwenye kikao cha barabara cha Mkoa niliomba nikakubaliwa, lakini tuliambiwa tusubiri Serikali iidhinishe upandishaji wa hadhi. Barabara ni muhimu ambayo itaunganisha mpaka Wilaya ya Igunga ni muhimu kiuchumi kwa sababu wafanyabiashara wa Wilaya ya Meatu, Maswa, Singida wote sasa wanaelekeia Igunga kwa ajili ya kupata bidhaa hiyo, hivyo na kuchocheara uchumi katika Wilaya ya Meatu na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla. (*Makofi*)

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngasa.

## TAARIFA

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mchingiaji kwamba wafanyabiashara wanaotoka Meatu, Shinyanga na Simiyu pamoja na Singida, imefikia hatua wamelipa soko la Igunga jina Kariakoo ya Igunga na kila Jumatano wanakuja pale kufanya mnada na kununua bidhaa. Kwa hiyo, kama anavyoomba Mheshimiwa taarifa kuhusu barabara yake, naomba nimpe taarifa ili aweze kupewa kipaumbele na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge narudia tena, mmesikia taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Massay? Mmeisikia Wabunge? Maana saa nyingine tunaongea sana kwa hiyo hatusikilizi. Taarifa inayoweza kutolewa ni kama ile, sijui kama

tunaelewana vizuri! Tutumie muda wetu vizuri, wabunge wengi wanataka kuchangia hapa mbele sawa jamani, nadhani hilo limeeleweka. Mheshimiwa Leah Komanya malizia mchango wako.

**MHE. LEAH J. KONANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali kwa kuonyesha nia sasa ya kujenga daraja la Mto Simiyu upande wa Mwanza ambalo linaunganisha Mkoa wa Simiyu kwa upande wa Wilaya ya Busega. Barabara hii ni muhimu pia kwa magari yanayoteka Rwanda, Mwanza na mikoa mingine kuelekea Nairobi. Lakini kumekuwa hakuna mahali pa kupishana lakini niipongeze Serikali, imeonyesha nia kwa kutafuta fedha kwa kupitia Benki ya Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Amandus Chinguile, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, ajiandae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na wizara yetu ya Ujenzi, nichangie kwenye eneo la barabara ya Kibiti - Lindi, barabara hii haina muda mrefu lakini kwa sasa ina maeneo korofi kweli kweli niombe wizara ifanye kadri inavyoweza ili yapitie maeneo haya na kuyarekebisha mara moja. Maeneo haya Mbwemkuru, Malendego mpaka Nangulukuru kipande hiki ni kibovu kweli kweli na kinaweza kikasababisha ajali endapo hazijachukuliwa hatua za makusudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninzungumzie eneo la barabara za kutoka Nangulukuru kwenda Liwale, Liwale - Nachingwea, Nachingwea - Ruangwa, Ruangwa - Nangulukuru. Maeneo haya yamedumaa kwa sababu pamoja na mambo mengine ni hali ya barabara ya maeneo haya, tukijengewa barabara maeneo haya hata kiuchumi yatakwendwa kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa masikitiko makubwa niendelee kusema tu kwamba maeneo haya tunazalisha korosho kwa wingi, tunazalisha ufuta kwa wingi, lakini barabara zake ni mahandaki. Niombe sana sana wizara iweke upendeleo maalumu kabisa. Mheshimiwa Mbunge wa Liwale hapa amezungumza, amezungumza jana tena kwa hisia kali kabisa, kwa kweli ipendeze baada ya Bunge hili au wakati Bunge linaendelea Mheshimiwa Waziri aende akatembelee haya maeneo akajionee mwenyewe. tunachokizungumza tunamaanisha watu wetu wanapata shida kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa unyenyekevu mkubwa nizungumzie kipande cha barabara kutoka Masasi kwenda Nachingwea. Wakati tunafunga kampeni za uchaguzi mwaka jana aliyekua Rais wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hayati alizungumza na wapiga kura wa Jimbo langu la Nachingwea kwa njia ya simu na kati ya vitu alivyowaahidi ni barabara hii ya Nachingwea kwenda Masasi kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye kumbukumbu ya barabara hii upembizi yakinifu umeshakamilika miaka mitano iliyopita, lakini mwaka 2016 ilitengewa shilingi bilioni moja kwa maana ya kishika kasima hakuna kilichoendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na saba kumi na nane ilitengewa bilioni 3.5 hakuna kilichoendelea 2018/2019, 2019/2020 ikatengewa bilioni 1.3, 2020/2021 ikatengewa bilioni 1.4 mwaka huu imewekewa bilioni 1.5. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Waziri atakapokuja kujibu hapa kwa kweli nitashika shilingi kama huna maelezo yatakayotoa matumaini ya lini barabara hii itajengwa, na kwenye hotuba yako huku nimeona Mheshimiwa Waziri amesema Serikali inaendelea na kutafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya Masasi – Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetafutwa kwa miaka mitano, upembuzi yakinifu na vitu vingine vimeshakamilika hebu tuchukuwe juhudzi za makusudi kwa ajili ya watu wetu hawa. Watu hawa wanajuwa kujiletea maendeleo yao wenyele lakini kama miundombinu ikiwa ni shida kwa kweli hii haikubaliki. Nitaishikilia shilingi hiyo Mheshimiwa Waziri mpaka mwisho ili nione unawatendea haki wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nizungumzie pia changamoto nyengine ya kipande cha barabara nilichokizungumzia cha kutoka Nachingwea - Ruangwa. Tukumbuke Ruangwa yupo Mheshimiwa Waziri Mkuu anateremka Uwanja wa Ndege wa Nachingwea hii barabara ni mbovu. Naomba tufanye juhudzi za makusudi ili kuwezesha hata viongozi wetu wakiwa wanateremka uwanja wa ndege waweze kutembea kwenye barabara ambazo kwa kweli watakuwa na usalama zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara ya kutoka Masasi - Lindi ina matuta na mimi nafikiria hawa wakandarasi au wahandisi wetu walifkiria nini maana haya matuta ni makubwa kiasi ukiendesha *speed* hata kama ni 60 ukipita kwenye hilo tuta utapata ajali tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsate sana, kengele imegonga.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Salim Hasham ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kuhusu barabara, mipango mizuri ya Serikali ipo lakini nachoomba ni utekelezaji. Naongelea barabara ya Ngiloli - Iyogwe - Kilindi (Tanga). Tatizo hapa tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu jambo kubwa lingine ni kuhusu madaraja. Kuna madaraja ya Chakwale na Nguyami. Madaraja haya yanajengwa kila mwaka lakini mwaka mvua ikinyesha yanakatika. Je, ni lini haya madaraja ya Chakwale na Nguyami yaliyopo Gairo yatajengwa kwa ukamilifu ili kuondoa tatizo la kukatika kila mwaka kwani tunaharibu fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine nayoongelea ni ambayo imeshaongeleta ni ya Kidatu - Ifakara - Malinyi - Londo - Kitanda - Namtumbo. Barabara hii tumeiongelea mara nyangi humu Bungeni inasuasua na ni ya muhimu sana. Kwa hiyo, mipango yote iliyopangwa tunaomba itekelezwe kwa sababu tumeiongelea muda mrefu na lakini hakuna utekelezaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine ni ya Bigwa - Mvuga - Kisaki ambayo inakwenda mpaka Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere. Tunashukuru imewekwa kwenye mpango na imetengewa kiasi kidogo cha fedha, lakini kwa umuhimu wake tunaomba mipango yote iliyopangwa iweze kutelezwa kwa sababu nayo hii barabara tumeiongelea miaka nenda miaka rudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine ni Ubena - Zamozi - Ngerengere - Mvuga - Kisaki. Barabara hii nayo imetengewa fedha kiasi lakini kutenga sio kutenda, tunaomba itekelezwe kama ilivyopangwiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine ni Dumila - Magole - Turiani - Mziha - Handeni. Hii barabara nayo tumeiongelea lakini nashukuru kipande cha Magole - Turiani kimetengenezwa kwa lami, kipande cha Turiani - Mziha - Handeni bado hakijatengenezwa. Naomba kufahamu hiki

kipande kitatengenezwa lini? Kipande hiki pia kimetengewa fedha lakini naomba utekelezaji uende kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Dumila - Ludewa - Kilosa - Mikumi tumeiongelea mara nyngi. Barabara ya Dumila - Ludewa tayari imejengwa kwa kiwango cha lami na barabara ya kutoka Ludewa - Kilosa ujenzi unaendelea. Tatizo ni kipande cha barabara ya kutoka Kilosa - Mikumi, usanifu ulishafanyika muda mrefu, sasa mnasema mipango ya kutafuta hela inaendelea, sasa itaendelea mpaka lini? Naomba kujua kipande cha barabara ya kutoka Mikumi - Kilosa kitatengenezwa lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ifakara - Lupilo - Mahenge - Mwaya, sijaiona kwenye mpango wowote. Watu wa Mahenge tunaomba hii barabara kwa sababu Mahenge ni Wilaya inayozalisha sana mpunga na kuna madini. Naomba na barabara hii iweze kuonekana kwenye mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ifakara - Mlimba - Lupembe; wakati wa mvua huwezi kupita. Tunaomba na yenye we itengenezwe vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Kihansi - Madeke - Njombe. Hii ni barabara inayounganisha mikoa miwili ambapo tunaweza kufanya biashara kama itatengenezwa mpaka Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya mwendo kasi. Tuinashukuru sana Serikali kwa kujenga hii reli ya mwendo kasi ambapo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kuanzia Dar es Salaam - Morogoro imefikia asilimia 91, tunashukuru. Tunaomba ujenze uende vizuri kusudi tuweze kuifaidi kama ilivyokusudiwa ambapo wananchi wa Morogoro wataweza kunufaika kwa kufanya biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo nilipenda kuchangia, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hasham na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma ajandae.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote, napenda niishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imetekeleza miradi mingi na mikubwa kwenye Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Wizara kwa ulipaji wa fidia wa kupisha Uwanja wa Ndege wa Msalato, ambapo wananchi wameanza kulipwa fidia zao. Vilevile, naishukuru sana Serikali kwa sababu wameanza maandalizi ya malipo ya fidia kwa wananchi ambao wanapisha *Outer Ring Road*. Nashukuru sana kwa hatua hiyo. Pia naishukuru sana Serikali kwa kuwa hivi sasa ile barabara korofi ya kuanzia Nyuka - Mvumi kuzunguka Kikombo ya kilometra 76 muda wowote zabuni itatangazwa ianze kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi, hapa Dodoma panajengwa barabara ambayo ni *Outer Ring Road, Middle Ring Road* na *Inner Ring Road*. Kwenye *Inner Ring Road*, wananchi wangu wamesimamishwa kuendeleza maeneo yao kwa muda wa takribani miaka miwili hivi sasa; wananchi wa maeneo ya Nzuguni, Mbuyuni, Chidachi na Nkonze. Wananchi hawa wote wanashindwa kuyaendeleza maeneo yao kwa sababu wanaambiwa kuna mradi unakuja wa *Inner Ring Road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, kama mradi huu haupo tayari au hautekelezwi tunaomba wananchi wale wapewe taarifa kwa sababu ni muda mrefu umepita. Katika baadhi ya maeneo zoezi la urasimishaji makazi limeanza lakini wananchi hawa wanashindwa kurasimishiwa kwa sababu ya mradi huu ambao tunautengemea na bado haujafika. Hivyo, namuomba Mheshimiwa Waziri kwenye hii *Inner Ring Road* atuambie kama barabara hizi zipo au hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati anaweka jiwe la msingi pale *SGR*Ihumwa aliahidi zile kilomita kadhaa kutoka barabaran pale Ihumwa kwenda mpaka kwenye stesheni kule. Namwomba Mheshimiwa Waziri pia aliangalie hili kwa sababu ni sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushie barabara ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu juzi ya Ihumwa - Hombolo - Mayamaya zaidi ya kilomita 57 ambayo na yenye pia ipo kwenye llani ya Uchaguzi. Naomba Serikali iangalie kwa sababu mnaweza mkashughulikia hizi *Outer Ring Road* na mkahisi kwamba Dodoma ina barabara nyingi sana. *Outer Ring Road* lengo lake kubwa ni kupunguza msongamano wa magari makubwa hapa jijini lakini siyo barabara ambayo inakwenda kuwagusa wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo, ziko barabara ambazo zinawagusa wananchi moja kwa moja ikiwemo hii ya Hombolo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri katika mipango ya Serikali muiangalie barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu wananchi wanapata shida kubwa sana na gharama za usafiri zimekuwa kubwa sana kutoka Hombolo kuja hapa mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia iko barabara ambayo wenzangu Mheshimiwa Dkt. Chaya na Mheshimiwa Nollo wamezungumzia; barabara ya kutoka Manyoni - Bahi inatokea Mbabala na kuikuta *Outer Ring Road*. Barabara hii ina mchangao mkubwa sana kwa wananchi wetu wanaotokea pembezoni, ikinjengwa kwa kiwango cha lami itakuwa imesaidia sana kwa sababu inakuja pia kuungana na barabara ya *Outer Ring Road* ili tuweze kuwarahisishia wananchi wetu usafiri na hasa kwa kuwa inagusa takribani majimbo zaidi ya mawili kwa maana ya Jimbo la Manyoni lakini vilevile Jimbo la Bahi na Jimbo la Dodoma Mjini. Ni barabara muhimu sana tunaomba Serikali iweze kuiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna changamoto wananchi wengi wakikutwa kwenye barabara ambao wanapaswa kusubiri utekelezaji wa miradi ya barabara,

wenyewe wanapaswa wasubiri mpaka Serikali ikiwa tayari kujenga barabara lakini tunawatesa sana wananchi kama hawa ambao nimewasema wameacha kuendeleza maeneo yao wanabubiri mpaka Serikali ikiwa tayari kutekeleza miradi hii. Hii siyo Dodoma tu ni nchi nzima, naomba Serikali iweke utaratibu ambao hautamuumiza mwananchi wa kawaida, kama bado hatuko tayari tusiwasimamishie wananchi hawa uendelezaji wa maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Salim Hasham atafuatiwa na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma na Mheshimiwa Daniel Awack ajiandae.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia katika Wizara hii japo nimeona malalamiko mengi sana ya Wabunge kuhusu suala la barabara na kuna uwezekano mkubwa sana Serikali ikawa haina bajeti kubwa kwa ajili ya barabara lakini inawezekana pia ikawa hawajajipanga vizuri kwenye mgawanyo kwa ajili ya barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie barabara za upande wa jimbo langu; kuna barabara ya kutoka Ifakara - Ulanga kujengwa kwa kiwango cha lami, imekuwa bingwa kuongoza kutajwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu lakini mpaka leo hii sijaona hata kilometra moja ambayo imetengewa barabara ile ili wananchi wangu wa Ulanga waweze kupata barabara ya lami. Hata kama ni kwa kilometra chache basi mgawanyo ule ungezingatia kidogo kuona kwamba watu wengi wana uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mwenzangu jana alitaka kuruka sarakasi hapa kuona kwamba kuna mtu ana lami anaomba bajeti ya kurekebishiwa lami yake wakati sisi wengine hatuna lami na hatujawahi hata kuiona. Sijui

huwa wanatumia vigezo gani, kiukweli inaumiza sana.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuja na *special case* kabisa, kwenye jimbo langu kuna daraja liko kwenye Kijiji cha Ikangao ambayo inaunganisha Kata mbili za Ilonga na Ketakeli. Daraja lile limekatika na linahudumia zaidi ya watu 28,000 na wanafanya shughuli za maendeleo ikiwemo ni pamoja na kilimo. Watu wale mwaka jana walilima ufuta walikuwa wanauz Sh.3,000 kwa kilo, baada ya daraja lile kukatika wakawa wanauz ufta kwa shilingi 1,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia suala la kilimo ni lazima tujue kwamba bila barabara hakuna kilimo ambacho kitaenda kwa sababu mazao yale hayawezi kufika sokoni kabisa. Naomba sana Mheshimiwa Waziri mara Bunge litakapoisha nifanye naye ziara kwenye jimbo langu kwa sababu jimbo lile limesahaulika kabisa. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri yupo hapa, naomba daraja hili liende likajengwe, mimi sitaki kujua fedha zitatoka *TARURA* au *TANROADS*.

Naomba wananchi wangu wakajengewe daraja hili kwa sababu lisipojengwa tena mwaka huu ina maana biashara zitakuwa zimekufa na wale wananchi mwaka ujao inawezekana wasilime kabisa kwa sababu hawana wanakoweza kupeleka bidhaa zao. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutaendeleza sana kudumaza uchumi wa nchi hii kama hatutazingatia suala la barabara. Barabara ni muhimu sana, huwezi kuzungumzia viwanda kama hujazungumiza barabara, huwezi kuzungumzia kilimo kama hujazungumzia barabara. Kwa hiyo, mimi niwaombe sana, inawezekana kweli Wabunge wengi wamelalamikia suala la barabara, kuna uwezekano kwamba mkatakiwa kwenda kujipanga vizuri lakini pia hata kama mkienda kujipanga naomba sana daraja hili lipewe kipaumbele ili wananchi hawa waweze kuendelea shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madaraja mengine ambapo wananchi tumejipanga kwenda kufanya kazi wenyewe kujenga daraja lille kwa sababu watu wanakufa kwa ajili ya kuliwa na mamba. Tumesema tutaenda kufanya kazi na wananchi wangu kwa kuweka hata daraja la mbao ili waweze kuendelea na shughuli zao lakini hili ni daraja kubwa sana ambalo linaunganisha watu wengi sana. Hawa nimezungumzia wananchi wachache 28,000 kutoka kwenye hizi kata mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Samweli Hhayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Awack na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwani kuna siku mimi na Mheshimiwa Flatei tulimuelezea kuhusu barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom - Katesh jinsi ilivyo na umuhimu wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Alikuwa msikivu hatimaye akamtuma Naibu Waziri kutembelea barabara hii lakini nikiri kwamba Mheshimiwa Waziri bado hajajitikisa vya kutosha kwa sababu kwenye bajeti hii sijaona chochote ambacho kimetengwa kwa ajili ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imeahidiwa muda mrefu toka 2005 mpaka wakati wa bajeti ya 2021, Mbunge aliyenitangulia Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu aliomba hapa Bungeni akakumbushwa na Mheshimiwa Mavunde kwamba kwa sasa sua limezama, ni barabara imeahidiwa muda mrefu. Kwa sababu ya umuhimu wake barabara hii inaunganisha Wilaya ya Mbulu na Wilaya ya Hanang lakini hapo katika kuna mashamba makubwa ya ngano. Tunaaagiza ngano kiasi kikubwa sana nje ya nchi, tunatumia fedha za kigeni, tukiwekeza kwenye barabara hii wananchi watazalisha na ngano ya kutosha itapatikana kutoka kwenye Jimbo langu la Hanang. Tutaokoa zile fedha tunazozitumia

kununua ngano nje ya nchi lakini pia itarahisisha huduma kwa wananchi wanaotegemea Hospitali ya Rufaa ya Haydom. Mheshimiwa Waziri kwenye barabara hii tumesema sana, barabara imeahidiwa muda mrefu, naomba ujiguse ili barabara hii ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna barabara yetu kutoka Naangwa – Gisambalang – Kondoa, ile barabara haipitiki kabisa wakati wa mvua. Kuna daraja la Muguri B limeondolewa na mafuriko ya 2019/2020 ili mvua kubwa. Tumeambiwa kwamba sasa kuna zoezi la usanifu ili kujenga daraja jipya, lile ni suala la dharura, wananchi ambao wanategemea barabara ile kwa shughuli zao zaidi ya laki tatu, mvua zikinyesha hakuna chochote kinachofanyika maana yake uchumi wa wananchi unakwama na Serikali inakosa mapato. Hilo naona mlione kama ni suala la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna barabara yetu ya kutoka Dareda - Bashinet - Lukumandar - Secheda - Basonesh – Hilbadauh, upande wa Singida barabara hii iko chini ya *TANROADS* na inatengenezwa vizuri. Wananchi wa upande wa Manyara wanajiuliza sisi tumekosa nini upande huu kwa nini barabara isijengwe vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mheshimiwa Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe ajiandae.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Nami niungane na wenzangu ambaao kwenye wilaya yao hawajapata chochote kwani nami ni mmojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Karatu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mjue ni jimbo ambalo limekombolewa kutoka kwenye miaka 25 ya kutawaliwa na Vyama vya Upinzani. Wakati tunatafuta kura tukiwa na wenzangu wa Chama cha Mapinduzi wakiwepo viongozi

wakuu akiwepo Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi Taifa ambapo wakati huo alikuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi kule tuliahidi mengi. Tuliahidi barabara ya kutoka Karatu - Njia Panda - Junction Matala barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu, hiyo ni kilometra 328 ambazo ziko kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi lakini hakijatengwa kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutoka hii barabara ambayo Mheshimiwa Flatei anataka kupiga sarakasi imeanzia Karatu, katika llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi lakini wameenda kuweka kilomita 25 pale Mbulu kwenda Haydom. Barabara hii kwenye llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi imeanzia Karatu - Mbulu - Haydom - Singida. Mimi silalamiki kwamba kwa nini wale wa Mbulu wamepata kilometra 25, niseme tu kwamba sasa Mheshimiwa Waziri sisi Karatu atutengee kiwango kidogo ili na sisi tuwepo katika kula matunda ya nchi hii ambayo tumeyakosa kwa miaka 25 tukiwa chini ya Upinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli pale Karatu Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kilometra 2 katika Mji wa Karatu lakini mpaka leo hakuna hata kilometra moja. Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kilometra 10 kwa mwaka wa 2015 leo ni mwaka 2021 hakuna hata kilometra moja. Mwaka jana tarehe 24 wakati Rais wa Jamhuri wa Tanzania Hayati Dkt. Magufuli akininadi alisema kama anajenga *fly overs* Dar es Salaam hashindwi kujenga kilometra 10 katika Mji wa Karatu. Sasa nashangaa tena kwenye bajeti hii hamna hata kilometra moja sasa wananchi wale 2025 nitawaaambia nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliongea kwamba mwaka 2025 kwenye Jimbo lake la Tanga hawezি kurudi kama hajafanikisha maendeleo ambayo ameahidi kwa wananchi wa Tanga Mjini. Nami kwa wale wa Karatu tulivyoahidi Chama cha Mapinduzi na tukiwa na viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwamba tunaweza kuleta maendeleo kwa *speed mkikichagua* Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Karatu walijitahidi kuchagua Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, nami kilio hiki nimefikisha kwenu ninyi Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ni ombi langu kwamba maombi haya yatazingatiwa na kilometa hizi kumi ndani ya Jimbo la Karatu tuweze kupata na kilometa hizi kutoka Karatu – Mbulu – Singida tunaweza kupata, vilevile barabara hii ya kutoka Oldeani – Mangola – Matala – Lalago kule Simiyu; na barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Simiyu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, tuliniadi llani ya Chama cha Mapinduzi na wananchi walio wengi waliamini ahadi kubwa sana ya Chama cha Mapinduzi na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ni imani yangu kwamba llani ile ya Chama cha Mapinduzi ili wananchi waendelee kuiamini, kwamba sasa inaweza kwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Vilevile nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wawili na watendaji wote wakuu wa taasisi ambazo ni za Wizara hii tunayoizungumzia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wabunge sana. Wabunge wamefanya kazi kubwa sana kuanzia jana. Kazi waliyofanya ni kazi yao ya Kikatiba. Naomba nikiri, kweli mimi tangu nilipochangia hotuba ya Waziri Mkuu nilizungumzia barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Serikali kitu kimoja; mnajenga barabara, lakini mnajenga barabara

ambazo sizo. Hamjafanya *research* ya kutosha mkajua barabara zinazostahili kujengwa. Mnarudia barabara zile. Serikali imesoma hotuba hapa, lakini hotuba ambayo Serikali mmeisoma ni ya Serikali; hotuba ambayo inapaswa kutekelezwa na Serikali, ni hotuba inayotoka kwa wananchi hawa; hawa Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikajua kwamba wanaozijua barabara hizi ni Wabunge. Wabunge ndio wanaotoka wananchi walipo; Wabunge wanawakilisha wananchi kwenye majimbo yao, ndio wanaozijua hizi barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ukweli, sitaki kusema kwa kirefu, lakini Serikali niwaombe sasa, tena nawaomba kwa mara ya pilli; fanyeni kazi kubwa kuanzia kesho, mpite nchi nzima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mkazijue hizi barabara. Barabara nyingi vijijini hamjazijenga ndiyo maana kumekuwa na kelele mno hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Wabunge wote waliosema, hakuna kichaa hata mmoja humu. Wote wana akili timamu. Haiwezekani mtu na akili zake timamu atake kucheza *karate* humu ndani, hapana. Anaogopa 2025 watammeza Wajumbe. Hali ni mbaya sana kwenye majimbo yetu, hasa ya vijijini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali nawaomba – tena nisime kwamba nawaomba, hapana; nawasimamia sasa. Haya ni madaraka yangu niliyopewa na Katiba kwamba niwashauri, lakini wakati mwingine niwasimamie. Hamzijui barabara ambazo mnapaswa kuzijenga. Barabara nyingi sana, zote zilizotajwa na hawa Wabunge hapa, ndizo barabara ambazo zinahitaji kujengwa. Hotuba mliyoisoma hiyo, sasa pateni picha kamili, hotuba ni hii huku. Hii huku ndiyo hotuba. Sisemi lugha tofauti, lugha yangu ni kwamba hotuba mnayopaswa kuiangalia ni hii inayotoka huku sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nimeeleweka.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANNE K. MALECEL**A: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu mbili nizungumze kitu kimoja; barabara nimeeleweka...

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ANNE K. MALECEL**A: Hapana, dakika mbili bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kidogo kuhusu bandari. Tumezungumza sana kuhusu barabara...

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30 malizia sentensi.

**MHE. ANNE K. MALECEL**A: Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kidogo, ahsante. Amenipa dakika mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza sana kuhusu barabara, tunaisahau bandari. Bandari ni kitu kikubwa chenye mambo mengi ambalo ndilo lango la uchumi wa nchi hii, lakini bandari tumekwenda tukaiweka ndani ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Tuwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mfanyabiashara mzuri kama India, lakini mwaka 2020 India ameichukua bandari akaiundia Wizara yake ili aweze kuishika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Sawa Mheshimiwa. Muda wetu umekimbia sana. Ahsante sana. Nimwite sasa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe*, mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Namshukuru Mungu kwa uzima na nafasi. Pia namshukuru

Mheshimiwa Waziri, Eng. Dkt. Leonard Chamuriho, kwa ushirikiano; Naibu Waziri mwenzangu; Makatibu Wakuu wote wawili; familia yangu; na wapiga kura wa Jimbo la Tarime Vijiji; pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, shikamoo. Tumewasikia. Nimekaa hapa, tumesikiliza maoni. Nimewaamkia Waheshimiwa Wabunge, shikamoo tena Waheshimiwa Wabunge. Nawasalimia kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali ni Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, hii ni bajeti yake ya kwanza katika Awamu ya Sita. Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi ndiyo Wizara ambayo alikuwa anaongoza Hayati Dkt. John Pombe Magufili. Kwa hiyo, nilishtuka sana nilipoona Waheshimiwa Wabunge wanataka kupiga sarakasi kwa bajeti ya kwanza ya Mheshimiwa Mama Samia na Wizara ya Hayati Dkt. Magufuli na wengine wakataka kugaragara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaombe, hakuna sababu ya kugaragara, kazi inaendelea. Sisi wasaidizi wa Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Serikali hii ya Awamu ya Sita tunafanya kazi hiyo. Ndiyo maana nikasema shikamooni Waheshimiwa Wabunge na tumewasikia vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa aliwahi kusema, ili Taifa liendelee mambo matatu yanahitajika; la kwanza ni watu. Sisi tupo Waheshimiwa Wabunge na ninyi na Watanzania wengine. La pili, akataka tuwe na uongozi bora. Uongozi bora wa Awamu ya Sita upo, mama Samia ameshika usukani. Pia tunatakiwa tuwe na siasa safi, ndiyo maana hata juzi wakati Mheshimiwa Rais Samia anateua Wakuu wa Mikoa, ameteua na mtu aliyejewa Upinzani, tena

alipambana naye kutaka kuwa Rais wa nchi hii; kwa hiyo, hiyo ni siasa safi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa, mimi ni Naibu Waziri mzoefu kidogo, hii ni Wizara ya tatu; nilikuwa TAMISEMI, nikaenda Muungano, sasa nimekuja Ujenzi. Ukweli ni kwamba wakati Waheshimiwa Wabunge wanachangia hoja, mimi nilikuwa Mbunge wa Ukonga, Mbunge wa mijini. Sasa ni Mbunge wa Tarime Vijiji. Niili kuwa nawasikiliza vizuri kuanzia kwenye utosi mpaka kwenye unyayo wa mguu. Mnachokizungumza, mnataka barabara za majimbo yenu zipitike na kura zetu ziendelee kuwa salama na hasa kwenye uchaguzi ujao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tunayo maelekezo ya chama katika maeneo hayo mahususi kabisa, tunaya fanyie kazi na yote yanaungana mkono na maoni mliyoyatoa hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, kuna Wabunge walijaribu kuhoji hata miradi mingine ya kimkakati. Amiri Jeshi Mkuu, Kiongozi Mkuu wa Serikali, Rais wa Nchi, ameshasema kazi iendelee na amesema ndani ya Ukumbi huu wa Bunge kwamba miradi ya kimkakati, miradi vielelezo ni lazima iendelee. Kwa hiyo, hakuna namna ya kuanza kujadili tena habari ya Daraja la Busisi, habari ya SGR, Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere na miradi mingine ya kimkakati; itaendelea. Rais ameshasema, nani tena apinge katika mazingira hayo? Kwa hiyo, hakuna mjadala mwингine wa hivyo. Sisi kazi yetu ni kutekeleza na kuhakikisha kwamba fedha ya Serikali inasimamiwa vizuri, kazi iende vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mahususi ambazo zimezungumzwa, nataka nijibu baadhi ya maeneo. Kwa mfano, maboresho ya bandari, imezungumzwa hapa. Hata hivyo, tukumbuke Mheshimiwa Rais juzi tu ameteua Mtendaji

Mkuu wa Bandari hii; haya ni maboresho. Tunajua kwamba kuna fedha zimewekezwa kule Tanga, zimewekezwa Bandari ya Mtwara, tumeweka fedha Kigoma; na mabadiliko lazima yafanyike. Mtarajie mabadiliko makubwa katika maeneo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna watu wamezungumza habari ya fidia; Mheshimiwa Kunti Majala amezungumza hapa. Juzi Kamati ya Miundombinu ilikuwa hapa, fedha zimetoka na watu wanalipwa fidia Uwanja wa Ndege wa Msalato, wanalipwa fidia Uwanja wa *ring road* ya hapa Dodoma, fedha zinatoka na mambo yote yanafanyiwa kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Musoma, tunapozungumza Mheshimiwa Mathayo anajua kabisa, fedha zimetengwa; jana na leo na kesho, watu wote watakuwa wamelipwa fidia. Mkandarasi yupo *site*. Tarehe 30, Desemba, 2022 Uwanja wa Ndege wa Musoma utaanza kufanya kazi. Sasa kazi hii inafanyika vizuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, zimezungumzwa hapa barabara. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli Wizara hii inataka kufanya kazi nzuri sana. Wote hapa ni Wanasyansi; Dkt. Chamuriho ni *Engineer*, mimi ni Mwanasyansi hapa, tunajua barabara ni sayansi pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kunti Majala ametaja barabara ambayo ina kilometra 20, wametengewa shilingi bilioni tano za kuanzia, anasema ye ye hahusiki na fedha hiyo; lakini tunataka tujue kwamba kwa kuwa kuna Wabunge hapa kweli hawakupata mgao, haya ndiyo mambo ambayo Mheshimiwa Waziri ameshatuelekeza, tukimaliza tu bajeti hii kesho, sisi hatulali, ni kupitia maoni na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ili wale waliokosa kipindi hiki, bajeti ijayo uwe mjadala tofauti. Hata sisi tungefurahi sana mambo yakienda sawa sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na watendaji pia, baada ya bajeti hii kupidishwa leo, mkitupitishia fedha mkatutuma kazi, hata watendaji wenyewe huko waliko wakae mguu sawa. Haya mambo yote mliyojadili tumechukua, tumeyafanya kazi. Sisi ni wasikivu Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mtuelewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema hivi, yako mambo ambayo sisi tunategemeana sana humu; na hii ni Serikali ya Watanzania; na barabara hizi mnazozungumza; viwanja vyta ndege na maeneo mbalimbali ni vitu ambavyo na sisi pia ni wahusika. Tunataka tusaidiane katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe umezungumza, nami nimesema nitakwenda kwenye barabara yako kule Mbeya na shida ambayo unazungumza na migomo mbalimbali, Mheshimiwa Waziri ataaeleza, tumewasikia vizuri sana. Nataka niwaambie tu kwamba mkipitisha fedha zinazotengwa hapa, sisi bajeti ijayo lazima tuje kuonesha zinafanya kazi zipi na utekelezaji wa miradi. Uzuri ni kwamba miradi yenye mtaiona huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmetupa ushauri, sisi hatatalala. Mimi, Mheshimiwa Waziri, Naibu mwenzangu, watendaji wakuu na kila mtu pale alipo tutafanya kazi ya ziada sana. Tumepewaa mfano hapa wakati wa mchango kwamba tuangalie mchango wa Wizara ya Maji, wamefanya kazi nzuri sana. Tumesema na Mheshimiwa Waziri kwamba kipindi kijacho, Wizara ya Ujenzi itakuwa ni Wizara ya kupigwa mfano kwa sababu ni Wizara ambayo inashikilia uchumi wa nchi hii, inamgusa kila Mbunge, inagusa kila Mtanzania, inagusa kila mkoa, inagusa kila wilaya. Kazi yetu, Mungu ametupa uhai, Mheshimiwa Rais ametuamini; tutachapa kazi kweli kweli. Hapa kazi lazima iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wengine wa Serikali, Watanzania wanataka tufanye kazi; na wanataka wafanye kazi ili hotuba ya

Mheshimiwa Rais nzuri hapa Bungeni lazima itimie kwa vitendo huko kila mwananchi alipo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kunisikiliza, naomba niseme naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, atafuatiwa na mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa hitimisho la hoja ya Mpango na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka huu wa 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho kwa ushirikiano mkubwa anaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Unaibu kwa urahisi. Pia namshukuru Naibu mwenzangu hapa kwa jinsi tunavyoweza kushirikiana katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi niweze kujibu hoja mbalimbali ambazo zimejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo la barabara wameongea kwa hisia kali sana. Ni kweli mahitaji ya barabara na hasa kwa kiwango cha lami, ni makubwa sana. Tukirudi nyuma miaka michache tu, miaka sita, tutakumbuka miundombinu ya barabara ilivyokuwa. Hivyo, tuna kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa awamu zote kwa jinsi ambavyo imekuwa ikifanya vizuri katika sekta

ya miundombinu. Kikubwa tu ni kwamba barabara hizi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba moja ya kigezo kikubwa sana ambacho kimeeingiza Serikali ya Awamu ya Tano na Wabunge wengi kupata kura nyingi sana za kishindo kilichangiwa sana na eneo hili la jinsi Serikali ilivyofanya vizuri katika sekta ya miundombinu ikiwa ni barabara, reli, bandari na viwanja vyatendege. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niende kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imesema nini? Ni kweli kwamba tuna ilani ambayo tunatekeleza, lakini ilani hii inatekelezwa kwa miaka mitano. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025, kilometra ambazo zimeainishwa zitajengwa kwa kiwango cha lami, kwanza zinakamilishwa 1,716, zinazojengwa ni 6,006 kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inayohitajika kukamilisha barabara hizi ni takribani shilingi trillioni 11. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge isingekuwa rahisi barabara zote hizi ambazo zimeainishwa zikapata nafasi kwa kipindi hiki, lakini tukubali kwamba tunatekeleza barabara hizi kwa miaka mitano. Barabara ambazo zitafanyiwa upembuzi yakinifu zina kilometra 7,500; zinahitaji karibu shilingi trillioni 11.5. Kwa hiyo, ukiangalia unaweza ukaona hiyo bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu hoja ya mchangaji mmoja na hasa Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma sasa hivi wana barabara tatu zinazoingia makao makuu. Barabara ya Kigoma – Nyakanazi wakandarasi wote wako *site*. Barabara inayounga Tabora na Kigoma imebaki kipande cha Malagarasi – Uvinza ambacho muda wowote kinaanza kutengenezwa. Pia Mpanda kwenda Kigoma, wakandarasi wapo wanapunguza barabara ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa nadhani ni Mkoa wa Katavi tu na Kigoma ambao wanafika Makao Makuu bila

kupita kwenye lami, lakini wakandarasi wako *site*. Angalau mikoa yote mtu ana uwezo wa kufika Makao Makuu kupitia kwenye lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala lilijitokeza la muda wa barabara. Nitolee mfano barabara ya Dodoma – Iringa; tatizo kubwa ilikuwa, barabara hii ni *traffic projection* ambayo hatukutegemea kama barabara itakuwa na mzigo mkubwa na wingi wa magari kama hayo ambayo yamejitokeza hapo katikati, lakini ndio maana umepunguza muda ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la matuta lilijitokeza. Iko sheria ambayo imetoka, miongozo ambayo pia tunayo ya *SADC* ambao tunashirikiana nao, niwahakikishie Wabunge kwamba tumeendelea kutoa matuta yale ambayo hayakindi vigezo ama hayaendani na huo mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwape *comfort* Waheshimiwa Wabunge kwamba barabara zote ambazo zimeathirika kutokana na mafuriko, tumejipanga; yako madaraja ya muda ambayo tumeyaagiza, tutahakikisha kwamba tunafanya tathmini na kurudishia maeneo yote ambayo yamekatika ikiwa ni pamoja na kuinua matuta sehemu ambazo zimeathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la vigezo vinavyotumika kutengeneza barabara za lami, barabara ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami lazima iwe ni barabara ya ukanda, yaani barabara ambazo zinaunga kwenye ushoroba, ziwe zinaunga mikoa, barabara iwe ni ahadi ya viongozi wa kitaifa kwa maana ya Mheshimiwa Rais, Makamu ama Waziri Mkuu, iwe ipo kwenye Ilani ya Chama Tawala, iwe ni kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano. Pia barabara zinazoenda kwenye eneo la kuchochaea uchumi ambalo ni kama utalii, uzalishaji mali na vitu kama hivyo na vile vile liwe ni eneo la ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba tu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge watupitishie bajeti ili

twende tukatekeleze hiyo mipango ambayo wananchi wanahitaji sana barabara zao zikatengenezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Engineer Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho aje ahitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kufika hatua hii ya mwisho katika kuhitimisha hoja yangu ambayo niliwasilisha jana tarehe 17 Mei na kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ambayo ni kichocheo cha ufanisi wa utendaji wa sekta zingine za kiuchumi na kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo yake ambayo imenisaidia wakati nikitimiza majukumu ya Serikali katika kipindi hiki kifupi kutoka ateuliwe kuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia usoefu wake wa uongozi katika kutuongoza kwa umahiri na kimkakati kutekeleza majukumu yetu kila siku hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Spika na pia kukushukuru wewe binafsi Naibu Spika na Wenyeviti wa Wabunge kwa ushirikiano mnaopatia Wizara hii ninayoiongoza katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya Serikali ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wao wa dhati wanaonipatia kutoka nilipoteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, nimejifunza masuala mengi kutoka kwao, ujuzi ambao utaniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa sasa kwa kiwango cha hali ya juu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso pamoja na Wajumbe wa Kamati yake ambao wamepitia bajeti ya Wizara kwa niaba ya Bunge lako Tukufu na kuanisha namna bora ya kiutendaji kazi kufikia malengo ya Taifa letu. Naahidi kwamba Wizara itazingatia maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati hii kwa weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru Mheshimiwa *Engineer Godfrey Msongwe Kasekenya* na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara pamoja na Makatibu Wakuu Mhandisi Joseph Christopher Mwalongo na Gabriel Joseph Migile wa Ujenzi na Uchukuzi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Vitengo, Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara, Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano mzuri na juhudhi walizozifanya kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba, Wizara ninayoismamia itatimiza matarajio ya Serikali na kuhakikisha kazi inaendelea. Mimi kama waziri mwenye dhamana nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na weledi wa hali ya

juu kwa kushirikiana na wenzangu katika Wizara yangu. Ni imani yangu tutafikia matarajio ya Taifa ikiwa ni pamoja na yale ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, michango ambayo itanisaidia sana katika kuboresha hoja niliyoiwasilisha. Naomba sasa nijielekeze katika kutoa maelezo kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika bajeti yangu. Waheshimiwa Wabunge 59 waliochangia wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu na Waheshimiwa 158 wamechangia wakati wa hoja ya Wizara yangu ambapo 84 wamechangia kwa kuzungumza na 14 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi punde Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wa Wizara yangu wameanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana kwa jinsi ambavyo wamejibu baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hoja hiyo niliyoitoa hapa Bungeni wakati nawasilisha hapo jana, hoja kuhusu mpango wa bajeti wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na kuziwasilisha kwao kabla ya kuhitimisha kwa Mkutano wa Bunge hili la Bajeti unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufanuzi wa kijumla wa baadhi ya hoja zilizojitokeza. Bajeti ya Wizara imejikita katika kutengeneza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia 2021/2022 hadi 2025/2026, Ilani ya Uchaguzi wa

Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera, Mikakati na Miongozo Mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Maendeleo pamoja na Ilani ya Uchaguzi zina lengo kuu la kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Wizara ninayoiongoza ina jukumu kuu la kuwezesha kufikiwa kwa lengo hili kwa kuwa inawezesha sekta nyingine kufikia malengo yao ikiwa ni pamoja na kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko. Hii ina maana kwamba ufanisi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi utawezesha Sekta nyingine za uchumi na kijamii kuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi wa mwaka 2020 Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi wa kishindo ngazi ya Urais, Wabunge na Madiwani. Hii ilitokana na ubora wa Ilani yake ya Uchaguzi ambayo kiumla inalenga kujenga uchumi imara na kuwawezesha wananchi kunufaika nayo ikiwa ni pamoja na kuondoa kila aina ya kero za wananchi kuliko ilivyokuwa kwa Ilani nyingine. Kwa kuzingatia hili nina wajibu wa kueleza vitu ambavyo Wizara ninayoiongoza itatekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia 2021/2022 hadi 2025/2026 tukianza na mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameitaka Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati iliyoanza kutekelezwa kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, kwa kuwa miradi ndiyo msingi wa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Miradi hiyo ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa ukarabati wa barabara kuu za mikoa ili kuiunganisha nchi, ujenzi wa madaraja ya muhimu ya barabara na vivuko, kuendelea na ujenzi wa reli ya *Standard Gauge*, uboreshaji na upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na kuendelea na ujenzi wa ukarabati wa meli katika maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabitii wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhamiria kuendelea kutekeleza miradi yote ya kimkakati ili Taifa liweze kunufaika nayo kwa kujenga uchumi endelevu. Miradi hiyo inatekelezwa na Wizara yangu kama ilivyoanishwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa umakini na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mazuri tunayoyaona, lakini tumedhamiria kazi iendelee ili mazuri zaidi yaje kuonekana ifikapo mwaka 2025. Serikali zilizopita za Chama cha Mapinduzi zilijiwekea dhamira ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote nchini kwa barabara kuu za lami. Dhamira hii inakaribila kufikiwa ambapo kwa uchache kwa nchi ambapo kazi inaendelea. Kazi hizo zinahusisha ujenzi wa barabara za kuunganisha Mikoa ya Tabora na Kigoma, Mikoa ya Kigoma na Kagera, Mikoa ya Tabora na Mbeya. Aidha, maeneo mengine ni pamoja na kuunganisha na Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Morogoro ambao utapewa kipaumbele ndani ya kipindi hiki cha utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na wasaidizi wangu tutakuwa karibu sana, karibu sana na mahali pa kazi za ujenzi wa barabara zinazofanyika ili kuhakikisha zinafanyika kwa ubora kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge. Ningependa kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari tunatangaza miradi 16 ya barabara ambayo tumeanza kuitangaza wiki hii, ambayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kwanza, ni Barabara ya Ntendo hadi Muze kilometra 25; Barabara ya Isonje hadi Makete kilometra 25; Barabara ya Mianzini hadi Ngaramtoni kilometra 18; Barabara ya Bigwa – Kisaki kilometra 15; Barabara ya Uvinza – Malagarasi kilometra 51.1; Barabara ya Mbulu – Hydom kilometra 25; Barabara ya Matai – Kasesya kilometra 25; Barabara ya Ntyuka Junction – Mvumi Hospital

hadi Kikombo Junction kilometa 25; Barabara ya Tarime - Mgumu kilometa 25; Barabara ya Vikonje hadi Uvinza kilometa 25; Barabara ya Kibondo hadi Mabamba kilometa 10; Barabara ya Noranga – Itigi hadi Mkiwa kilometa 25; Barabara ya Itoni hadi Lusitu kilometa 50; Barabara ya Handeni hadi Kibereshi kilometa 20; Barabara ya Kitai hadi Litai kilometa 35; na Barabara ya Kibaoni hadi Stalike kilometa 50. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Bunge lako Tukufu wataona kwamba kazi inaendelea na tunaendelea kuZitendea haki barabara kama ambavyo zimepangwa katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja vya Ndege vina uhusiano wa karibu sana na huduma za usafiri kwa njia ya anga. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na kwenye Bunge hili la bajeti wameainisha umuhimu wa usafiri wa njia ya anga. Kiutalam ndege inatakiwa kuwa angani kwa wastani wa masaa 12 hadi 15 katika saa 24 za siku, hiki ni kigezo kimoja muhimu cha matumizi sahihi ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nchi yetu ina urefu wa zaidi ya kilometa 1,200 Mashariki hadi Magharibi na zaidi ya kilometa zaidi 1,700 kutoka Kaskazini Magharibi hadi Kusini Mashariki. Umbali huu ni stahiki sana kwa matumizi ya usafiri wa njia ya anga, hata hivyo ni viwanja vile tu, vya Julius Nyerere *International Airport*, Kilimanjaro *International Airport*, Mwanza na Dodoma ambavyo kwa sasa vinaweza kutumika kwa saa 24 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Shirika letu la Ndege linufaike na uwepo wa viwanja hivi vya ndege, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itawekeza vifaa muhimu vyenye kukidhi mahitaji ya utoaji huduma wa ATCL ikijumuisha taa za kuongoza ndege kwenye viwanja vya kimkakati kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022. Viwanja ambavyo vipo kwenye mpango huo ni Uwanja wa Ndege

wa Kigoma, Uwanja wa Ndege wa Mbeya, Uwanja wa Ndege wa Mtwara, Uwanja wa Ndege wa Bukoba na Uwanja wa Ndege wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Viwanja vyatya Ndege vyatya Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Songea na Iringa navyo wakati wa ukarabati wake vitafanyiwa utaratibu wa kuwekewa taa za kuongozea ndege. Ukamilishaji wa mradi huo wa kuweka taa za kuongozea ndege kwenye viwanja vyatya ndege utaongeza ufanisi kiutendaji kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (*ATCL*). Maelekezo yangu ni kwamba kabla ya mwisho wa mwaka wa 2021 Mamlaka ya Viwanja vyatya Ndege, *TANROADSna ATCL* zikutane ili kujipanga kufikiwa kwa lengo hili mahsusii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nydingi duniani zilizopiga hatua kubwa za kimaendeleo zimefanya hivyo kutokana na sababu kadhaa mojawapo ikiwepo ni kuwepo na huduma za reli zenye uhakika, gharama nafuu na salama. Kwa kulitambua hilo moja ya vipaumbele kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 ni kuendelea na ujenzi wa reli ya *SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge hili Tukufu kwamba tutaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa vipande viwili vyatya reli vyatya *SGR* ambavyo ni Dar es Salaam hadi Morogoro kilometra 300, ambapo kwa sasa imefikia asilimia 91 na kipande cha Morogoro hadi Makutupora kilometra 422 kilichofikia asilimia 60.2 ya ujenzi na kipande cha Mwanza hadi Isaka kilometra 341 ambacho kwa sasa Mkandarasi yupo katika hatua za awali ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea na kipaumbele cha kutafuta fedha za ujenzi wa reli ya *SGR* kwa vipande vitatu vyatya Makutupora hadi Tabora kilometra 294, Tabora hadi Isaka kilometra 133 na kile cha Tabora hadi Kigoma kilometra 411.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishwaji wa reli hizi utaziingizia Taifa kipato kikubwa cha fedha za kigeni kutokana na kusafirisha mizigo ya nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kwa sasa wataalam wanakamilisha taratibu za kuanza kumtafuta mkandarasi wa kujenga kipande cha Uvinza hadi Msongati kwa ajili ya kubeba tani milioni tatu kwa mwaka za mizigo ya kwenda na kutoka Burundi hadi Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango itafanya kazi ushauri wa Waheshimiwa Wabunge katika kutumia mbinu mbalimbali za kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vipande vilivyobaki kwenye mtandao wa *Standard Gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wowote unatakiwa kuwa na vigezo vikuu vitatu; uhakika, gharama nafuu na usalama. Kwa upande wangu nitalisimamia kwa umakini suala la usalama wa usafirishaji na usafiri, nitaendelea kuhakikisha kwamba matumizi bora ya TEHAMA katika kuboresha huduma za uchukuzi unafanyika. Aidha, changamoto katika matumizi ya mifumo ya ufuutiliaji wa mabasi na tiketi za kielektroniki zitafanyiwa kazi kwa karibu na kushirikisha wadau wote hususani wasafirishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taasisi za mafunzo Sekta ya Uchukuzi nchini itazidi kuboreshwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ukuaji huo, ukuaji wa mahitaji ya wataalam wenye weledi wa kusimamia na kuendesha miundombinu na huduma za uchukuzi yanazidi kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hili Wizara itazidi kuboresha vyuo vya mafunzo ili viweze kuzalisha watalaam wenye weledi unaotakiwa kukidhi haja hii. Aidha, tutafanya jitihada za makusudi kukamilisha uanzishwaji wa Bodi ya Watalaamu wa *Logistic* na Usafirishaji ili watalaam wa sekta ya uchukuzi waweze kusimamiwa vizuri na sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha, ningependa kuongelea hoja mahsus ambazo zimetolewa na Wabunge, kwanza nikianza na hoja ya daraja la *JPM* ambalo tuliambiwa lina changamoto kwamba kuna mkandarasi ambaye hawajibiki vizuri, lakini ukweli ni kwamba mkandarasi yule ameahidi kuchangia huduma kwa jamii, kwa Kijiji cha Bukumbi kwa kuchangia milioni 50 na analipa mrabaha wa kila tripu ya kokoto kwa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na hadi hivi sasa amekwishalipa jumla ya milioni 20. Vilevile mkandarasi huyo ameajiri wakandarasi wazawa wanane ambao wanamsaidia katika kazi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wazawa ambao wameajiriwa katika shirika lile wanafikia asilimia 90, kwani kuna wafanyakazi 274 ambao ni wa Kitanzania kati ya wafanyakazi 350 ambao wanafanya kazi pale. Mnamo tarehe 12 Januari mwaka huu nilitembelea daraja lile na taarifa hizi nilizipata pale mimi mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *ATCL* tayari tunafanya kila tunaloliweza kuhakikisha kwamba mifumo ambayo inafanya kazi pale hairuhusu watu kufanya hujuma za kujaza ndege bila sisi wenyewe kutarajia. Mifumo ile hairuhusu kukata tiketi kama ndege imeja lakini kuna *station* ambazo zina adhabu ya kuwa haziwezi kujaza ndege, vituo hivyo ni kama Bukoba, Songea, Mbeya na Iringa ambapo kiutalaam huwezi kujaza ile ndege na ukaondoka nayo kwa usalama, hivyo huwa hajjai na pengine wananchi hudhani kwamba ndege ile imeachwa bila kujaa kwa makusudi, lakini siyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri umetolewa kuhusu viwanja vya ndege, ujenzi wake, tutakwenda kulifanyia kazi hilo, kwamba kuangalia ni wapi waendelee kuvijenga ni *TAA* au *TANROADS* kulingana na ushauri ambao Wabunge wametupatia. Vilevile zile *bypasses* katika Miji ya Mbeya, Songea, Dodoma, Mwanza na Arusha na Iringa tutakwenda kuzifanyia kazi ili tuweze kuendana na ushauri wa Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa rasilimali vilevile utazingatiwa kulingana na ushauri walioutoa Wabunge hapa Bungeni na hakutakuwa na tashiwishi katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeongelewa vilevile ucheleweshaji wa kutolewa *GN* kwa ajili ya barabara mbalimbali. Hili suala nalo tunaenda kulifanyia kazi tayari, tumekwishaongea na wenzetu wa Wizara ya Fedha na umeandalialiwa mpango maalum ambao utahakikisha kwamba hizi *GN* za misamaha ya kodi zinatolewa mapema ili tuweze kuharakisha katika mijengo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, mwisho ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe hoja yangu kwa kuwa tunataka kusimamia kwa niaba ya wananchi wote utekelezaji wa maendeleo na ya llani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 pamoja na mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Tatu wa mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyenzo ya kutuwezesha sisi pamoja na watumishi wenzetu katika Wizara hii ni bajeti hii na kupitia kwake Serikali itafanya kila iwezekanalo kuhakikisha kwamba, miundombinu ya sekta ya ujenzi na uchukuzi na huduma zake zinaboreshw na kulingana na matakwa ya sasa na miaka ijayo. Hivyo, kwa niaba ya wenzangu katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na kwa niaba yangu mwenyewe ninaomba sana bajeti hii ipitishwe ili kazi iendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja zingine ambazo zimetolewa na Wabunge zote tutazizingatia kwa mfano hii ya viwanja vinne ambavyo ni viwanja vya Sumbawanga, Kigoma, Tabora na Shinyanga ambavyo vina ufadhilli wa benki ya *EIB* tunakwenda kumalizia maongezi nao ili tuweze kuhakikisha kwamba vile vikwazo ambavyo vilikuwepo tunaviondoa vyote na viwanja hivi vinaanza kujengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa reli yetu ya *TAZARA* ambayo imeonekana ni kiungo muhimu kwa nyanda

za juu, tayari tuna mpango wa *open access* ambao tunaruhusu watu binafsi kuendelea na kupitisha mizigo yao pale. Tayari kuna kampuni moja ambayo inaitwa Calabash inafanya kazi hiyo na tayari tumetoa zabuni ambapo wauzaji wawili wa kizawa wako tayari kujiunga pale na kuweka treni zao binafsi ili ziweze kusaidia katika kuendesha pale *TAZARA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile tunaendelea na ukarabati wa reli ya *TAZARA* ili kuhakikisha kwamba reli hiyo inatoa huduma nzuri katika mikoa ya nyanda za juu na kote inakopita.

Vilevile, tunalipa madeni ya *TAZARA* hasa ukizingatia kwamba tunatao ruzuku ya mishahara kwa wafanyakazi wa *TAZARA* ili tuweze kuhakikisha kwamba *TAZARA* yetu inaendelea. La mwisho kwa *TAZARA* tunamalizia marekebisho ya sheria mpya ili tuweze kuboresha uwekezaji ndani ya *TAZARA* lakini vile vile tuwezeshe kuruhusu mambo ambayo yataongeza tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge. Tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI** Waheshimiwa tukae, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

## KITABU CHA PILI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### FUNGU 62 – WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (UCHUKUZI)

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*... ... Sh. 3,390,761,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kifungu hiki ndio kina mshahara wa Waziri na Waheshimiwa mbalimbali wameomba fursa hapa ya kutaka ufanuzi wa mambo ya kisera. Sasa nikawa naijuliza kwa majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri sijui kama bado kuna watu wanataka ufanuzi, lakini majina yako hapa. Mheshimiwa Reuben Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana jambo moja la kisera ambalo nahitaji ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri ni kwamba uelekeo wa Serikali ni kuunganisha mkoa na mkoa kwa lami. Mkoa wa Tanga haujaunganishwa na Mkoa wa Manyara na haujaunganishwa na Mkoa wa Morogoro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara hii ya Handeni – Kibilashi – Kiteto – Singida inaunganisha mikoa minne, fedha inayotengwa hapa ni bilioni 4 na wanasema wanaanza na kilometra 20. Kwenye hii bilioni 4 kuna barabara tatu ukiacha ile ya Handeni – Kibilashi – Singida kuna barabara ya Kongwa – Kibaya – Arusha na kuna barabara ya Singida – Sepuka – Ndago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kiasi gani cha fedha kitakachowezesha kujenga hizi kilometra 20 kwa mwaka huu wa fedha? Naomba ufanuzi wa hilo jambo na Mheshimiwa Waziri kwa kweli asiponipa ufanuzi wa kuridhisha nitashika shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa uafanuzi kwa Mheshimiwa Reuben Kwagilwa kwa hizi barabara zake za kuunga Tanga na Mkoa wa Manyara na Mkoa wa Morogoro kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi ambacho kimetengwa pale ni kianzio kwa sababu barabara hizi zitajengwa kwa awamu hazitajengwa kwa mwaka mmoja hivyo, hicho kiwango ambacho kimeingia pale bilioni 4 tunaanza nacho baada ya hapo tunaendelea kwa sababu ni azma ya Serikali kuunga mikoa hii kwa lami na ndicho ambacho tutakwenda kufanya. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa naona umesimama.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri ninakubaliana naye kwamba, atashughulikia jambo hili *sensitive* la barabara ya kiuchumi inayounga mikoa minne. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakumbuka Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, mama yetu mama Samia Suluhu Hassan alipofanya mabadiliko ya uongozi bandari alitoa maelekezo na kuipa mamlaka yetu ya bandari na uongozi mpya miezi sita kuhakikisha wanafanya mabadiliko ya kuimarisha utendaji wenye kuleta tija kwa bandari zetu na hasa bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nisikie *commitment* ya Serikali uongozi uliopo bandarini ni kusudi la kikatiba kabisa la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuisimamia Serikali. Na moja ya kazi ya kuisimamia Serikali ni kuhakikisha

miongoni mwa mambo na matamko yanayotolewa na Rais yanatekelezwa kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nikupe taarifa na Waziri ninahitaji nipate *commitment* fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimekuwa zikitolewa na Serikali kuhakikisha bandari inafanikiwa kufanya kazi kwa tija pamekuwepo na ninaushahidi nikiambiwa nilete ushahidi...

**MWENYEKITI:** Hebu ngoja kwanza kengele imegonga hapa, najaribu kuelewa hoja yako ni nini kwa sababu kama ni hoja ya bandari umeshasema Rais katoa miezi sita, hata mwezi mmoja bado hoja yako ni nini unayotaka ufanuzi?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ninayotaka ufanuzi ni kwamba, Serikali imekuwa haipeleki fedha za miradi ya maendeleo kwa upande wa bandari. Ninataka nipate kauli ya Waziri nini *commitment* ya Serikali katika kupeleka fedha za miradi ya maendeleo katika suala zima la uendeshaji wa bandari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu nahitaji tena ufanuzi kwasababu bandari ya Dar es Salaam juzi ameenda Waziri Mkuu, tumeona pale sijui vinaitwaje vile, sijui ni vijiko, sijui vitu gani vinapishana kwamba kuna mambo yanafanyika. Sasa usipoliweka vizuri kwenye hoja yako yaani unataka Waziri ajibie lipi? Unaweza kutaja mifano miwili mitatu ya bandari ambazo hajijapelekewa hiyo fedha ya maendeleo ili sasa Waziri ajue anajibu hoja ipi?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema fedha za miradi ya maendeleo nina imani Waziri amenielewa.

**MWENYEKITI:** Mimi natakiwa nikuelewe ili nimpe Waziri fursa mimi hapa maana mimi ndio inabidi nimuite ili asimame kwa hiyo, nieleweshe mimi ili nielewe njue yule akiieleza nimeelewa au sijaelewa kwa hiyo nieleweshe mimi ninayetakiwa kumsimamisha Waziri.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba bandari palikuwepo na changamoto ambazo zimepelekea Rais kufanya mabadiliko ya kiuongozi na mabadiliko haya ya kiuongozi ambayo kimsingi ninayasema Rais alipota miezi sita, miezi sita hii tunaweza tukasema kwamba maelekezo aliyotoa Rais yasifanikiwe kwa sababu kuna fedha za miradi ya maendeleo na ninajua ninalizungumza hili sio lazima nitaje *in details* lakini Waziri anajua kuna...

**MWENYEKITI:** Sawa umeeleweka Mheshimiwa, kaa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Kingu ni ya msingi sana lakini kwa sababu hoja yake inahusianisha na utendaji wa bandari kwamba, bandari haifanyi vizuri kwa sababu hizo ambazo yeye ameona ngoja akae nazo hana haja ya kusema. Kwa sababu hiyo ile miezi sita ambayo ameitoa Rais maadam hajaisha Mheshimiwa Kingu tuipe fursa Wizara ikafanye hiyo kazi yake na kule bandari wafanye kazi hiyo miezi sita, halafu kwa sababu Bunge linaendelea kukutana kutana tutapata fursa ya kujua Serikali imefikia wapi baada ya miezi sita. Mheshimiwa Joseph Kakunda. (*Makofii*)

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nina hoja ya msingi kabisa ya kuiuliza Serikali itoe ufanuzi wa kina na nisiporidhika itabidi kwa kweli nichukue shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya barabara na tozo ya mafuta ya mwaka 2006 na sheria ya barabara ya mwaka 2007 na sheria ya wakala wa Serikali *Executive Agencies Act* ya mwaka 1997 iliyoanzisha *TARURA* zote hizo zinatambua barabara za Kitaifa, barabara za mikoa, barabara zinazouganisha wilaya, barabara za kata, za mitaa na vijiji. Lakini hazitambui barabara ambazo zinatakiwa kuunganisha vitongoji ambavyo tuna vitongoji zaidi ya 64,000 hizi

hazitambuliwi na sheria hizo nilizozitaja. Atoe ufanuzi lini Serikali italeta marekebisho ya sheria hapa ili *ku-include* vitongoji navyo vipate barabara kwa mujibu wa sheria? Asipota ufanuzi wa kina hapa nakusudia kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Kwa kweli nimemuelewa yule Mbunge ambaye alikuwa anazungumza hapa watu wanahitaji barabara za vitongoji, wengine za mikoa, wengine za wilaya haya barabara za vitongoji Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa kwa hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Joseph Kakunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kakunda inahusisha kubadilisha sheria na hoja ya kubadilisha sheria ina mchakato mrefu, kwa hiyo tumepokea hiyo hoja yake ambayo inatutaka tuangalie uwezekano wa kutambua barabara zaidi ya zile barabara ambazo zinatambulika katika sheria zetu. Kwa hiyo, ikafanyiwe mchakato kulingana na utaratibu ule ule wa kawaida ambao unaishia kwenye maoni ya wadau, ambao Mheshimiwa Kakunda naye atakuwa mmojawapo wa wadau. Halafu tukimaliza hilo sasa hayo matokeo yake ndio tutayakusanya pamoja ikitajiji kuwekwa, tutaitleta hapa kwenye Bunge lako Tukufu tufanyie kazi, ikisema vinginevyo itakuwa ndio hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kakunda nadhani ufanuzi wa utengenezaji wa sheria uko hivyo. Naona umesimama?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tu kumshukuru kwa maelezo mazuri ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba

nipate ufanuzi kupitia suala la kisera juu ya suala la vivuko. Kumekuwa na baadhi ya maeneo ambayo yana changamoto kubwa sana ya vivuko kiasi ambachoo yamekuwa yakisababisha maafa makubwa sana kwa wananchi. Nitataja tu baadhi ya vivuko, kivuko cha Mto Malagarasi Kigoma, Kivuko cha Mto Ruvuma katika kivuko hicho kivuko kinachoitwa Limonga, Mkenda, Mitomoni lakini pia kivuko cha Sasawala Mozambique, kivuko cha Same, kivuko cha Kalemawe Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napenda nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na niseme tu kama ufanuzi ambao atakaonipa hautaniridhisha maana yake patachimbika nakusudia kuondoa shilingi ya mshahara wake. Kwa hiyo, niombe sasa anipe ufanuzi kwenye hivi vivuko hasa kivuko hiki cha Limonga, ni lini pesa zitapelekwa kwa ajili ya kujenga kivuko? ili wananchi hawa wasiendelee kupoteza maisha katika eneo hilo kwa sababu wananchi zaidi ya 12 wamekufa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, kengele imegonga.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufanuzi wa vivuko vyote kwa ujumla.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufanuzi kuhusu vivuko vyote hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika hotuba yangu ya Wizara imeelezea vizuri mpango wetu wa vivuko ambao umetamka bayana ni sehemu gani tutavipeleka vivuko na kwa sababu gani. Sasa, kwa sababu, kuna haja ya kupatiwa vivuko vingine sehemu nyingine ambazo zimeonekana zina haja, tutaendelea na huo upembuzi tufahamu mahitaji mengine ambapo kote kunakohitajika vivuko na tutawapatia vivuko. Kama ulivyoona katika bajeti

mwaka huu tutajenga vivuko vitano, kwa hiyo tukiona kuna haja ya kujenga vivuko vingine pamoja na huko ambako umekutaja vivuko vitawekwa kama ambavyo mahitaji yatahitajika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline naona umesimama.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni bajeti yake ya kwanza basi naomba nimpe fursa hii ili aweze kufanya kazi vizuri. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana, Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nisiporidhika na maelezo ya Waziri nakusudia kushika shilingi. Asilimia kumi tu ya wakandarasi walioko nchini ni wakandarasi wa nje ukilinganisha na asilimia 90 ambaa ni wa ndani. Lakini hawa asilimia 10 ndio wanaochukua asilimia 60 ya kazi zote za ukandarasi nchini na changamoto kubwa inayowafanya wakandarasi wetu kushindwa kufanya kazi za ukandarasi ni ukosefu wa mitaji wakiungana waweze kufanya kazi masharti ya kupata kazi au tender yako juu sana. Kwa mfano, wanatakiwa kuweka *bank guarantee* hawa ambaa wameungana ili waweze kupewa tender. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ma-director wanaenda *ku-mortgage* nyumba zao wakifanikiwa kupata hiso *tender* hawapewi malipo yao kwa wakati, kuna changamoto ya kupewa *VAT exemption* kwa wakati wanaambiwa *GN* haijatoka.

Kuna changamoto hasa kwenye hii miradi ambayo ni *donor funded projects* wanapeleka *certificate* ya kufanya kazi kwenye Wizara ya Ujenzi, wakitoka pale Hazina nao kwa sababu ndio wameingia mkataba na yule *donor*, Hazina nayo inataka *i-review* ule mkataba, jambo ambalo linachukua muda mrefu na kuwafanya hawa watu wawe frustrated na kushindwa kufanya biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Waziri kwenye hotuba yake kwamba, wamejitetahidi kuwawezesha wakandarasi na Mheshimiwa Rais Marehemu alijitetahidi kukaa na wakandarasi lakini bado changamoto ya kuwawezesha wakandarasi wetu iko pale pale. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *primary function* ya Wizara ya Ujenzi ni kuwawezesha wakandarasi wazawa, nataka kujua wanawezaje kutatua changamoto ili wakandarasi wetu wa ndani waweze kupata *tender*, pesa ambazo watakazozipata zizunguke kwenye mzunguko wa uchumi wa Tanzania na hili deni ambalo tunaambiwa ni 14. *Something billions* ya CAG. (Makof)

**MWENYEKITI:** Haya ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufanuzi malipo kwa wakandarasi wa ndani.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Salome Makamba kwa kuonyesha uzalendo wake wa kuwatetea wakandarasi wa ndani ambao ni asilimia 90 lakini wanapata kazi asilimia 40. Jambo hili tunalifahamu na sisi tunalifanyia kazi sana na kwa bahati nzuri hili nimelifanyia kazi kwa miaka 10 sasa kwani vile vile na mimi ni mtaalam wa ujenzi kwa hiyo nimelifundisha na ni changamoto ambayo tumeiona na tunajua *solution* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayojitokeza hapa kwa wakandarasi wazawa ni kama uliyosema kweli ni uwezo wao mdogo lakini hilo tumelifanyia utaratibu tumewawekea kozi za aina tatu. Kozi za *small contractors*, *medium contractors* na *large contractors*, ili waweze kujiongeza ule weledi wao wa kuweza kupambana katika hizi *tender*. Lakini kwenye changamoto ya pili ambayo ni ya

kifedha ambayo huwa wanakutana nayo mara wanapoenda kwenye *bidding*, kuna changamoto ya kwanza ni ya kupata *bid bonds* ambayo zinawasumbua hiyo tumeweza kuwatengenezea *contractors assisted funds* ili waweze kukua nayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakishapata hiyo *tender* changamoto ya pili wanakuja kwenye *advance payment bond* na *performance bond* hilo nalo limekuwa ni changamoto. Kwa hiyo, sasa hivi tunafanya mkakati wa kuongea na mabenki ili wakandarasi wanapopata mikataba ile, mikataba ile itumike kama dhamana ili waweze kuaminika na waweze kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili tunalifahamu na tuko mbioni kulikamilisha na hivi punde changamoto hili itaondoka na wakandarasi wetu wataweza *ku-participate* zaidi katika miradi mikubwa. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Salome ameelewa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mikataba ambayo ukipeleka benki sasa hivi haidhaminiki ni hii mikataba ya kandarasi za Serikali.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Salome, umeeleza hoja sasa hivi unasema mikataba ambayo haiaminiki benki na hoja hiyo ndiyo ametoka kusema hapa kwamba wanaongea na mabenki ili waweze kutengeneza sasa utaratibu mzuri wa kutoa hiyo mikataba. Sasa ni maelezo gani tena ya ziada unataka Mheshimiwa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utanielekeza kama nakosea.

**MWENYEKITI:** Haya toa hoja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja anayoisema Mheshimiwa Waziri wameshaifanya *for the*

*past ten years.* Naomba nitoe hoja ili Wabunge wenzangu waweze kuniunga mkono na kufafanua vizuri kuhusiana na hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono lakini muda wetu umekwenda tunakwenda *guillotine*. Katibu. (*Makofi/Kicheko*)

### **FUNGU 62 – WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (UCHUKUZI)**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i> .....	Sh.3,390,761,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.725,951,000
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.1,865,283,000
Kifungu 1004 - <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.281,848,000
Kifungu 1005 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh.535,911,000
Kifungu 1006 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.354,685,000
Kifungu 1007 - <i>Legal Services Unit</i> .....	Sh.407,580,000
Kifungu 1008 - <i>Information and Communication Technology Unit</i> .....	Sh.414,774,000
Kifungu 2005 - <i>Transport Infrastructure Division</i> .....	Sh.1,398,623,000
Kifungu 2006 - <i>Transport Services Division</i> .....	Sh.81,403,738,000
Kifungu 5002 – <i>Trans. Safety and Environment Division</i> .....	Sh.964,257,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **FUNGU 98 – WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (UJENZI)**

Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.2,092,858,800
---	------------------

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..... Sh.722,797,900  
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*.... Sh.548,329,600  
Kifungu 1004 - *Government Communication  
Unit*.....Sh.166,873,600  
Kifungu 1005 - *Procurement Management  
Unit*.....Sh.236,457,800  
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.....Sh.249,164,500  
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*.....Sh.200,670,500  
Kifungu 1008 - *Information and Communication  
Technology Unit*.....Sh.166,332,500  
Kifungu 2002 - *Technical Services Division*..... Sh.14,118,253,800  
Kifungu 2005 - *Roads Division*.....Sh.19,471,646,500  
Kifungu 5002 - *Safety and Environment Unit*.....Sh.312,165,100  
Kifungu 6001 - *Airport Construction Unit*..... Sh.255,236,400

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **KITABU CHA NNE**

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 62 – WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (UCHUKUZI)**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit* ... Sh.216,223,319,440  
Kifungu 2005 - *Transport Infrastructure  
Division*... .... .... .... .... ..Sh.1,191,806,410,000  
Kifungu 2006 - *Transport Services Division*... Sh. 620,276,680,560

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **FUNGU 98 – WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI (UJENZI)**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*.....Sh.318,680,000  
Kifungu 2002 - *Technical Services Division*... Sh.84,913,214,000  
Kifungu 2005 - *Roads Division*.....Sh.1,406,271,346,200  
Kifungu 5002 - *Safety and Environment Unit*.... Sh.2,077,134,000  
Kifungu 6001 - *Airport Construction Unit*.....Sh.95,123,113,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja, taarifa.

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 123(3)(a) na (b), naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako lillikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofii)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofii)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa kwa utaratibu wetu tulionao nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kwa niaba yetu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri lakini

pia Naibu Mawaziri kwa bajeti hii waliyoileta kwa maana ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Watendaji wao wote. Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wamesikia mawazo ya Wabunge, hoja za Wabunge na matatizo yaliyoko majimboni kwa Wabunge. Bunge hili limeidhinisha fedha kama mlivyoomba, hakuna hata shilingi imetoka, yale ambayo mmeyaahidi kwenye bajeti hii tunaamini mtakwenda kuyatekeleza na tunawatakia kila kheri katika utekelezaji huo. (*Makof*)

Nafikiri katika hizi siku mbili zimewapa picha ninyi, Waziri na Naibu Mawaziri lakini pia na watendaji wenu kwamba miundombinu ya nchi hii tunatamani iwe bora zaidi kuliko ilivyo sasa. Ili nchi yetu tuseme inaendelea basi tunatamani tuone mabadiliko kwenye eneo la miundombinu. Walivyokuwa wanasiifia bajeti yako ni kwamba wanatambua kazi kubwa ambayo imeshafanywa na Serikali sehemu mbalimbali. Hata hivyo, hiyo peke yake haitoshelezi kama kuna maeneo ambayo hayajafikiwa, hawezi kusimama mtu hapa akasema natambua, natambua, kwa hiyo, nafikiri hiyo imekupa picha. (*Makof*)

Pia Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wako, wote tunatambua kwamba ndiyo kwanza mmenza, hii ni bajeti ya kwanza kwa maana ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano lakini pia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanapozungumza haimaanishi wao hawajui huu ni mwaka wa kwanza, wanajua ni mwaka wa kwanza, lakini wanataka mwaka wa kwanza huu utambue kwamba huko unakokwenda wana changamoto nyingi majimboni kwao kwa hiyo lazima uzitazame. (*Makof*)

Nadhani hoja zote zilizotolewa mlikuwepo hapa mmezisikia. Ni vizuri kama Wizara myatazame haya mambo kwa ujumla wake, kuliko kupeleka kila mahali kadogo kadogo halafu kila siku kadogo kadogo miaka 20, miaka mingapi, ni afadhalii Waheshimiwa Wabunge hawa wawe wanapata hiyo picha pana katika miaka mitano mtafika sehemu ngapi na mtaanza na ipi ili iwe rahisi. Ndio maana mtu akisimama

hana anashangaa katika kilometra 200 akipewa moja anawaza sasa tutazifika saa ngapi hizo 200 lakini angeangalia ule mpango mzima angepata picha kwamba suala la miundombinu kwake litafikiwa lini. Namuona hapa Mbunge wa Liwale ananiangalia kama nizungumzie Liwale lakini sasa nadhani walishakusikia kuhusu hoja za Liwale. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hiyo kwamba hii ni bajeti ya kwanza basi tuendelee kuwaushuri Wizara hii ili ifikie yale maeneo ambayo tunaona yana changamoto kubwa zaidi pengine waanze na hayo halafu tutaendelea kwa sababu nchi yetu hii ipo, ilianza na itaendelea. Hata zile sehemu zinazohitaji maboresho si kwamba Wabunge sasa ndiyo wanataka kule kusimame kabisa kwa sababu sasa kuja kujenga upya itakuwa ni gharama zaidi kwa Serikali. Kwa hiyo, tunayatambua hayo yote lakini ni dhahiri mmezielewa vizuri hoja za Wabunge kwamba wanatamani maeneo yao pia yafikiwe. (*Makofii*)

Jambo la msingi, Wabunge wengi wakati mwingine wakichangia wanazungumzia 2025 kama atarudi ama hatarudi lakini yale ni maneno wakati wa uchangiaji, hiyo siyo hoja ya msingi, mtu anaweza akawepo humu ndani ama asiwepo lakini wananchi wanahitaji huduma, hiyo ndiyo hoja ya msingi. Hoja kwamba Mbunge atarudi au hatarudi hilo ni suala lingine lakini hoja ni kwamba yeye kama mwakilishi wa wananchi anajaribu kuonesha namna ambavyo ni muhimu sana watu wake kufikiwa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.50 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 19 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*